# Nipashe

Jumatano Juni 26, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579954

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper






UCHAMBUZI:
Kakunda: Serikali iigawe Sikonge kusogeza huduma kwa wananchi
Ukurasa 19

Ukurasa 18
Senate yakataa mauzo ya silaha kwa Saudia Arabia

Kimataifa
Kivuli cha Kabila chazidi kuitesa DRC
Ukurasa 14

siasa
JUMATANO JUNI 26, 2019
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

BAADA YA MIAKA 55
Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano - 2

MZEE Pius Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.
Vilevile, Mzee Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mizizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.
Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu la kuundwa Muungano huo, ameamua kuan-
Endelea 16

Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. PICHA: MTANDAO

Mawaziri wadaiwa kula njama ya kumuua Naibu Rais Ruto
Ukurasa 17

Trump afuta mashambulizi dhidi ya Iran dakika 10 kabla hayajaanza Ukurasa 20

## Muhimbili yajenga ICU maalum ya wajawazito

UKURASA 5

UKURASA 13

# JPM azindua Taifa 'Gas'




**NI** Mihan Gas, sasa kuuzwa kimataifa, ataka bei ya gesi kushuka kuokoa mazingira... *Endelea ukurasa wa 4*



Rais John Magufuli akipeana mikono na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Taifa Gas Tanzania Limited, Rostam Aziz, baada ya kuzindua ghala na mitambo ya gesi ya LPG ya kampuni hiyo Vijibweni, Kigamboni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Neema tele bajeti 2019/20

**Tozo,** kodi dagaa na kampuni zafyekwa, serikali yajitosa kujenga viwanda taulo za kike, viwanda 27 kutaifishwa...*Endelea ukurasa wa 2, 3*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### WAANDISHI WA IPP WANG'ARA TUZO EJAT

WAANDISHI wa habari tisa kutoka vyombo vya habari vya IPP wameingia fainali katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari ...

UKURASA WA 5

### ASASI ZAKUSUDIA KUUPINGA MUSWADA MAHAKAMANI

ASASI za kiraia 300 nchini zimesema endapo muswada wa mabadiliko ya sheria zinazohusu asasi hizo utapitishwa bila kuwashirikisha...

UKURASA WA 7

### MAOFISA WATATU WA SERIKALI WAFA AJALINI

MAOFISA watatu wa serikali wamefariki dunia jana alfajiri kwenye ajali iliyohusisha gari la Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) na lori aina ya fuso mkoani Iringa, huku wengine...

## Mapya yaibuka kesi ya kigogo Takukuru

UKURASA 4

**MICHEZO** AMUNIKE: NI USHINDI TU KWA HARAMBEE STARS UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

# Neema tele bajeti 2019/20, Mpango apangua hoja

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amepangua hoja za wabunge ikiwamo kupinga kurejeshwa kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye taulo za kike katika bajeti ya serikali ya mwaka 2019/20.

Hata hivyo, amesema serikali imeamua kupunguza kiwango cha kodi ya mapato ya kampuni (corporate tax) kutoka asilimia 30 mpaka 25.

Pia alisema serikali itaingia mkataba wa makubaliano ya utekelezaji na kila mwekezaji atanufaika na punguzo hilo la kodi, ambayo itaainisha wajibu wa kila upande, lakini kwa sasa serikali itafuatilia mwenendo wa bei za hizo taulo za kike.

Mpango alitangaza uamuzi huo wa serikali jana bungeni jijini hapa wakati akijibu hoja za wabunge waliochangia mjadala kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2019/20 na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2018/19 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2019/20.

Kwa mujibu wa Waziri Mpango, kodi hiyo iliyopunguzwa kutoka asilimia 30 mpaka 25 kwenye sheria ya kodi ya mapato itatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka ujao wa fedha hadi mwaka 2020/21, kwa wawekezaji wapya na viwanda vinavyozalisha taulo za kike hapa nchini.

Bajeti ya serikali iliyopitishwa kwa ajili ya mwaka ujao wa fedha unaoanza Julai mosi mwaka huu, ni Sh. trilioni 33.1

Kuhusu msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike kwamba urejeshwe na hatua zichukuliwe kuhakikisha wafanyabiashara wa bidhaa hiyo wanawekewa bei elekezi, serikali imetafakari juu ya mapendekezo ya wabunge na kwa kuzingatia maoni na ushauri, anapendekeza mambo matatu.

"La kwanza ni kupunguza kiwango cha kodi ya mapato ya kampuni kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 25 kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka ujao wa fedha hadi mwaka 2020/21 kwa wawekezaji wapya na viwanda vilivyopo vinavyozalisha taulo za kike hapa nchini.

"Lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji katika uzalishaji wa hii bidhaa muhimu sana lakini pia kuongeza ajira na mapato ya serikali. Kwa kuwa hatua ya uwekezaji inaweza kuchukua muda kiasi na ni nia ya serikali kuhakikisha hatua hii inaleta manufaa kwa haraka," alisema.

Vile vile, Waziri Mpango alisema ili kuongeza matumizi ya pamba nchini lakini pia kuzalisha ajira, serikali inakusudia kujenga viwanda vya kuzalisha taulo za kike nchini, kimoja kitajengwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na kingine kitajengwa katika mkoa wa Simiyu.

Alisema hatua ya tatu inabaki ile ile kwamba serikali inafuta msamaha wa VAT uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike kwa kushindwa kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake kuwanufaisha wafanyabiashara.

"Kwa kweli lengo la serikali ni kumnufaisha mtoto wa kike na si wafanyabiashara kujilimbikizia faida. Napenda kusisitiza kwamba dhamira ya serikali ni kuhakikisha bidhaa hiyo muhimu inapatikana kwa bei nafuu, hivyo kuwawezesha watoto wa kike na wanawake kuinunua," alisema.

Alisema yako baadhi ya maeneo mapya yaliyoungwa mkono na wabunge wengi, ikiwamo hatua ya serikali kupunguza au kufuta tozo 54 lakini la pili ni serikali kukutana na wafanyabiashara na kuanza

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akimpongeza Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Phil hoja za wabunge kuhusu Bajeti ya Serikali, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFIS**

## Waziri Mkuu atoa tamko Watanzania kubaguliwa Kenya

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amelieleza Bunge kuwa serikali za Tanzania na Kenya zimelazimika kuingia katika mazungumzo ya kidiplomasia baada ya Mbunge wa Jimbo la Starehe nchini humo, Charles Njagua 'Jaguar', kutoa saa 24 kwa Watanzania kuondoka Kenya.

Majaliwa alitoa tamko hilo bungeni jana jioni baada ya Spika Job Ndugai kuiagiza serikali kuja na majibu ya kuwahakikishia usalama Watanzania wanaoishi Kenya baada ya tamko la mbunge huyo.

Waziri Mkuu aliwataka wabunge na Watanzania kuwa wavumilivu kuhusu kauli iliyotolewa na mbunge huyo wa Kenya licha ya kuwa imebeba chuki na ubaguzi kwa wageni hasa Watanzania.

Alisema serikali imeshalisikia na haijakaa kimya na ilihitaji kwanza kujiridhisha aliyeitoa ana mamlaka yapi.

Majaliwa alisema tayari Balozi wa Kenya nchini ameshaweka wazi kwamba kauli ya mbunge huyo si msimamo wa Serikali ya Kenya.

"Serikali yetu inatambua nchi ya Kenya ni nchi rafiki, ni nchi jirani sana na hata viongozi wetu wakuu wanazungumza lugha moja.

"Na nchi hizi hasa Kenya inapakana na Tanzania kwa mpaka mrefu sana kutoka mkani Tanga mpaka mkoani Mara. Wananchi wa Tanzania na

INAENDELEA UK. 8

## Viwanda taulo za kike kujengwa

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAKATI wabunge na wadau mbalimbali nchini wakipinga pendekezo la serikali kurejesha kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye taulo za kike katika bajeti ijayo ya mwaka 2019/20, serikali imetangaza itajenga viwanda vya kuzalisha taulo za kike kama hatua ya kumwezesha mwanamke kupata bidhaa hiyo muhimu.

Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashantu Kijaji, alisema serikali itajenga viwanda hivyo, alipokuwa akijibu hoja za wabunge waliochangia bajeti ya serikali ya mwaka 2019/20 ya Sh. trilioni 33.1

Alisema viwanda hivyo ujenzi wake utaanza mwaka huu huku akitanabahisha kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa kushirikiana na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) utajenga kiwanda cha taulo hizo mkoani Simiyu.

Dk. Kijaji alisema kiwanda kingine kitajengwa mkoani Pwani na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na vyote vitauza bidhaa hiyo kwa bei rahisi.

"Kukatwa VAT (kodi ya ongezeko la thamani) kwenye taulo za kike, mimi ni mwanamke na nina mchango wangu kwa kila kinacholetwa na Waziri wa Fedha. Naijua kadhia hii haipendezi hata kidogo kwa maneno aliyoelezwa kwa Waziri wa Fedha kwenye Bunge hili. Inapoletwa hoja huwa ni ya serikali na si yake, tusimshambulie naye ni binadamu anaumia," alisema Kijaji.

Aidha, Naibu Waziri huyo alisema si kweli kama inavyodaiwa na baadhi ya wabunge kuwa bajeti hiyo ya Sh. trilioni 33.1 haijakidhi misingi ya kijinsia.

"Watu wanasema bajeti haina misingi ya kijinsia. Nimefanya mapinduzi makubwa kwa afya ya wanawake. Tumepeleka Simiyu Sh. bilioni 4.5 kujenga hospitali kwenye halmashauri zake ili wanawake wapate huduma za afya. Tumepeleka Geita Sh. bilioni tatu kwa mwaka mmoja. Kanda yote ya Ziwa tumepelekwa Sh. bilioni 22," alisema.

Naibu Waziri huyo pia alisema baada ya kuondoa VAT kwenye taulo za kike, serikali ilifanya utafiti kwa kushirikiana na Tume ya Ushindani nchini (FCC) na Wizara ya Viwanda na Biashara.

"Tulichokibaini kwanza wanawake wengi hawajui kama kodi hiyo imeondolewa, pia bei haikupungua, taulo iliyouzwa 2,500 bado iliuzwa kwa bei hiyo hiyo. Lakini baada ya kuondolewa kwa kodi, viwanda vya ndani vilipunguza uzalishaji wa bidhaa.

"Hatua hiyo iliondoa ajira za vijana walioajiriwa kwenye viwanda vya ndani. Hii ni bidhaa muhimu, unapokuwa na bidhaa hii hauwezi kukabiliana nayo kwa hatua za kikodi pekee," alisema.

Kuhusu kufungwa biashara nchini, alisema tangu bajeti ya kwanza, Waziri wa Fedha na Mipango aliwaelekeza maofisa wa TRA kutofunga biashara bila kufuata taratibu.

"Soko huria moja ya sifa ni uhuru wa kuanzisha na kufunga biashara. Tukiangalia wengi waliofunga si kwa sababu wamelazimishwa kufunga biashara. Kwenye uchumi wa soko huria, ifahamike biashara inaweza kufungwa kwa sababu mbalimbali.

Alizitaja sababu hizo: "Inaweza kuwa kubadilisha aina ya biashara, ushindani, kushindwa kuisimamia biashara husika au wameshindwa kuelewana kwa wanahisa, mzigo wa madeni kwenye taasisi za kifedha au kodi.

Alisema hawezi kuvumilia kuona wafanyabiashara wanashirikiana na watumishi wa serikali kukwepa kodi.

Alisema Mei hadi Aprili mwaka huu, zaidi ya watumishi 30 wa TRA wamesimamishwa kazi.

"Aprili 19, mwaka huu, nilipokea vijana watatu ofisini kwangu kulalamika wamepewa makadirio makubwa ya kodi, nilipoanza kuifuatilia ilikuwa maroli manne ya tani 10 yaliyobeba vitenge kutoka China. Yamepita Bandari ya Dar es Salaam, kwenda Uganda ambapo yalionekana yamepita kwenye mpaka wa Mtukula, lakini hawakuwa na nyaraka kuonyesha kama yametokaje Uganda.

"Nilichokibaini waliokuja wale vijana walikuwa madalali wakishirikiana na maofisa wa TRA, waliokusanya kodi halali kutoka kwa wafanyabiashara. Kama hilo ndio linalotafsiriwa Ashantu (Kijaji) anasimamia kufungwa biashara, sitaruhusu Watanzania waibiwe, nitahakikisha kodi zinakusanywa kulingana na sheria zilizopitshwa na Bunge," alisititiza Naibu Waziri Kijaji.

## HABARI ZA BAJETI



lip Mpango na Naibu wake, Dk. Ashatu Kijaji (kulia), baada ya waziri wa fedha na naibu wake kujibu
SI YA WAZIRI MKUU

# Spika aonya wanaochokonoa Muungano

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema hatakubali Bunge la 11 kuwa chanzo cha kusababisha ufa na ataongeza umakini kufuatilia michango yenye kuhatarisha Muungano.

"Uhodari wa kuunajisi Muungano kwa maneno machafu ili kupata umaarufu wa kisiasa, tusikubali. Tunakubali Serikali ya Zanzibar ina bajeti yake, mpango wake wa maendeleo na ilani ya chama. Tunafahamu yote yanahitaji rasilimali kutekelezwa na serikali ya Muungano tunapaswa kuhakikisha rasilimali hizo zinapatikana ili yote yatekelezwe," alisema.

Spika Ndugai alitoa mwongozo huo jana, baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Januari Makamba, kueleza masikitiko yake kuhusu michango ya baadhi ya wabunge kuhusu masuala ya Zanzibar.

"Naungana na wewe (Makamba), hatutaruhusu Bunge kuwa sehemu ya kuanzisha cheche zitakazowasha moto kuunguza nchi yetu. Tutaongeza umakini kufuatilia na kusikiliza kuhakikisha mambo hayo hayatokei tena. Bila Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hata Bunge halitakuwapo, kazi yetu ni kulinda," alisema Ndugai.

Wakati Waziri Makamba anajibu hoja za wabunge waliochangia mjadala wa hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2018 na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2019/20 pamoja na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2018/19 na mapendekezo ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2019/20, alisema Muungano ulivyozungumziwa kwenye mchango ya baadhi ya wabunge kuna maneno yaliyojenga na kubomoa.

Alisema baadhi ya lugha zilizotumika hazichangii kujenga Muungano kwa kuwa zimetuhumu, kutusi na kuleta fedheha kubwa. "Naomba kwa heshima ya Bunge na nchi, kwa dhana ya kuhimiza umoja na mshikamano umefika mahali maneno ya aina hiyo yasitumike katika bunge letu. Baadhi ya michango imedai kunukuu bajeti iliyosomwa Zanzibar kuwa Waziri (Philip) Mpango na serikali ya Tanzania ina roho mbaya, wivu na chuki kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kugoma kutekeleza mambo ya maendeleo ya Zanzibar.

"Hayo maneno kama yalivyonukuliwa kuwa yalisemwa kwenye bajeti ya Zanzibar, si kweli kwani nilikuwapo wakati bajeti hiyo ikisomwa. Ilisomwa kwa staha na umakini. Tusiwatie maneno viongozi wa Zanzibar, kujenga hoja ya maeneo yenye kutaka kuvuruga Muungano.

Waziri Makamba alisema mchango uliotolewa na Mbunge Mohammed Amour ulikuwa na maneno ambayo si mazuri na kuwafanya baadhi ya wabunge kuvumilia kutohamaki.

# Kilio wavuvi, wauza dagaa chasikika

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

HATIMAYE serikali imesikia kilio cha wavuvi na wafanyabiashara wa dagaa nchini kuhusu tozo ya ushuru wa uvuvi wa dagaa (export loyalty) iliyokuwa ikitozwa kwa Dola za Marekani 0.5, baada ya kuamua kuishusha hadi kufikia Dola 0.3

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luaga Mpina, amesema serikali imerekebisha na kwa kukubali ushauri wa wabunge wa kutaka serikali iondoe mkanganyiko uliopo kati ya wafanyabiashara wa dagaa wanaovuliwa baharini na wanaovuliwa kwenye maziwa kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi.

Mpina alikuwa akijibu hoja za wabunge kuhusu kodi hiyo iliyokuwa ikitozwa katika ukanda wa Pwani, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria.

"Ukija kwenye suala la tozo ni kwa nini iwe kwenye uvuvi, ni kweli kabisa kwamba dagaa walikuwa wanatozwa Dola 1.5 za Marekani. Sasa nataka ni waambie hivi, tumerekebisha. Serikali imesikia kilio cha wavuvi na imekubali pia ushauri wa wabunge, tumepunguza kodi kutoka 0.5 mpaka 0.3. "Kwa Ziwa Nyasa tumepunguza vile vile kutoka Dola za Marekani 0.5 mpaka 0.3 na Ziwa Tanganyika tumepunguza kutoka Dola 1.5 mpaka Dola moja. Sababu nyingine ni kwa nini hizi tozo zinatozwa tofauti kila eneo ni kwa sababu ya ahitaji ya kila eneo. Dagaa wa Ziwa Tanganyika huwezi kuwafananisha na dagaa wa Ziwa Victoria na dagaa wa pwani," alisema.

Dagaa wanaotoka ukanda wa pwani tozo yake kabla ya serikali kuja na uamuzi huo ilikuwa ni Dola za Kimarekani 1.5 kwa kilo moja, sawa na Sh. 3,400 wakati huo tozo ya dagaa wanaotoka kwenye maziwa ilikuwa ni Dola za Kimarekani 0.16 kwa kilo moja sawa na Sh. 360 kwa kilo moja.

Zamani ushuru wa kusafirisha nje ya nchi dagaa hao hao wa pwani ulikuwa Sh. 300 kwa kilo, lakini serikali ilipandisha hadi Sh.3,400.

Mpina pia alisema sekta ya mifugo na uvuvi inaajiri takribani asilimia 50 ya Watanzania na inachangia asilimia 6.9 kwenye pato la taifa. Shughuli za uvuvi zinachangia asilimia 2.2 ya pato la taifa.

Katika michango yao kuhusu sekta hiyo, wabunge walieleza kuwa baadhi ya maeneo ya nchi uvuvi ndiyo shughuli kuu ya uchumi wakitolea mfano wa asilimia 30 ya wakazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji wanaoishi kwa kutegemea shughuli za uvuvi.

Hata hivyo, walisema bado serikali haijafanya uwekezaji wa kutosha ili kuifanya sekta hiyo kuwa chanzo cha uhakika cha mapato ya serikali.

# Viwanda vya nguo sasa kutaifishwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amesema serikali itavirejesha viwanda vyote vya nguo vilivyobinafsishwa, baada ya 32 vilivyokuwapo nchini kubakia vitano pekee ambavyo vinafanya kazi kwa sasa.

"Viwanda vya nguo nchini vilikuwa 32 sasa hivi vimebakia tano ambavyo vinafanya kazi. Wengi wamekiuka mikataba ile ambayo walitia saini kwa mujibu wa ubinafsishaji. Nataka kuhakikisha viwanda hivi vinaanza kufanya kazi ili wakulima wa pamba tusitegemee tu ginnery (viwanda vya kusindika pamba) kama soko peke yake.

"Sasa tunaanza kwenda kwa vitendo kwa kuhakikisha mkulima anapovuna shamba, soko lingine linakuwa ginery na zingine zinaenda kwenye viwanda ili kutengeneza pamba nyuzi na wakulima wetu wapate soko la uhakika," alisema.

Bashungwa alisema hayo jana alipokuwa akijibu hoja za wabunge walioigusa wizara yake wakati wa mjadala kuhusu hali ya uchumi wa taifa kwa mwaka 2018 na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2019/20 pamoja na tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2018/19 na mapendekezo ya mapato na matumizi ya serikali kwa mwaka 2019/20 ya Sh. trilioni 33.1

Ili kurejesha viwanda hivyo, alisema serikali inafungua fursa za masoko za kimataifa kwa kushiriki mikutano mikubwa kama 'World Economic Forum' kwa kuhakikisha inashirikiana na balozi za Tanzania nje ya nchi kutafuta masoko ya uhakika duniani.

Kuhusu kukosekana kwa masoko ya uhakika kwa wakulima wa pamba na korosho, alisema Rais John Magufuli ana nia njema ya kuunganisha kilimo na viwanda kwa sababu kufanya hivyo kutawainua wakulima wengi nchini kwenda kwenye uchumi wa kati. Kwa mujibu wa Waziri Bashungwa, kuendelea kutegemea viwanda vya kusindika pamba kama soko la wakulima, hakutawawezesha kutoka kwenye mkwamo wa bei ambao umesababisha kushindwa kupanda.

Kutokana na ukweli huo, alisema serikali imeazimia kuhakikisha viwanda ambavyo vilibinafsishwa lakini havifanyi kazi, baada ya Bunge ataanza navyo.

Kuhusu soko la korosho, Waziri Bashungwa alisema kumekuwa na upotoshaji mkubwa ambao umesababisha dunia kuamini kwamba korosho ya Tanzania haifai na imeoza, wakati si kweli.

Alisisitiza kuwa baada ya kuapishwa, alikwenda ghala kwa ghala na kukuta korosho ziko katika hali nzuri na kwamba hakuna korosho ambayo ni mbovu.

## Waandishi wa IPP wang'ara tuzo EJAT

**Na Elizabeth Zaya**

WAANDISHI wa habari tisa kutoka vyombo vya habari vya IPP wameingia fainali katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2018 zinazoandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT). Waandishi wa habari hao ni miongoni mwa 81 waliofanikiwa kuteuliwa kuingia hatua ya mwisho ya tuzo hizo kati ya 644 waliokuwa wamejitokeza kushiriki kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchi nzima.

Idadi hiyo (81) ni sawa na ongezeko la wateule 27 ikilinganishwa na wateule 57 wa tuzo hizo mwaka 2017.

Walioteuliwa kutoka IPP kuingia katika hatua ya mwisho ya tuzo hizo ni Sanula Athanas, Elizabeth Zaya, Salome Kitomari, Rahma Suleiman, Marco Maduhu, Ashton Balaigwa (wote Nipashe), Felister Peter, Aisia Rweyemamu (The Guardian) na Joseph Mwambije (ITV). Akitangaza majina ya wateule hao jana jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya EJAT, Kajubi Mkajanga, alisema kutangazwa kwa wateule hao kumefanyika baada ya jopo la majaji saba ambao ni wataalamu wa masuala ya habari, kukamilisha kazi ya kupitia na kuchagua kazi zenye ubora zaidi iliyofanyika kuanzia Juni 13 hadi 19, mwaka huu.

Alisema jopo hilo la majaji lilipitia kazi za kiuandishi 644 zilizowasilishwa kwenye makundi ya kushindaniwa 20 kwenye tuzo hizo.

Mukajanga alisema katika awamu hii kumekuwapo na mwitikio mkubwa ikiwamo kuongezeka kwa wateule katika upande wa runinga kutoka wateule 15 wa mwaka 2017 hadi wateule 20 wa mwaka 2018.

Alitaja eneo lingine ambalo limeongeza wateule kuwa ni upande wa radio ambao wameongezeka kutoka 11 mwaka 2017 hadi 20.

Kwa upande wa magazeti, alisema wateule wameongezeka kutoka 19 mwaka 2017 hadi kufikia wateule 46. Alisema idadi ya wateule wanawake pia imeongezeka kutoka 24 mwaka 2017 hadi 34. Alisema hafla ya utoaji wa tuzo hizo itafanyika Juni 29, mwaka huu, huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Profesa wa Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chris Peter.

Mwenyekiti wa Jopo la Majaji wa EJAT 2018, Kiondo Mshana, aliwataka waandishi wa habari kuendelea kuboresha kazi zao kuhakikisha zinakamilika na kuzaa matunda.

# JPM azindua Taifa Gas

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amezindua ghala la mitambo ya gesi ya mitungi inayotumika kupikia (LPG), inayomilikiwa na Kampuni ya Taifa Gas Tanzania, jana Wilaya ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam na kuwataka wasambazaji kupunguza gharama za mitungi ya gesi ya kupikia sokoni.

Vilevile, amempongeza mfanyabiashara Rostam Azizi kwa uwekezaji huo mkubwa na kuwahimiza Watanzania hususani wa Dar es Salaam ambao kwa siku hutumia magunia ya mkaa 40,000, wabadilike na kutumia nishati hiyo.

Kampuni hiyo ambayo ni mmiliki wa gesi ya mitungi ya Mihan, sasa inapanua biashara hiyo ya gesi nje ya mipaka kwa kuuza katika nchi za Afrika zikiwamo za Afrika Kusini, Rwanda, Kenya, Uganda, Burundi, DRC na Sudan ya Kusini kwa kulitangaza jina la Taifa.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo, Rais Magufuli alisema amefurahi kusikia Taifa Gas imeanza kutengeneza na kukarabati mitungi yake yenyewe na matarajio yake ni kuwa itashusha bei ya mitungi na kuhamasisha wananchi kutumia gesi zaidi.

"Ikiwezekana mfanye kama vile wanavyofanya kampuni za soda na bia. Ukinunua kwao soda au bia maana yake hulipii kreti," alisema na kuongeza:

"Ninafahamu matumizi ya gesi asilia yameongezeka takribani viwanda 40 na nyumba 500 zimeunganishwa na zaidi ya magari 200 yanatumia gesi, hii inafanya matumizi ya gesi kwa bomba letu kuongezeka kutoka asilimia tano mwaka 2015. "Ukusanyaji mapato umeongezeka, mwaka huu wa fedha unaoishia mlipangiwa kukusanya Sh. bilioni 394 hadi Mei 2019 mlikusanya Sh. bilioni 484," alisema.

Magufuli alitoa wito kwa wananchi hususani wa Dar es Salaam ambao kwa siku hutumia magunia ya mkaa 40,000 sawa na inayopatikana nchini, wabadilike na kuanza kutumia gesi.

"Nikilinganisha na gesi, mkaa ni gharama, magunia mawili ya mkaa maeneo mengi yanaweza kugharimu Sh. 120,000 kwa mwezi, lakini familia hiyo kwa mwezi inaweza kutumia mtungi mmoja wa gesi wenye kilo 15 ambao gharama yake ni Sh. 47,000 hata ikiwa miwili bado ni 94,000," alisema.

AMMWAGIA SIFA ROSTAM

Rais Magufuli alisema anaiona Kigamboni mpya inakuja na kwamba alichokifanya mfanyabiashara Rostam ndicho anachokitaka kwa sababu hapendi wawekezaji wa maneno maneno.

"Umeonyesha na hii imenipa nguvu sana tafuta wawekezaji wengine hata 10 au 20 tu wenye moyo wa namna hii wa kuwekeza, tutawasaidia wawekezaji," alisema na kuongeza:

"Tunahitaji wawekezaji wa ukweli, waje wasikilize maneno ya wale ambao hawatutakii mema, waje wawekeze tutawasaidia, tunataka wanapowekeza serikali kupitia wananchi wake nao wafaidike, nawashukuru wawekezaji wengine

INAENDELEA UK.26

## Shahidi adai Gugai alikabidhiwa hati ya viwanja 12

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeambiwa na Msajili Msaidizi wa Ardhi kutoka Kanda ya Ziwa, Aivan Amulike (35), kwamba Mhasibu Mkuu wa zamani wa Takukuru, Godfrey Gugai, anamiliki viwanja Mwanza na Simiyu.

Pia, alidai kuwa anamfahamu Gugai kwa sababu ni mteja wao na alimilikishwa vipande vya ardhi na Msajili wa Ardhi Kanda ya Ziwa na alikabidhiwa hati za viwanja 12 mwaka 2017.

Ushahidi huo ulisikilizwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Awamu Mbwagwa.

Shahidi huyo wa 13 alidai kuwa Msajili Msaidizi aliyestaafu, Magreth Mziray, alimkabidhi majalada ya hati za viwanja 12 mwaka 2017, ikiwamo majalada ya viwanja viwili vilivyopo mkoani Mara na Simiyu na majalada 10 yako jijini Mwanza. Akifafanua alidai kuwa jalada la hati ya kiwanja namba 230, kitalu B Nyegezi, alianza kukimiliki tangu mwaka 2015 na alikinunua kutoka kwa Ibrahimu Marijani kwa Sh. 44,000,000 na alilipia na usajili wa Sh. 112,000. Viwanja vingine ambavyo alinunua ni namba 713, kitalu B Kiseke - Mwanza, ambacho alikinunua kutoka PPF kwa Sh. 31,315,037, viwanja namba 471, 472 na 473, kitalu C Nyegezi, alinunua kwa Sh. milioni 92 katika mnada na kiwanja namba 438, kitalu D Nyegezi - Mwanza, alikinunua kwa Sh. milioni 58 katika mnada wa CRDB.

Alitaja viwanja vingine vya Gugai ambavyo alikuwa mmiliki wa kwanza kuwa ni kiwanja namba 297, kitalu 2, Nyamgongoro - Mwanza, 296 kitalu 2, Nyamgongoro Mwanza, 90 kitalu 5, Bugalika - Mwanza, 439 kitalu D, Nyegezi, Mwanza, 277 kitalu 2, Nyamgongoro, Mwanza na kiwanja namba 275 Kitalu 2 Nyamgongoro, Mwanza.

Akihojiwa na wakili wa utetezi, Alex Mgongolwa, alidai majalada hayo alikabidhiwa na kufahamishwa kwamba yana kesi na kwamba aliwahi kuhojiwa na mpelelezi wa kesi hiyo, lakini hamkumbuki jina lake.


*Jipatie Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro kwa Bei Elekezi za Rejareja kama Ifuatavyo:-*

- Nusu Lita (500ml) – TSHS. 500/=
- Lita Moja na Nusu (1.5L) – TSHS. 1,000/=
- Bei Hizi Elekezi ni Kwa Nchi Nzima
- Maji ya Kunywa ya Kilimanjaro ni Maji ya Kuaminika Kila Siku



## HABARI KITAIFA

# Muhimbili yaanzisha ICU maalum ya wajawazito

**Na Beatrice Shayo**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH) imesema katika kupunguza vifo vya kinamama vinavyotokana na kifafa cha mimba imetengeneza chumba mahususi cha huduma ya uangalizi maalumu (MAICU).

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya kinamama na uzazi, Dk. Vicenti Tarimo, kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji, alisema MAICU ina vitanda 10, mashine tano za kusaidia kupumua na kipimo cha ultrasound.

Alisema kinamama wanaohitaji huduma hiyo inapatikana katika jengo lao, huduma hiyo awali ilikuwa ikitolewa chumba cha ICU ya kawaida iliyopo umbali wa mita 150 hali iliyokua inahatarisha uhai wa mama na mtoto.

Dk. Tarimo alisema maisha ya kinamama wengi yameokolewa kupitia MAICU.

Pia, alisema uwapo wa MAICU umesaidia kupunguza vifo vya kinamama na kwa mwaka 2017/2018 vilikuwa 125 ilipoanzishwa Julai mwaka 2018 hadi Juni 2019 vifo hivyo vimeshuka hadi kufikia 86.

Alisema tatizo kubwa lililojitokeza katika vifo hivyo ni kuwapo kwa kifafa cha mimba na kinamama kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua.

Dk. Tarimo alisema hospitali inaendelea kuchangia na kutekeleza malengo ya serikali pamoja na malengo ya milenia ya kupunguza vifo vya kinamama.

"Hospitali ina ICU ya watoto wachanga (NICU) yenye vitanda (18), watoto kuanzia mwezi mmoja PICU yenye vitanda (12), wagonjwa wa tiba (MICU) yenye vitanda (15), wagonjwa wa upasuaji (SICU) yenye vitanda (18), wagonjwa wanaopandikizwa figo vitanda (5) na kinamama wajawazito (MAICU) yenye vitanda (10)," alisema.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO), linazitaka hospitali kuwa na asilimia 10 ya vitanda vya ICU.

Alisema MNH ina vitanda 1,550 hivyo inatakiwa kuwa na vitanda 155 vya ICU kwa sasa ina vitanda 78 sawa na asilimia 50 ya takwa la WHO. Hizi ni jitihada kubwa za uboreshaji huduma kwa wananchi.

Vilevile, alisema kwa upande wa mafunzo na utafiti serikali kupitia Wizara ya Afya inaweka mikakati mbalimbali ya kuboresha ICU katika hospitali za rufani na mikoa.

Alisema hospitali hiyo imefanya ukarabati mkubwa wa wodi tatu hadi sita za Mwaisela na kuweka mfumo wa oxygen pamoja na vitanda saba kila wodi sawa na vitanda 28 vya kutoa huduma kwa wagonjwa maalumu (HDU).

Naye Mkuu wa Idara ya Ukunga na Uzazi, Dk. Mugara Mahunguruo, alisema ICU ya kinamama imesaidi kupunguza vifo vya uzazi.

# Asasi zakusudia kuupinga muswada mahakamani

**Na Beatrice Shayo**

ASASI za kiraia 300 nchini zimesema endapo muswada wa mabadiliko ya sheria zinazohusu asasi hizo utapitishwa bila kuwashirikisha watakwenda kuupinga mahakamani.

Asasi hizo zimesema mchakato wa uwasilishwaji wa muswada huo umekuja kwa hati ya dharura hivyo haukuwa na ushirikishwaji wa wadau, hivyo wamependekeza mchakato huo usitishwe na badala yake wadau washirikishwe ili kupata maoni yao.

Akisoma tamko hilo kwa niaba ya asasi hizo, Mratibu wa Kituo cha Utetezi wa Mtandao wa Haki za Binadamu nchini (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema muswada uliopelekwa bungeni unakwenda kuua asasi za kiraia.

Alisema muswada huo umezua sitofahamu na taharuki kwa azaki ambao ni walengwa wakuu kwenye muswada huo.

"Miongoni mwa sheria hizo ni ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2002, Sheria ya Jumuiya za Kijamii, Sheria ya Mabaraza ya Wadhamini na Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2002. Sheria hizi ni miongoni mwa sheria kuu zinazoongoza asasi za kiraia nchini," alisema.

Olengurumwa alisema uchambuzi walioufanya na asasi za kiraia zaidi ya 170, muswada huo ukipitishwa utaleta changamoto nyingi katika utekelezaji na uendeshaji wa azaki.

Alisema miongoni mwa changamoto hizo ni kuminya kwa uhuru wa azaki nchini kinyume cha Katiba pamoja na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.

Alisema msajili amepewa mamlaka makubwa bila kudhibitiwa namna ya kusimamia Azaki ikiwa ni pamoja kufuta usajili pasipo kufuata utaratibu wa kisheria.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Usawa kwa Wasichana (EFG), Jane Magigita, alisema kutokana na changamoto walizoziona ni vizuri Bunge likafanya maboresho na kufuta vipengele vinavyoathiri Azaki za nchini.

"Tunawaomba wabunge kuusoma kwa umakini na kuuelewa ili watakapokuwa ndani ya Bunge watoe mapendekezo ya kurekebisha vipengele vyote vinavyoathiri azaki nchini," alisema.

Magigita alisema wanaomba muswada huo uondolewe kwenye hati ya dharura na kushirikishwa katika hatua zote.




FSSP
Field Support Services Project | Tanzania

**CONSULTANCY POSITION FOR GENDER EQUALITY TECHNICAL SPECIALIST TO SUPPORT THE GOVERNMENT OF CANADA (GLOBAL AFFAIRS CANADA)**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide consultancy services as the Gender Equality Technical Specialist under the Global Affairs Canada-funded Field Support Services Project (FSSP) Tanzania.

The specialist will provide analysis and advice on the planning, design, management, monitoring and coordination of the Government of Canada's development assistance programming and policy dialogue in Tanzania (among other tasks).

Launched in June 2017, Canada's Feminist International Assistance Policy recognizes that supporting gender equality and the empowerment of women and girls is the best way to build a more peaceful, inclusive and prosperous world. **The Gender Equality Technical Specialist will pay an integral role in the implementation of Canada's Feminist International Assistance Policy in Tanzania.**

Candidates will be evaluated based on the following key qualifications and experience:

i. Bachelor's degree from a recognized university. A qualification higher than a bachelor degree will be an added advantage.
ii. A minimum of 4 years of professional work experience as technical expert and advisor on gender equality, of which at least two years are in relation to international development work in developing countries, preferably Tanzania or East Africa region.
iii. Experience providing gender equality technical advice and support on complex international development programs and projects in one or more of the following sectors: education, health, inclusive economic growth and inclusive governance.
iv. Experience in providing written gender equality analysis and comments on program/project proposals, implementation plans, progress reports and evaluations.
v. Experience in engaging in technical forums and policy dialogue on gender equality issues with development partners and government officials.
vi. Experience in carrying out research and analysis of systemic and emerging gender equality issues and trends.
vii. Knowledge and deep understanding of gender equality and empowerment of women and girl's issues in Tanzania

The following skills and competencies, while not essential, are assets for the work to be performed. Candidates should demonstrate them to the extent possible:

- Strong research, analytical and writing skills
- Strong skills in leadership, teamwork, networking, coordination and intercultural communication
- Advanced professional proficiency in English
- General professional proficiency in Kiswahili

**Strong candidates will be offered a competitive rate.**

Interested candidates should obtain a detailed description of these services by sending request email to **procurement@fssptz.org** specifying in the requests as follows: **"Consultancy position for FSSP Gender Equality Technical Specialist."**

Requests for further information will be received up to three working days prior to the **last submission date, 12 July 2019.** Any request received later than that may not be responded to.

**FSSP Manager**

215293702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hukumu kali zitasaidia kudhibiti ujangili wa wanyamapori nchini

**TANZANIA** inatajwa kuwa miongoni mwa nchi za Afrika inayotoa hukumu kali kwa wanaokutwa na hatia ya kuhusika na ujangili wa wanyamapori na maliasili, ikiwa na lengo la kumaliza ujangili nchini.

Kabla ya kuimarishwa kwa ushirikiano baina ya taasisi za umma, idara za serikali na sekta binafsi katika vita dhidi ya ujangili, Tanzania ilitajwa kuwa na idadi kubwa ya tembo na faru waliouawa. Hiyo ilisababishwa na kila aliyekamatwa na kufikishwa mahakamani ushahidi uliharibiwa kwa nguvu ya fedha. Kuanzia miaka ya 2012 hadi 2016, tembo wengi waliuawa na meno yao kuchukuliwa, huku faru wakiwa miongoni mwa wanyama walio hatarini kutoweka kutokana na kushamiri kwa biashara ya ujangili, ambayo soko lake kubwa ni China.

Kutokana na hali hiyo, hadi sasa takwimu za faru ni siri na wanalindwa kwa gharama kubwa, ikiwamo kuwekewa vifaa maalum vya kutoa taarifa wanapokaribiwa na hatari.

Kwa kipindi hicho chote, kesi za wanyamapori hazikuhukumiwa kwa adhabu kali kutokana na sababu mbalimbali, kubwa ikiwa ni kukosekana kwa ushirikiano na sauti moja kwa mamlaka husika, huku wahusika wakiwa ni wenye nafasi kubwa serikalini na kwenye taasisi za wanyamapori.

Tangu kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano imechukua hatua mbalimbali za kulinda maliasili ikiwamo kuimarisha kikosi kazi cha Kikosi kazi cha Taifa cha Kuzuia Ujangili, ambacho hupambana na ujangili wa ngazi zote kuanzia ya kwanza hadi ya tano hadi juu, tofauti na miaka ya nyuma ngazi ya nne na tano ambayo ni watu wenye maamuzi na watunga sera waliachwa.

Kazi kubwa imefanyika kuleta pamoja mamlaka zote, ikiwamo kuwapa mafunzo majaji na mahakimu juu ya rasilimali za wanyamapori, na kwa sasa kuna mafunzo yanayoendelea kwa njia ya mtandao ikiwamo kushirikisha Chuo cha Mahakama Lushoto.

Kesi ya kwanza kuhukumiwa mwaka 2017 ni ya Boniface Maliango maarufu kama Shetani, aliyehukumiwa miaka 12, ambaye anadaiwa kuua tembo zaidi ya 1,000 na kuwa na mtandao wa ujangili katika nchi mbalimbali za Afrika.

Kesi nyingine mwaka 2018 ni ya raia wa China Yang Feng Glan maarufu kama Malikia wa Tembo, alihukumiwa miaka 17 jela kwa kuwa mfadhili mkuu wa mtandao wa ujangili Afrika, ambaye ilisambaratisha mtandao wa ujangili.

Hii ni habari njema kwa sekta ya utalii ambayo inaongoza kwa kuingiza fedha za kigeni kwa asilimia 25, kuchangia pato la taifa kwa asilimia 17.2, imeajiri zaidi ya watu 600,000 na ajira zisizo rasmi ni milioni 1.4. Kwa mwaka 2018 pekee watalii waliingia nchini ni milioni 1.5 ambao waliingizia nchi Dola za Marekani bilioni 2.4, huku asilimia 28 ya mapato yakipatikana kutokana na Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro (Kinapa).


Tunaipongeza serikali kwa jitihada hizi kubwa ambazo zimerejesha heshima ya nchi na utalii utaendelea kuingiza fedha nyingi kwa taifa, na kuzitaka mamlaka husika kuendelea na jitihada hizo bila kuchoka.

Hii inaonyesha kuwa iwapo kutakuwa na nia ya dhati kwa kila mamlaka kushirikiana kwenye jambo fulani mafanikio ni makubwa zaidi kuliko kila ngazi kufanya kazi yenyewe.

Tumeona kwenye jambo hili mafanikio ya kujivunia, na sasa viongozi wa taasisi za wanyamapori waliokuwa wanyonge sasa wanatembea kifua mbele, tofauti na awali kesi nyingi ziliishia njiani kutokana na kukithiri kwa rushwa, utakatishaji fedha na mengineyo. Tunawashauri wote wenye dhamana katika kusimamia rasilimali za taifa hususan za wanyamapori pamoja na mahakama zetu kutanguliza mbele uzalendo katika utekelezaji wa majukumu yao, na hii itawezesha nchi yetu kuendelea kuwa mfano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Hatua zichukuliwe sasa dhidi ya mabadiliko ya tabianchi

Na Jenifer Gilla

**YUMKINI** mabadiliko ya hali ya hewa ni tishio kubwa kwa maisha ya binadamu kwa sababu yanaleta uharibifu kwa maisha ya watu na mali zao, hasa kwenye nchi zinazoendelea ambapo uwekezaji katika sayansi na teknolojia ni duni na idadi kubwa ya watu ni maskini.

Kwa sababu ya uharibifu unaotokana na majanga ya asili kama vile mlipuko baharini, ukame, mafuriko na magonjwa yaliyo na uhusiano wa moja kwa moja na mabadiliko ya hali ya hewa, serikali mbalimbali kupitia Umoja wa Mataifa (UN) zimekusanyika pamoja nchini Ujerumani ili kuweka mikakati ya kuzuia athari hizo.

Kwa sababu nyingi ya vyanzo vya mabadiliko ya hali ya hewa ni za kibinadamu ni muhimu kwamba serikali ziunganishe mipango yao ya maendeleo ili kukabiliana na mabadiliko haya ya hali ya hewa.

Vyanzo vya mabadiliko haya ya hewa tunayoyashuhudia yanachangizwa pamoja na mengine masuala kama ya ukataji miti, matumizi ya mimea kama chanzo cha nishati kwa kaya, uzalishaji wa viwanda ambao hutoa hewa ukaa (carbon dioxide) katika anga.

Maafa yaliyotokea nchini Msumbiji mwaka huu wakati kimbunga Idai kilipoipiga nchi hiyo, yanaweza kuzuiwa iwapo kuna mipangilio bora na ya uhakika na hasa ndani ya mipango mbalimbali ya maendeleo ya serikali.

Muungwana ana maoni kwamba serikali zinapaswa kuhamasisha uwekezaji katika vyanzo vya nishati safi zinazojumuisha nishati ya jua na upepo.

Nishati zitokanazo na vyanzo hivi ni mbadala wa zile zitokanazo na mafuta kama ya petroli, dizeli, mafuta ya taa, kuni na makaa ya mawe ambayo hutoa hewa ukaa inayoharibu safu ya ozoni.

Safu hii ya ozoni inahusika kulinda ardhi dhidi ya miale mikali ya jua moja kwa moja na hivyo kuzuia athari mbalimbali ambazo zingeweza kuleta maafa.

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), mabadiliko ya hali ya hewa yanaathiri mamilioni ya watu.

UNFCC inabainisha kwamba kama hatua za kukabiliana na hali hii mbaya hazitachukuliwa, kuna hofu kwamba baadaye dunia na kwa maana hiyo mataifa mbalimbali itashuhudia uharibifu zaidi.

Kwamba athari zake zitakumba dhahiri visiwa, wanyama na mimea na kuna uwezekano wa kutoweka kabisa na hivyo kuhatarisha maisha ya binadamu.

Hivyo basi katika mipango mbalimbali ya kimataifa, kitaifa na kwa maana hiyo Tanzania, tahadhari inapaswa kuchukuliwa kwa kuingiza suala la mabadiliko ya hali ya hewa na hatua stahiki za kuchukuliwa ili kulinda maisha ya watu kwa maana ya kulinda afya ya binadamu na mazingira.

Kama nilivyoosema hapo juu umuhimu wa kudhibiti mabadiliko ya hali ya hewa una maslahi mapana katika kukamilisha mipango mbalimbali ya maendeleo ya nchi na ndiyo maana chini ya UNFCCC, nchi zinahitajika kupunguza uzalishaji wa kaboni utokanao na sababu mbalimbali lakini hasa hasa viwanda.

Mataifa makubwa ya viwanda kama vile China na Marekani yanahitajika kuwekeza katika vyanzo vya nishati safi ili yaweze kupunguza uchafuzi wao mkubwa ambao ingawa nchi zao pia zinakabiliwa na athari, ni nchi maskini kama vile Tanzania na Msumbiji ambazo zinaathirika zaidi.

Na ni watu wa kipato cha chini katika nchi hizi maskini ambao wanaathirika zaidi kutokana na hali duni ya makazi yao, lakini pia hata miundombinu katika makazi yao ni duni ukiacha hali nzima ya mazingira katika makazi yao kwa ujumla wake.

## HABARI KITAIFA

# Maofisa watatu wa serikali wafa ajalini

**George Tarimo,** IRINGA

MAOFISA watatu wa serikali wamefariki dunia jana alfajiri kwenye ajali iliyohusisha gari la Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) na lori aina ya fuso mkoani Iringa, huku wengine wawili wakijeruhiwa.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Iringa, Juma Bwire (pichani), alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea saa 11:45 alfajiri maeneo ya Kata ya Izazi Tarafa ya Isimani wilayani Iringa barabara kuu ya Iringa -Dodoma.

Bwire alisema ajali hiyo ilihusisha gari lenye namba za usajili STL.3807 aina ya Toyota Hilux mali ya Tarura ambalo lilikuwa ikiendeshwa na Lodrick Richard Urio (35), mkazi wa jijini Dar es Salaam likitokea Iringa kwenda Dodoma na kugongana uso kwa uso na fuso namba za usajili T.146 BAZ, mali ya Wilson Msenga, mkazi wa Iringa.

Lori hilo lilikuwa linaendeshwa na dereva aliyetambulika kwa jina moja Amos, mkazi wa Iringa likitokea Dodoma kwenda Iringa.

Bwire aliwataja waliofariki ni Urio (dereva wa Tarura), Joyce Enezar Mlay (45) na JamadiJn Mikata (32), wote wafanyakazi wa Tarura.

Awali aliwataja majeruhi ni Ernest Mgeni (49), Gervas Myovela (44) wote wakazi wa Mbozi Mkoa wa Songwe na kuongeza kuwa majeruhi hao wote walikuwa kwenye gari ya Tarura na wamehamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa.

Alisema miili imekabidhiwa kwa Meneja wa Tarura Manispaa ya Iringa kisha kupelekwa Dodoma kwa ajili ya taratibu za maziko.

Alisemachanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa fuso kushindwa kumudu gari lake na kusababisha kuhama upande mmoja na kuelekea mwingine na kusababisha ajali hiyo.

Alisema dereva fuso alikimbia baada ya kusababisha ajali hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Dk. Alfred Mwakalebela, amekiri kupokea majeruhi watatu, lakini mmoja alifariki wakati akipatiwa matibabu.



Alisema Mkata alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu.

Wakizungumza hospitalini hapo majeruhi Myovela alisema hakusikia chochote bali alijikuta yupo hoi.

Mgeni alisema yeye na dereva walikuwa wamefunga mkanda, lakini hakujua kama wengine walikuwa nyuma yake wamefunga mkanda na baada ya ajali kutokea, aliulizia wenzake, lakini hakupewa majibu kama wamepona ama la.

# Mkazi Dar kortini madai kutakatisha Dola 750,000

**Na Hellen Mwango**

MKAZI wa Magomeni jijini Dar es Salaam, Haji Msongela (33), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa na tuhuma za uhujumu uchumi ikiwamo kutakatisha Dola za Marekani 750,000.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kevini Mhina.

Wakili wa Serikali Wankyo Simon, alidai katika shtaka la kwanza kuwa Juni 19, mwaka huu katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere alitoa tamko la uongo.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitoa tamko la uongo akiwa anatoka nchini kuwa alikuwa na Dola za Marekani 750,000 na kwamba fedha hizo zinamilikiwa na H.Haji (GSM.Company).

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku na mahali pa tukio la kwanza, mshtakiwa alikutwa na Dola za Marekani 750,000 zilizopatikana isivyo halali.

Hakimu alisema kwa kuwa mashtaka yanayomkabili mshtakiwa ni ya uhujumu uchumi mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Alisema mashtaka ya kutakatisha fedha hayana dhamana mshtakiwa atakwenda mahabusu mpaka Julai 9, mwaka huu.

Wankyo alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya, ***Boston Auction mart na Jaga auction mart***,kwa niaba ya **AccessBank Tanzania Limited** watauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Hivyo basi ifahamike kuwa utakapopita muda wa siku kumi na nne tangu kutoka kwa gazeti hili,Dhamana husika zitauzwa kwa njia ya mnada . Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali hapo chini.

| S/N | TAWI HUSIKA | KAMPUNI INAYO HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MWENYE DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | TEMEKE | BOSTON AUCTION MART | USSI/SHAHA ME,MBARUKU | USSI/SHAHA ME,MBARUKU | NYUMBA | NZASA | 11/7/2019 SAA 6:019M |
| 3 | TEMEKE | BOSTON AUCTION MART | MLAY/WILBRIGHT,WALTER | MWINYIMVUA/ABDALAH,KHURUKA | KIWANJA | VIKUNAI | 10/7/2019 SAA 6:01 PM |
| 4 | TEMEKE | BOSTON AUCTION MART | SALUM/ALI,LUTFI | NYUMBA/ABDALAH,MOHAMED | NYUMBA | SAKU | 10/7/2019 SAA 6:01PM |
| 5 | TEMEKE | BOSTON AUCTION MART | SADALA/S,MZELELA | SADALA/S,MZELELA | KIWANJA | VIANZI | 13/7/2019 SAA 5:00 AM |
| 6 | TEMEKE | BOSTON AUCTION MART | MATAU/LEONS,EPAPHRAS | MATAU/LEONS,EPAPHRAS | NYUMBA | KIWALANI | 11/7/2019 SAA 4:00AM |
| 7 | TEMEKE | BOSTON AUCTION MART | NGOMANDODO/ABRAHAM,CATHERINE | NGOMANDODO/ABRAHAM,CATHERINE | NYUMBA | CHEMCHEM | 10/7/2019 SAA 4:00 AM |
| 8 | TEMEKE | BOSTON AUCTION MART | ISHEMBE/R,SILIVESTER | MABERE/MAUGO,FAIDA | KIWANJA | TOANGOMA | 10/7/2019 SAA 4:00AM |
| 9 | LUMUMBA | BOSTON AUCTION MART | JONGO/TWALIBU,KITWANA | JONGO/TWALIBU,KITWANA | KIWANJA | MABWEPANDE | 12/7/2019 SAA 4:00 AM |
| 10 | LUMUMBA | JAGA AUCTION MART | LYAKURWA/ELIAS,ANSILA | MOSHI/SIFAELI,WILKINS | SHAMBA | KIBAHA-VISIGA | 10/7/2019 SAA 4:00AM |

1. UKAGUZI UNARUHUSIWA MARA USOMAPO TANGAZO HILI.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA MALIPO YA 25% YA FEDHA TASLIMU PAPO HAPO NA 75% BAADA YA SIKU 14 TOKA SIKU YA MNADA KUFANYIKA NA UKISHINDWA KULIPA MALIPO YALIYOBAKI MNADA UTARUDIWA NA FEDHA ULIZO LIPA HAZITARUDISHWA
3. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI MWENYEWE, KUMBUKA VIGEZO NA MASHARTI KUZINGATIWA.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**
**PIGA SIMU NO. 0715203804-Boston**
**0713123427-Jaga**
**WOTE MNAKARIBISHWA.**

215294502



## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA NYANGE AUCTION MART

Kwa niaba ya **AccessBank Tanzania Limited** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara, Nyumba na viwanja vilivyowekwa kama dhamana ya mikopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Mnada utafanyika sehemu nyumba na viwanja husika vilipo siku na tarehe kama vilivyotajwa kwenye jedwali lifuatalo:

| NAMBA | TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MMILIKI DHAMANA | AINA YA DHAMANA | AUCTION COMPANY | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KAHAMA | MAKONDO/MAGESE,TABU | MAKONDO/MAGESE,TABU | NYUMBA | NYANGE AUCTION MART CO. LTD | CHELA/MSALALA | 10/7/2019 | SAA5:00 ASUBUHI |
| 2 | KAHAMA | KITINDI/P,MAKOYE | KITINDI/P,MAKOYE | NYUMBA | NYANGE AUCTION MART CO. LTD | ITWANGI | 11/7/2019 | SAA5:00 ASUBUHI |
| 3 | KAHAMA | SALUMU/B,MIGAYO | SALUMU/B,MIGAYO | NYUMBA | NYANGE AUCTION MART CO. LTD | SHIRIMA/KIKUBIJI/KWIMBA | 13/7/2019 | SAA7:00 MCHANA |
| 4 | KAHAMA | LUHENDE/M,YUSUPH | LUHENDE/M,YUSUPH | NYUMBA | NYANGE AUCTION MART CO. LTD | KAHAMA MJINI | 10/7/2019 | SAA04:00 ASUBUHI |
| 5 | KAHAMA | MAKEJI/MALKAM,KEFA | MAKEJI/MALKAM,KEFA | NYUMBA | NYANGE AUCTION MART CO. LTD | BULUNGWA/USHETU | 10/7/2019 | SAA10:00 JIONI |
| 6 | KAHAMA | FUNGAMEZA/M,ANDREA | FUNGAMEZA/M,ANDREA | NYUMBA | NYANGE AUCTION MART CO. LTD | NYIJUNDU/NYANG'HWALE | 10/7/2019 | SAA9:00 MCHANA |
| 7 | KAHAMA | MHUNA/M,FAIDA | MHUNA/M,FAIDA | FARM (10ACRES) | NYANGE AUCTION MART CO. LTD | NANDA/MBOGWE | 10/7/2019 | SAA5:00 ASUBUHI |
| 8 | KAHAMA | MGENDI/M,SHABANI | MGENDI/M,SHABANI | KIWANJA | NYANGE AUCTION MART CO. LTD | BUNANGO/BUGALAMA/MSALALA | 12/7/2019 | SAA12:00 MCHANA |
| 9 | MWANZA | RUBETO/B,SHABAN | RUBETO/B,SHABAN | CAR T 339CHM | JOSINA COMPANY LIMITED | NYASAKA-MWANZA | 03/07/2019 | SAA 5:00 ASUBUHI |
| 10 | MWANZA | RUBETO/B,SHABAN | ROBETO/BUNDALA,LUCAS | CAR T465BEX | JOSINA COMPANY LIMITED | NYASAKA-MWANZA | 03/07/2019 | SAA 5:00 ASUBUHI |
| 11 | MWANZA | MRONI/MARWA,JULIUS | MRONI/MARWA,JULIUS | NYUMBA | BOSTON AUCTION MART | MANDU-MWANZA | 10/7/2019 | SAA 5:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

**Dhamana zitauzwa mahali zilipo**

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (nyundo itakaposhushwa), salio la 75% ni lazima lilipwe ndani ya siku 14 kutoka siku ya mnada. Kiasi cha asilimia Ishirini na tano (25%) kitakachokuwa kimelipwa hakitarejeshwa iwapo mshindi atashindwa kulipa salio katika kipindi cha siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
   i. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.
   ii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**Kwa mawasiliano:**
**Mratibu wa MIKOPO AccessBank Tanzania Limited-Makao Makuu**
**Simu: 022 2774355, Nukushi: 022 2774340**
**Barua pepe: info@accessbank.co.tz**
**Simu ya Dalali husika: 0765 607 079**

**WOTE MNAKARIBISHWA.**

215294502

# Ndugai: Makabrasha ya wabunge yanajaza 'pick up'

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, (pichani) amesema katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti, wabunge hupewa makabrasha ambayo yanaweza kujaza gari aina ya 'pickup' kwa kila mmoja.

Kutokana na hali hiyo, wamejipanga kusafisha meza za wabunge kwa kuondokana na matumizi ya karatasi kwa kuwapatia kompyuta mpakato (laptop).

Ndugai alitoa kauli hiyo wakati akitoa maelezo ya msaada wa kompyuta mpakato 70 ambazo zimetolewa na Serikali ya China, zilizokabidhiwa na Balozi wa nchi hiyo, Wang Ke.

Alisema nyaraka zinazochapishwa hulenga idadi ya wabunge ambao ni 393, na kwamba katika bunge hilo nyaraka nyingi zimechapishwa.

"Inahitajika mbunge kurudi nyumbani na pick up lililojaa document (nyaraka) mbalimbali, ambazo wamekuwa wakiziacha ovyo ovyo na hata kwa matumizi ya rejea baadaye kuitafuta document jimboni tena si rahisi, lakini akiwa na kompyuta mpakato ni rahisi kuwa na nyaraka zote anazitafuta na kuzipata," alisema.

Alisema kwasasa wanaangalia kupata miundombinu ambayo itafanya madawati ya wabunge kuwa rahisi na kupata popote wanapohitaji.


"Pia watafundishwa namna ya kuzipata na taarifa hizi ni muhimu sana kwa masuala ya rejea," alisema.

Aliishukuru Serikali ya China kwa msaada huo na kwamba ni mpango wa Bunge wa kulisafisha dawati la Mbunge na kulifanya Bunge kuwa la kisasa.

"Kila taarifa zitakuwa ndani ya mtandao huko ndiyo tunakoelekea huo ndiyo mpango wetu," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Spika Dk. Tulia Ackson, alisema katika mpango mkakati wa Bunge unakusudia kusafisha dawati hilo na kuwekwa utaratibu mzuri ambao mbunge hatahitaji kutumia makaratasi.

"Hizi kompyuta mpakato 70



tutaanza nazo na tutaendelea kuongeza kulingana na muda unavyokwenda na tutaanza na wale wenye ufahamu huo, na baadaye watapewa mafunzo namna ya kutumia ili waweze kujua namna ya kupata taarifa mbalimbali," alisema.

Awali, akikabidhi kompyuta hizo, Balozi wa China nchini Tanzania Wang Ke, alisema zawadi hiyo ni ahadi aliyoitoa Naibu Spika wa Bunge la China mwaka jana alipotembelea Bunge la Tanzania ikiwa ni ishara ya kuonyesha mshikamano kati ya mhimili hiyo.

"Kompyuta hizi gharama yake yote ni Sh. bilioni 70 na kwamba huu ni mwanzo tu wa ushirikiano baina ya mabunge haya mawili na tutaendelea kutoa misaada ya kimaendeleo katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, miundombinu, elimu, kilimo na uwekezaji," alisema.

# Waziri Mkuu atoa tamko Watanzania kubaguliwa Kenya

INATOKA UK. 2

Kenya wanaishi kama ndugu,

"Nawasihi wabunge na Watanzania kuwa watulivu kwa kuwa Serikali ya Kenya na Tanzania zinaendelea na mazungumzo ya kidiplomasia.

"Leo (jana), mawaziri wote wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walikutana kule Arusha na wamejadili jambo hili na wamelaani vikali," Majaliwa alisema.

Jaguar pia ni msaanii maarufu wa miondoko ya R&B katika ukanda wa Afrika Mashariki na msanii tajiri zaidi anayemiliki ndege.

Kauli yake ilitua bungeni jijini Dodoma jana baada ya Mbunge wa Rufiji (CCM), Mohammed Mchengerwa, kuomba mwongozo wa Spika akitaka kufahamu msimamo wa serikali kuhusu usalama wa raia wa Tanzania waishio Kenya.

"Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7), kwa kuwa jambo hili halijatokea mapema bungeni, lakini ni jambo la dharura na kwa kuwa jumuiya za kimataifa zinaendelea kuungana kwa kuvunja mipaka ya kiutawala.

"Na kwa kuwa sasa jumuiya yetu ya Afrika Mashariki imepiga hatua ya kimahusiano, lakini Mheshimiwa Spika kuna video imesambazwa na bwana Charles Njagua Kanji, Mbunge wa Starehe nchini Kenya, akitoa ushawishi kwa Wakenya kuwafukuza Watanzania.

Zaidi Mchengerwa alieleza: "Na kwamba ametoa saa 24 kwa Watanzania kuondoka kwenye maeneo wanayoishi vinginevyo atawashawishi wananchi wake wachukue hatua kali dhidi ya wageni wakiwamo Watanzania.

"Naomba mwongozo wako Mheshimiwa Spika, kuhusu usalama wa Watanzania wanaoishi Kenya, kwa kuzingatia matakwa ya muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, serikali inachukua hatua gani."

Akijibu mwongozo huo, Spika aliiagiza serikali kuja na majibu haraka kutokana na jambo hilo muhimu kwa usalama wa Watanzania.

Kwa kuwa jambo hili nimelisikia kutoka kwako, naagiza serikali ilichukue, lazima lipatiwe majibu sasa hivi," alieleza.

Kwenye mitandao ya kijamii imesambaa video ikimwonyesha mbunge huyo akizungumza na wafuasi wake akitoa agizo la kuwataka wageni kuondoka nchini humo kabla hawajachukua hatua za kuwapiga na kuwapeleka uwanja wa ndege.

Njagua alionekana akisema: "Tunaongea juu ya mamia wanaotoka nchi za nje kuja kufanyakazi hapa (Kenya), nataka niseme leo natoa saa 24 kama hao watu hawatarudi kwao mimi kama

mbunge wa hapa tutaingia kwenye maduka wanayofanyiakazi, tutawatoa, tutawapiga na tutawapeleka Airport (uwanja wa ndege).

"Kazi ya immagration (Uhamiaji) itakua kuwachukua uwanja wa ndege kuwapeleka kwao. Tumekuwa na kesi hapa leo, mtu kutoka nje anafanyabiashara hapa, imefika mahali wanakuja kuwasumbua hapa nchini kwetu, sisi kama wananchi wa Kenya na wafanyabiashara wa hapa, hatutasubiri watu kutoka nje kuja kuharibu biashara za Wakenya hapa.

Huku akishangiliwa na wafuasi wake, aliongeza: "Ukiangalia kwenye magari Wapakistani, Wachina wamechukua biashara, masokoni Watanzania na Waganda wamechukua hizo biashara. Sasa tumesema inatosha, kama tukiwapa saa 24 na hawajatolewa hapa, sisi tutawatoa, tutawapiga na hatuwaogopi."


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
25/06/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMISI tarehe 27/06/2019** kampuni ya **GENGS ENTERPRISES LTD** itasafirisha mizigo kutoka **KINONDONI** kuelekea **SAADANI** gari hilo lenye namba za usajili **STH 2712 /STH 2782**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:-

   **Urefu – mita 19m**
   **Upana - mita 3m**
   **Kimo – mita 4.7m**
3. Njia itakayotumika **KINONDONI hadi SAADANI** kupitia **BAGAMOYO-MSATA** gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00Jioni).

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215295302


## Neema tele bajeti 2019/20

INATOKA UK. 2

utekelezaji wa blue print (mpango mkakati), lakini tatu ni kuanza na kuendeleza ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati.

Pia Waziri Mpango alisema uamuzi wa kutopandisha ushuru wa bidhaa wa mazoea, hususani sigara na bia kwa kuielekeza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kubadilika ili kuwa rafiki na wafanyabiashara na walipa kodi, unalenga kupunguza utegemezi wa kibajeti lakini pia shughuli za kikodi kulinda viwanda vya ndani.

"Yako maeneo mengi ambayo wabunge wameishauri serikali iyawekee msumuko wa kipekee katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha na bajeti zinazofuata. Moja ni kuweka mkazo zaidi kwenye kilimo hususani utafiti, mbegu bora, mazao, ughani, pembejeo, kuongeza thamani, kutafuta masoko na kilimo cha umwagiliaji," alisema.

**KODI YA MISHAHARA**

Kuhusu hoja ya nyongeza ya mishahara na serikali kuboresha maslahi ya watumishi wa umma, Waziri Mpango alisema serikali inathamini sana mchango wa watumishi wa umma katika maeneo yote ya nchi na si kweli kwamba serikali imewasahau watumishi kama ilivyozungumzwa na baadhi ya wabunge.

Alisema katika mwaka wa fedha 2016/17 serikali ilipunguza kodi kwenye mishahara (PAYE) kutoka digiti mbili mpaka moja.

Aidha, alisema mpaka kufikia Mei mwaka 2018/19, serikali imelipa madai mbalimbali ya watumishi jumla ya Sh. bilioni 64.97 na pia ilipandisha madaraja watumishi wote waliokuwa wanastahili na jumla ya Sh. bilioni 14.55 zilitumika hadi Mei, mwaka huu.

Pia alisema ahadi ya Rais (Magufuli) ya kupandisha mishahara ya watumishi wa umma ik pale pale.

"Kuhusu kupunguza kodi kwenye mishahara ya watumishi, alisema serikali imekuwa ikiboresha mfumo wa kodi, tozo na ada mbalimbali ili kuongeza mapato, kuboresha mazingira ya kufanya biashara lakini pia mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii yanayoguswa na mfumo huo.

Alisema muundo wa uchumi umebadilika tangu miaka ya 90 na kwamba mahitaji ya fedha ya kugharamia matumizi ya kawaida ya serikali na ya miradi ya maendeleo kwa ustawi wa jamii umeongezeka lakini pia gharama za maisha kwa wananchi na hususani kwa wafanyakazi.

**DENI LA TAIFA**

Waziri Mpango alisema deni la serikali limeendelea kuwa kubwa mwaka hadi mwaka, hivyo kuathiri uchumi na maisha kwa ujumla.

Alisema katika kipindi cha mwaka ulioishia Aprili, mwaka huu, deni la serikali liliongezeka kutoka Sh. trilioni 49.86 na kufikia Sh. trilioni 51.03 ambalo ni ongezeko la asilimia 2.35.

# Magendo ya kahawa sasa kudhibitiwa kisasa

**Restuta Damian,** BUKOBA

MKOA wa Kagera umesema utapambana kwa njia ya kisasa badala ya matumizi ya nguvu kuzuia biashara ya magendo ya kahawa msimu wa mavuno.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa huo, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Posta (TPB), Dk. Edmundi Mndolwa, baada ya ufunguzi wa tawi la benki hiyo wilayani Karagwe.

Gaguti alisema fursa ya kupatiwa tawi la benki katika wilaya hiyo na Wilaya ya Kyerwa ambazo wakulima wa kahawa kuuza zao hilo kwa njia za magendo kabla ya msimu. Aidha, alisema changamoto kubwa kwa wakulima hao ni upatikanaji wa fedha ya kujikimu wanapoanza uvunaji, hivyo manunuzi ya magendo hushamiri kuanzia mashambani hadi mipakani.

"Kwa sasa tumeanza uvunaji, na sisi matarajio ya kuanza manunuzi ni Julai hadi Agosti, anaona ni bora auze kwa bei ya hasara ya shilingi 600 hadi 800 kwa kilo moja ambayo ni bei ya hasara lengo apate pesa kwa wakati," alisema Gaguti.

Alisema kupitia tawi la benki hiyo itasaidia kuondoa magendo kwa kutumia njia za kisasa zenye kuwapatia mikopo midogo wakulima ambao mashamba yao yana mibuni kuendeshea shughuli zao.

"Ombi langu kama Mkoa, ambao tunapambana na magendo kwa kutumia nguvu, sasa ni muda wa kupambana kisasa sio nguvu tena kwani wakulima kwa kuangalia mashamba yao wanakopesheka kwa pesa kidogo kama Sh. 300,000 baada ya mauzo wakarudisha pesa ya benki kwa kuingia makubaliano, hii itasaidia kuondoa magendo," alisema Gaguti.

Alisema wananchi wa Mkoa wa Kagera hutegemea zaidi kilimo na uvuvi kwa asilimia 54, asilimia 14 wafanyabiashara na asilimia moja ni watumisi walio na ajira yenye mfumo rasmi, wakati asilimia 54 wako nje ya mfumo rasmi.

Dk. Mndolwa alisema kupitia nguvu kazi ya vijana, mkoa utaweza kulima mibuni kwa kaya ndani ya mkoa, lengo liwe kila wilaya kuwa na zao la kahawa.



Mafundi wakiendelea na kazi ya kukarabati meli ya MV Victoria katika Bandari ya Mwanza, ukarabati wa MV Victoria unaoigharimu serikali Sh. bilioni 22, unahusisha uwekaji wa injini mpya, jenereta mpya, mitambo ya nguvu pamoja na vyombo vya uongozaji na uokoaji ambapo hadi kufikia Machi 2020 meli hiyo, itakuwa imeanza kutoa huduma kwa wananchi kati ya Mwanza na Bukoba. **PICHA NA ELIZABETH FAUSTINE**

# Watanzania waonyeshwa fursa ya uwekezaji masoko ya fedha

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wameshuariwa kuwekeza katika masoko ya fedha ili kunufaika na fursa zinazopatikana katika masoko hayo ambayo hayahitaji mtaji mkubwa wa kuanzia imeelezwa.

Ushauri huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Idara ya Hazina na Masoko wa Benki ya NBC, Peter Nalitolela, katika warsha maalumu iliyoandaliwa na Benki hiyo kwa wanafunzi wa Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS), iliyofanyika chuoni hapo jijini Dar es Salaam.

Alisema lengo kubwa la warsha hiyo ni kunoa uelewa wa wanafunzi hao kuhusu masoko ya fedha, ili wawe na uwezo wa kuchangamkia fursa lukuki zilizopo sokoni hapo punde wanapomaliza masomo yao.

"Kuna kasumba iliyojengeka miongoni mwa watu wenye vipato vya wastani kuwa kuwekeza katika masoko ya fedha ni ghali na ni eneo la uwekezaji ambalo limeachiwa matajiri, kitu ambacho hakina ukweli wowote ukiangalia hali halisi," alisema.

Nalitolela aliongeza kuwa kiwango cha chini kinachohitajika kuwekeza katika soko la fedha ni shilingi sita, fedha ambayo alisema inaweza kupatikana kwa mtu yeyote aliyejiwekea malengo ya dhati ya kutunza fedha kwa ajili ya kuwekeza kwa manufaa yake ya baadaye.

Alisema cha kushangaza, watu wengi ambao wanajichukulia kuwa wenye kipato cha chini wana tabia ya kuwekeza kwenye biashara zilizozoeleka kama kununua daladala au kufungua duka la rejareja, miradi ambayo kiuhalisia inahitaji mtaji mkubwa kupindukia ule unaohitajika kuwekeza katika hati fungati, hisa au dhamana.

" Tunawashauri Watanzania wawekeze kwenye kampuni nyingi zilizobinasishwa na ambazo zinafanya vizuri kibiashara, ili washiriki katika kuendesha uchumi wao na vilevile wajizolee sehemu ya faida inayotengenezwa na kampuni hizo," alisema Nalitolela.

Kuhusu mafunzo hayo Nalitolela, alisema ni sehemu ya mpango wa NBC kutumia sehemu ya faida yake kusaidia ustawi wa jamii, na yanalenga kuwapatia wanafunzi wanaosomea fani za fedha na benki katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam stadi za masoko ya fedha ili kuwaanda kuyatumia na kufaidika nayo.

## Shell yapewa 5 kuhamasisha nishati mbadala

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa mazingira wamepongeza juhudi zinazofanywa na Kampuni ya Shell Tanzania na hasa katika kuchangia eneo la utunzaji mazingira na matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza athari za nchi kugeuka jangwa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mara baada ya kumalizika kwa mjadala ulioandaliwa na kampuni hiyo kuhusu mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na uharibifu mkubwa wa mazingira, waliipongeza kwa kuwa mstari wa mbele kuhimiza matumizi bora ya nishati mbadala ili kulinda mazingira.

Mwakilishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Joseph Qamara, alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wote katika suala zima la uhifadhi na utunzaji wa mazingira ili kuliepusha taifa na majanga mbalimbali yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi.

"Tunatambua juhudi na vipaumbele vya Shell Tanzania na wadau wengine katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira kwa kuepuka uharibifu wa misitu, na badala yake kuhamasiaha matumizi ya nishati mbadala pamoja na upandaji wa miti," Qamara alisema.

Majadiliano hayo yaliwashirikisha washindi wa shindano maalum la mashujaa wazalishaji wa nishati mbadala ya mkaa, lililozinduliwa rasmi mwaka jana na Ofisi wa Makamu wa Rais - Idara ya Mazingira, ambao ubunifu wao unalenga kuongeza uzalishaji wa mkaa mbadala utakaosaidia kuokoa misitu na kuboresha mazingira kwa ujumla, waliishukuru kampuni hiyo kwa kuwawezesha.

Kampuni ya Shell Tanzania ilitoa Sh. milioni 300 kwa mshindi wa kwanza, Sh. milioni 200 kwa mshindi wa pili na Sh. milioni 100 kwa mshindi wa tatu kama mtaji ambao utawekezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kama sehemu ya kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Uongozi na Biashara (IMED), Dk. Donath Olomi, mbali ya kuipongeza Kampuni ya Shell Tanzania alisema mjadala ulikuwa na faida kubwa kwani uliwaleta pamoja wadau wote muhimu kwenye maeneo ambayo yalikuwa yakijadiliwa kwa uwazi mkubwa.

Alisema ushiriki wa serikali ni muhimu katika kuhakikisha Watanzania wanatumia nishati mbadala badala ya mkaa na kuni, hatua ambayo itasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira unaochangiwa zaidi na ukataji wa kuni na utengenezaji wa mkaa unaotumiwa kama chanzo kikuu cha nishati majumbani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Shell Tanzania, Marc den Hartog, alisema ipo haja ya Watanzania kubadilika kutoka katika matumizi ya mkaa na kuni na kuelekea kwenye matumizi ya nishati mbadala, hatua ambayo itaepusha athari zote zinazoletwa na mabadiliko ya tabia nchi ikiwa ni pamoja na ukame.

## Ndugai awapa angalizo wanaume likizo ya uzazi

SPIKA Job Ndugai amewataka wanaume wanaopata likizo ya uzazi, kukaa nyumbani kulea watoto badala ya kutumia likizo hiyo kushinda baa.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa rai hiyo bungeni jijini Dodoma jana baada ya Mbunge wa Viti Maalum, Anatropia Theonest (Chadema), kueleza kuwa wanaume ni kiungo muhimu katika malezi hasa kwa mama anayepata mtoto njiti au mapacha.

"Je, serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kubadili kanuni kukaa nyumbani kusaidiana na familia si chini ya wiki mbili au tatu ukizingatia hutolewa likizo hiyo kila baada ya miaka mitatu?" Mbunge huyo alihoji.

Kabla ya swali hilo kujibiwa na serikali, ndipo Spika Ndugai alipotoa rai yake kwa wanaume na kushauri waongezewe muda zaidi ili wakapakate watoto.

Akijibu swali la mbunge huyo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, alisema kwa mujibu wa kanuni, mwanaume anapewa siku tano katika kipindi hatarishi cha kujifungua ili akae na mama aliyejifungua.

Mwanjelwa alisema endapo kuna mazingira katika familia hayaruhusu mtumishi huyo wa kiume kutokuwa mbali na familia kwa wakati huo, anaweza kuomba kibali kwa Katibu Mkuu Utumishi kupitia kwa mwajiri wake.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji muda wa likizo ambao wamekuwa wakipewa wazazi pale wanapopata watoto mapacha zaidi ya wawili au watoto njiti.

Akijibu swali hilo, Mwanjelwa alisema kwa mujibu wa Kanuni H.12(2) ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, mtumishi wa umma mwanamke anapojifungua mtoto hupewa likizo ya uzazi ya muda wa siku 84 mara moja kila baada ya miaka mitatu. Alisema pia kwa mujibu wa Kanuni H.12(3) ya kanuni hizo, mtumishi husika anapojifungua watoto zaidi ya mmoja, hupewa siku 14 zaidi za likizo ya uzazi, hivyo kuwa na likizo ya siku 98.

"Kanuni tajwa haikubainisha muda wa likizo ya uzazi kwa mtumishi anayejifungua mtoto njiti. Matukio ya uzazi wa mapacha zaidi ya wawili na watoto njiti ni nadra kutokea mara kwa mara," alisema.

Alitoa wito kwa waajiri na wasimamizi wa rasilimaliwatu katika utumishi wa umma kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu Utumishi na kuomba kibali cha kuongezwa muda wa likizo ya uzazi wa watumishi wa umma walio chini yao pindi wanapojifungua watoto mapacha zaidi ya wawili au watoto njiti.

# Serikali yaandaa waraka vitambulisho wajasiriamali

SERIKALI imesema itatoa waraka mahsusi unaoainisha nani anapaswa kutozwa kodi na anayestahili kupata kitambulisho cha ujasiriamali.

Vilevile, imesema inatengeneza na itasambaza nchi nzima waraka unaoainisha kodi kero ilizofutwa.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), Mwita Waitara, alipojibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Bariadi, Andrew Chenge (CCM).

Mbunge huyo alihoji sababu za Ofisi ya Rais - Tamisemi kutotoa waraka kwa halmashauri zote kuainisha kodi zilizofutwa na Bunge baada ya kubaini kuwa ni kero.

"Pamoja na nia njema ya utoaji wa vitambulisho kwa wajasiriamali, lakini vimekuwa ni kero kwa wananchi, serikali haiwezi kutoa maelekezo ya jinsi ya kutekeleza zoezi hilo ili kuwe na 'usare' kuliko hali ilivyo sasa?" Chenge alihoji.

Akijibu maswali hayo, Waitara alisema waraka huo wa kodi zilizofutwa utatengenezwa na utasambazwa nchi nzima na wabunge watapewa nakala ili kujua zilizofutwa na serikali.

Hata hivyo, naibu waziri huyo alikiri kuwapo kwa changamoto katika utoaji wa vitambulisho vya ujasiriamali.

"Tutakapoanza mwaka wa fedha mpya Julai Mosi, tutatoa waraka mahsusi unaoainisha nani anapaswa kutozwa kodi ya ujasiriamali na nani anapaswa kupewa kitambulisho cha ujasiriamali na baada ya kutolewa kwa waraka huo, yeyote ambaye atakiuka na kwenda kinyume cha maelekezo hayo hakutakuwa na msamaha," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Kavuu, Dk. Pudenciana Kikwembe (CCM), alihoji sababu za baadhi ya halmashauri kukaidi agizo la Rais kuhusu ufutaji wa 'kodi kero'.

Akimjibu mbunge huyo, Waitara alisema kodi kero zilifutwa na serikali kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura 290 mwaka 2017.

"Halmashauri yoyote inayoendelea kuwatoza wananchi kodi ambazo zimefutwa na serikali kwa mujibu wa sheria, inakiuka maelekezo ya serikali. Natumia fursa hii kuziagiza halmashauri kuacha kutoza kodi ambazo zimefutwa kwa mujibu wa sheria," alisema.

Waitara alisema Ofisi ya Rais - Tamisemi haitasita kuchukua hatua za kisheria kwa halmashauri ambayo itabainika kuwatoza wananchi kodi ambazo zimefutwa kwa mujibu wa sheria.

"Kama mbunge anazo taarifa za halmashauri inayotoza kodi zilizofutwa, apeleke taarifa hizo ili serikali ichukue hatua," Waitara alisema.




Meneja wa Bidhaa ya Omo wa Kampuni ya Unilever, Upendo Mkusa (kushoto), akimkabidhi msaada wa sabuni, sukari na nguo Mkurugenzi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Children`s Home Msimbazi, Sista Etienne, katika kuhitimisha kampeni ya kampuni hiyo ya Toa Mkono wa Ukarimu iliyofanyika kipindi cha mwezi wa Ramadhani uliomalizika hivi karibuni. Makabidhiano hayo yalifanyika kituoni hapo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Taarifa utawala bora zaandaliwa

SERIKALI imeliambia Bunge kuwa hadi mwaka huu, Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (APRM) umeshaandaa taarifa mbili za utawala bora ndani na nje ya nchi.

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Gando, Othman Omar Haji (CUF).

Katika kujenga hoja yake kabla ya kuuliza swali, mbunge huyo alisema lengo kuu la APRM ni kuziwezesha nchi za Afrika kuimarisha utawala bora kwa kuwawezesha wananchi wake kubainisha changamoto.

"Je, ni hatua gani ambazo zinachukuliwa na Tanzania katika kutekeleza mpango huo?" Mbunge huyo alihoji.

Dk. Ndumbaro alisema mbali na taarifa hizo, umeandaliwa mpango kazi wa APRM wenye lengo la kutatua changamoto za utawala bora zilizobainishwa kwenye taarifa zilizotajwa.

"Ili kuwezesha utekelezaji wa taarifa za APRM, kimeundwa kikosi kazi cha APRM chenye jukumu la kuandaa taarifa za utekelezaji za kila mwaka na taarifa hizo huunganishwa kuwa taarifa moja ya nchi," alisema.


Alisema serikali imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya kazi za APRM kila mwaka na kulipa michango yake kwa taasisi hiyo kila mwaka.

Pamoja na hayo, Dk. Ndumbaro alisema serikali kupitia wizara hiyo kwa kushirikiana na wizara na taasisi za serikali na sekta binafsi, itaendelea kutatua changamoto za utawala bora kama ilivyoelekezwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na kuainishwa kwenye mpango kazi wa APRM.

Alisema wizara hiyo ilikabidhiwa jukumu la kuwezesha utekelezaji wa APRM nchini na katika kutekeleza jukumu hilo, wizara iliandaa semina za uhamasishaji juu ya mpango wa APRM ili kuwaandaa wananchi kushiriki kikamilifu katika mpango huo.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi 38 kati ya 54 barani Afrika zinazoshiriki katika mpango wa APRM, ikijiunga mwaka 2004 na Bunge la Tanzania liliridhia makubaliano hayo mwaka 2005," alisema.

"Hii ni kutokana na imani kubwa iliyonayo katika lengo kuu la mpango wa APRM ambalo ni kuziwezesha nchi za Kiafrika kujitathmini kwa vigezo vinavyokubalika vya utawala bora."




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Wanawake Longido washukuru Mmarekani kuwajengea zahanati

**Na Zanura Mollel,** ARUSHA

WANAWAKE wa Kata ya Olmolog Tarafa ya Enduiment, wamemshukuru Diana Raleigh, raia wa Marekani, kwa kuwajengea zahanati na shule katika Kitongoji cha Olmoti Kijiji cha Elerai kwa gharama zaidi ya Sh. bilioni 3.

Wamesema amewaepushia na kuwaepushia kusafiri umbali wa kilomita zaidi ya 50 kufuata huduma za afya ya uzazi. Nosimu Laizer alisema wana kila aina ya furaha kwa kupata ukombozi.

"Kweli kinamama na watoto wengi wamepoteza maisha sababu ya kufuata huduma mbali na hapa, lakini sasa tunamshukuru Diana Raleigh kwa kutujengea zahanati na shule," alisema.

Alisema awali kabla ya upatikanaji wa zahanati hiyo, walikuwa wakitembea kilomita 20, kufuata huduma Hospitali ya Ngarenairob Wilaya ya Siha, muda mwingine walikuwa wanaenda Hospitali ya Mama Maria Kijiji cha Lerangwa zaidi ya kilomita 18.

Diana Raleigh alisema alikuja nchini mwaka 2009, akiwa katika Hifadhi ya Wanyamapori Enduiment (EWMA) chini ya kampuni ya kitalii ya Kibo, inayomilikiwa na Wilbroad Chambulo na alifanikiwa kutembelea maboma ya Kimaasai, ndipo alipokutana na mkunga wa jadi, Yaya Ngulia.

Alisema alikutana na mkunga huyo akiwa na binti anayeumwa uchungu na ameshindwa kumzalisha, hivyo akawa anaomba msaada wa usafiri ili aokoe maisha ya binti huyo, naye alikubali kumsaidia, lakini baada ya msaada huo alimuuliza angependa amsaidie nini zaidi, naye alimwambia anaomba awajengee kliniki, kwani wanatembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

"Yaya aliniambia mimi ni mkunga wa jadi na sasa nimezeeka, sitaweza tena kufanya kazi hii, naomba utujengee kliniki kuokoa maisha ya kinamama wajawazito na watoto, hapo ndipo mwanzo wa ujenzi wa zahanati hii," alisema Raleigh. Alisema ndani ya miezi sita kliniki ya mama na mtoto ilikamilika na baadaye waliongeza majengo mengine, kikiwamo chumba cha upasuaji, wodi ya mama, baba na watoto na chumba cha kujifungulia kinamama na pia waliweka vifaa vyote muhimu katika zahanati hiyo.

Raleigh alisema mbali na msaada wa zahanati, pia alihamasisha jamii hiyo, juu ya afya na maambukizi ya Ukimwi na kuwataka kujitokeza kupima na kubaini hali zao, pamoja na kuhakikisha wenye matatizo ya fistula na ugonjwa wa macho (trakoma), wanapata matibabu kwa haraka katika Hospitali ya KCMC Mkoa wa Kilimanjaro.

"Kati ya watu 500 waliopima maambukizi ya Ukimwi, walibainika watu sita pekee wakiwa na maambukizi, nimesaidia watu 1,000 matibabu ya ugonjwa wa trakoma," alisema Raleigh.

Alisema kuwa katika suala la elimu nalo alipambana nalo japo ilikuwa ngumu sababu wanawake wa jamii ya kifugaji walimwambia kuwa hawapo tayari kuwapeleka watoto wao shule, kwani shule ipo mbali na makazi yao na kudai kuwa watabaki wakichunga mifugo.

"Walivyoniambia hivyo, nilishirikiana na marafiki zangu wa Marekani, tumejenga Shule ya Msingi Olmot majengo sita, kuna shule ya chekechea, kuna vyoo vya kutosha na sasa watoto wanasoma," alisema Raleigh.

Aidha, Raleigh, hakuishia hapo alisema vijana wa jamii ya Kimaasai (moran) zaidi ya 100 walimfuata na kumwomba kuwasomesha elimu ya watu wazima na kwenye shule hiyo, pia wanafundishwa vijana hao (Memkwa) ambayo haina umri. "Nina furaha sana kukabidhi miradi hii ya afya na elimu kwa serikali, lakini bado tuko pamoja siwezi kuwaacha," aliahidi Raleigh.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Candy &Candy, Joe Kariuki, akimkabidhi Mkurugenzi wa kituo cha watoto yatima cha Faraja, Faraja Mollel, gunia la unga ikiwa ni sehemu ya vyakula walivyopeleka kituoni hapo mwanzoni mwa wiki. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Wataka sheria ndogo kuwabana wananchi kujiunga bima ya jamii

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WADAU wa afya mkoani Manyara, wamezitaka halmashauri zote kuhakikisha zinatunga sheria ndogo za vijiji za kuwabana wananchi, kuhamasika kujiandikisha katika Mfuko wa Bima ya Jamii [CHF] ulioboreshwa, ili kuondokana na adha ya upatikanaji wa matibabu.

Makubaliano ya wadau hao yanataka wananchi wengi wajiunge na bima hiyokabla ya serikali kutunga sheria itakayowataka wananchi

wote kuwa na bima ya afya.

Walisema bila ya kuwa na sheria ndogo ambazo zitawataka wananchi kujiandikisha kwa wingi kwenye mfuko huo,wasimamizi wa mradi huu watashindwa kufanya kazi hiyo kwa weledi nawataendelea kuisubiri serikali kutunga sheria ya kuwalazimisha watukujiunga na bima.

Waliopitisha azimio hilo ni wakuu wa wilaya, wenyeviti wa

halmashauri, waganga wakuu wa wilaya na watoa huduma mbalimbali wa afya, ambao wanasimamia mfuko huo ambao wataalamu wa afya, wanadai ukisimamiwa vizuri utaleta matokeo chanya.

Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la PharmAccess International nchini, Dk. Heri Marwa, alisema afya ni uwekezaji, hivyo mtu akiwekeza matokeo yake atakuja kuyaona baadaye kwa kuwa hakuna biashara mtu anaweza kupata faida bila kuwekeza, hivyo serikali na wadau wakiwekeza kwenye kuelimisha watu, jamii itafika mbali.

"Mfano mzuri ni Rwanda kuna wakati tulienda na wabunge tukaambiwa inafika hatua ukienda kununua bia baa, unaulizwa una bima ya afya,

ukisema unayo, ndipo unapatiwa huduma ya kuuziwa bia unayotaka," alieleza.

Naye Meneja wa CHF, Slivery Mgonza, alisema pamoja na kukubaliana itungwe sheria ya kuwabana wananchi wajiunge na CHF, bado suala la elimu ni muhimu kwa wananchi, maana wapo baadhi wakilazimishwa watahofu watanyang'anywa ng'ombe wao.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, alisema mpango huo wa kuangalia vituo vya afya vya serikali, siyo rafiki kwa wananchi wake kwa sababu wengi wanatumia hospitali za dini hivyo hawawezi kuafiki.

# Watoto yatima wakumbukwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KAMPUNI ya Candy & Candy imetoa misaada wa vyakula, vinywaji baridi na fedha za kununulia nguo za ndani watoto yatima, wanaolelewa kwenye kituo cha Faraja cha jijini Arusha.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Joe Kariuki, juzi aliongoza wafanyakazi wa kampuni hiyo, kugawa vitu hivyo pamoja na kuongea na watoto wa kituo hicho zaidi ya 200.

Alisema kampuni yao itaendelea kuwa karibu na kituo hicho na kuahidi kurudi kituoni hapo baada ya miezi miwili, ni endapo akiwakuta wamebadilika na kuwa na mwenendo mwema, atawapatia zawadi ya runinga.

"Baba yenu (Faraja) ameniambia hapa kuna waliokuwa wamehukumiwa na kufungwa, tunashukuru sasa mko kwenye hiki kituo mnalelewa vizuri, basi badilikeni tabia, ili msirudi tena kule kwenye matatizo," alisema Kariuki na kuongeza:

"Nitakuja hapa baada ya miezi miwili, baba yenu akiniambia mmebadilika tabia, hampigi watoto wa majirani na mnafanya usafi wa mwili (kuoga) nitawanunulia TV nitaifunga hapo (akionyesha ukutani)."

Mkurugenzi huyo ambaye kampuni hiyo ina matawi nchi mbalimbali, huku makao makuu yake yakiwa nchini, Uingereza alitoa fedha kwa ajili ya kusaidia masomo ya ziada ya mwanafunzi, Barakaeli ambaye alidai kuwa endapo asingelipa ada kwa siku ya Jumatatu, basi asingeruhusiwa kuingia darasani kujifunza.

Kariuki alitoa fedha kwa ajili ya kuwanunulia nguo za ndani watoto wenye umri wa kati ya miaka tisa na 16, kwenye kituo hicho baada ya kumweleza kuwa wengi wanayo moja, huku wachache wakiwa na ambazo hazizidi tano.

Naye Rais wa Programu ya U & I, (you and I) inayoendeshwa na Candy & Candy, Nasra Swai akiongea na watoto wenye umri wa kati ya miaka tisa na 17, aliwaeleza umuhimu wa kujitambua kama watoto.

Mkurugenzi wa kituo hicho, Faraja Mollel, alisema kuwa wanakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa chakula cha kutosha, kwa ajili ya watotohao ambapo wakati mwingine huwapa milo miwili tu kwa siku.



Wafanyabiashara ndogo ndogo, wakiwa na watoto wao kwenye soko la Pasua, Manispaa ya Moshi. Madai ya wazazi na walezi wao ni kukosa imani na wasichana wa kazi na ndugu wa familia kwa hofu ya kufanyiwa ukatili ukiwamo wa kingono. **PICHA: MARY MOSHA**

# Marufuku wafanyabiashara kwenda sokoni na watoto chini ya miaka 5

**Na Mary Mosha,** MOSHI

KUFUATIA malezi hatarishi ya watoto katika maeneo ya ujasiriamali, uongozi wa soko la kuu la mitumba la Memorial, Manispaa ya Moshi, umeahidi kushirikiana na dawati la jinsia la Jeshi la Polisi, kupiga marufuku wafanyabiashara wa soko hilo kwenda sokoni hapo na watoto chini ya miaka mitano.

Pia kabla ya kufanyika kwa zoezi hilo, uongozi huo utatoa elimu kwa wazazi na walezi wenye watoto kuanzia miaka sifuri hadi mitano ambao wanaonekana sokoni hapo kuanzia saa 12 alfajiri hadi saa moja usiku wakiwa na wazazi wao.

Mwenyekiti wa soko hilo, Godfrey Shayo, alisema hayo wakati wa utafiti wa kuongeza uelewa, uwajibikaji wa huduma bora za malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto (ECD), unatekelezwa na muungano wa vilabu vya waandishi wa habari nchini (UTPC), kwa kushirikiana na Taasisi ya CiC ya Ireland. "Ukija sokoni hapo majira ya saa 11 alfajiri utaona wazazi na walezi wakiwa na watoto wachanga...huu ni ukatili na unaathiri afya ya mtoto na malezi yake ya baadaye, tumeliona hili na tunaandaa mpango wa kutoa elimu kabla ya kuchukua hatua," alisema.

Mwenyekiti wa soko la Mbuyuni, Lameck Mziray na mwenyekiti mtaa wa soko la Pasua, Rahibu Juma, walikiri kuwapo kwa changamoto inayoathiri afya za watoto hao na kuahidi kuandaa mpango wa ushirikishwaji na wafanyabiashara ili kujadili suala hilo.

Daktari bingwa mwandamizi wa afya ya jamii, Uzazi na magonjwa ya kinamama, Dk. Moke Magoma, alisema malezi hayo yasipodhibitiwa yatachangia kwa asilimia kubwa kujenga taifa la kizazi kisicho na mwelekeo na chenye urahisi wa kujihusisha na matukio ya uhalifu. Alisema maeneo ya ujasiriamali siyo salama kwa malezi na makuzi ya watoto kiafya na kisaikolojia na kwamba jambo la msingi kwa wazazi na walezi ni kutafuta mbinu mbadala ili kuokoa kizazi hicho.

Baadhi ya wazazi Mwantumu Swalehe na Hadija Omary, walidai wanalazimika kwenda katika maeneo ya ujasiriamali na watoto kutokana na kukosa imani na walezi wengine husu-sani ndugu wa karibu wa kiume ambao huwafanyia ukatili wa kingono.

"Baba usituone tunahangaika na watoto wetu huku sokoni, tunafahamu kwamba ni hatari kwa afya, lakini inatulazimu kutokana na kubadilika kwa dunia ya sasa...huyo unayemwamini ndiye anaye kuharibia mtoto, serikali ilitizame hili," alisema Swalehe.

# Vijana wapewe fursa ajira kukusanya taka

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI mkoani Kilimanjaro imeitaka Halmashauri ya Manispaa ya Moshi kuibua ajira mpya kwa vijana kwa kuwapa fursa ya kukusanya taka majumbani kibiashara na kupeleka katika eneo maalumu litakalotengwa badala ya mfumo unaotumika sasa.

Kwa sasa manispaa inapitisha gari mitaani kubeba taka, jambo linaloweza kufanywa na vijana hao na kupeleka katika kituo maalum ambacho kitatumiwa kupeleka dampo kuu.

Katibu Tawala Msaidizi, Utawala na Rasilimali Watu mkoani hapa, Bwai Biseko, alisema hayo akifungua kikao cha mazingira kilichojumuisha viongozi wa mitaa na kata zinazozunguka msitu wa Rau ili kuondoa tatizo la utupaji taka katika msitu huo.

"Vijana wanaweza kutumika baada ya jamii kuchangia kiasi fulani cha fedha ili taka zirundikwe eneo moja huku magari ya manispaa yakipita kukusanya katika vituo vikuu na hili linawezekana kama jamii itakuwa na dhamira ya dhati kubadilika katika usafi wa mazingira," alisema.

Alisema lengo la mipango hiyo ni kuhakikisha msitu wa Rau unatumika kama sehemu ya utalii, lakini pia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayoleta athari za uharibifu wa mazingira.

Kwa upande wake Naibu Meya wa Manispaa hiyo, Jomba Koyi, alisema manispaa ina mipango ya kugeuza taka kuwa rasilimali kwa ajili ya uzalishaji wa gesi.

"Tayari tumetangaza zabuni ya ujenzi wa dampo jipya eneo la Mtakuja nje ya Manispaa, hadi kufikia Desemba mwaka huu taka zitakuwa mali na wananchi watauza taka zao badala ya kuzitupa...hii itabadili mtazamo na itatunza mazingira," alisema.

Naye Ofisa Maliasili mkoani hapa, Emmanuel Kiengi, alisema kikao hicho kilichoendeshwa kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), kimelenga kuhakikisha sheria, taratibu na mamlaka zinazosimamia misitu vinaheshimika.

Alitaka viongozi hao kubeba dhamana ya kulinda rasilimali za msitu huo kwa kutoa elimu kwa jamii inayouzunguka ili kuuhifadhi.

Awali Ofisa Misitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Joshua Mungure, alikiri kuwapo kwa uchafu wa taka ngumu na nyingine katika msitu wa Rau na kutaka jamii kubadilika tabia.

"Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 inahusu sana misitu haswa ya asili katika sehemu ya tano kifungu 26 kinaeleza utunzwaji wa misitu iliyohifadhiwa kisheria imetaja masuala kama kuingia msituni kuangusha miti, kuchimba madini, mifugo watakaokwenda kinyume na hayo wakitiwa hatiani watalipa faini siyo chini ya Sh. milioni moja," alisema.

# TRA yakabidhi bidhaa za mil. 26/- zilizokamatwa kama msaada

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imekabidhi sukari tani 18 na mafuta lita 4,766 vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 26 kwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ili kuwapa wahitaji hasa Magereza na vituo vya watoto yatima.

Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, alisema mafuta na sukari vimekamatwa kutoka kwa wafanyabiashara wadogo katika kipindi cha mwaka 2018/2019, waliotumia njia za magendo kuingizia bidhaa hiyo nchini kinyume na sheria.

"Tumefikia azimio la kukabidhi bidhaa hizi kwa mkuu wa mkoa ili ziweze kugawanywa kwa wahitaji kwa kuwa ilizoeleka zinapigwa mnada na wahusika wanakuja kuzikomboa na kuzirudisha sokoni jambo ambalo halikubaliki kisheria...zipo salama...Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), imethibitisha kuwa hazina madhara," alisema.

Alisema mbali na bidhaa hizo ambazo wamezikamata kutoka nchi mbalimbali ikiwamo Brazil, pia wamekamata simu za mkononi zaidi ya 1,250 zenye thamani ya Sh. 12,217,779.00 ikiwamo na kodi na adhabu Sh. 9,120,849.50 ambazo wanasubiri wahusika kwenda kulipia na kuchukua mizigo yao.

"Bidhaa nyingine ambazo zilikamatwa ni pamoja na pipi (Gomba bubble), maziwa ya brookside na bidhaa mchanganyiko kama malapa, steel waya na chumvi...pia magari zaidi ya 13 ambayo yanamakosa mbalimbali ya kiforodha pamoja na pikipiki tano ambazo zipo kwenye orodha ya mnada," alisema. Akipokea bidhaa hizo, Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Mghwira, alisema licha ya magendo ya sukari kupungua ikilinganishwa na miaka ya nyuma, bado mkoa kwa kushirikiana na mamlaka wataendelea kufanya operesheni kwa njia ya siri ili kutokomeza magendo kuingia nchini.

"Ni kweli nimepokea sukari na mafuta haya ambayo kama mkoa tutaelekeza vituo vya watoto yatima pamoja na Magereza, lakini tunawaomba wafanyabiashara wafuate utaratibu wa kuingiza bidhaa hizo ili kutokomeza magendo mkoa wa Kilimanjaro.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha mfanyabiashara mdogo anakuwa kwa kasi na kuleta mabadiliko katika biashara yake na kwa taifa kwa ujumla na si kuendekeza kamata kamata ambayo inaweza kuleta madhara katika biashara zao ikiwamo kupoteza mtaji.

"Jeshi la Polisi kwa kushirikiana naTRA hakikisheni mnaongeza doria na kuwaweka watendaji waaminifu, katika maeneo ya Kitobo/Kileo, Kivishini, Ziwa Jipe/Mgagao, wilayani Mwanga, Lower road mpaka maeneo ya mpakani Holili na Himo, Wilaya ya Rombo, Siha maeneo ya Sanya juu, West Kilimanjaro, Kamwanga/Rongai, Munga/Chunvini na barabara ya Moshi –Arusha," alisema.

Pia baadhi ya wafanyabiashara wa maduka katika kata ya Kiusa, Manispaa ya Moshi, Faustina Urassa na Efraimu Uiso, walisema bado baadhi ya wafanyabiashara wadogo wanatumia njia hizo kutokana na kukosa elimu ya forodha na namna bora ya kupitisha bidhaa katika eneo hilo.

Ukurasa 18



Senate yakataa mauzo ya silaha kwa Saudia Arabia

## UCHAMBUZI:

Kakunda: Serikali iigawe Sikonge kusogeza huduma kwa wananchi



Ukurasa 19

## Kimataifa



Kivuli cha Kabila chazidi kuitesa DRC

Ukurasa 14


# siasa

JUMATANO JUNI 26, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Mawaziri wadaiwa kula njama ya kumuua Naibu Rais Ruto

Ukurasa 17

## BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano - 2

MZEE Pius Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Vilevile, Mzee Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu la kuundwa Muungano huo, ameamua kuan-

Endelea 16



Spika wa Bunge mstaafu, Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

## Trump afuta mashambulizi dhidi ya Iran dakika 10 kabla hayajaanza

Ukurasa 20

# Kivuli cha Kabila chazidi kuitesa DRC

• Atajwa katika uamuzi wa kutengua ushindi wa wabunge 33

**Na Mashaka Mgeta**

JOSEPH Kabange Kabila aliingia madarakani mwaka 2001 baada ya kifo cha aliyekuwa mtangulizi na baba yake mzazi, Laurent Desire Kabila aliyeuawa Januari 16, 2001 kwa kupigwa risasi na mlinzi wake.

Baada ya kuwapo madarakani kwa takribani miaka 18, Joseph Kabila aliondoka madarakani Januari 24, mwaka huu, lakini habari za ushawishi wake kisiasa unatajwa kuendelea kuziathiri siasa za ndani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Hata hivyo, Kabila amebaki kimya pasipo kujibu madai hayo, hali inayotafsiriwa kuwa miongoni mwa 'nyenzo' anazozitumia kufanikisha namna bora ya kufanya siasa akiwa nje ya utawala wa Taifa hilo lenye historia ya kughubikwa na migogoro inayosababisha mapigano ya wenyewe kwa wenyewe.

Madai dhidi ya Kabila 'kuzimiliki' siasa na mifumo ya dola katika DRC zilianza kutolewa baada ya Tume ya Uchaguzi (SENI) kumtangaza Felix Tshisekedi kuwa mshindi wa urais katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika Desemba mwaka jana.

Matokeo ya uchaguzi huo yalikipa ushindi wa viti 388 vya ubunge chama cha Peoples' Party for Reconciliation and Democracy (PPRD) cha Kabila kati ya viti 500, wakati Union for Democracy and Social Progress (UDPS) ikipata viti 46 na muungano wa LAMUKA ukapata viti 96.

Kabila akadaiwa kupanga njama na Tshisekedi ili ashinde urais dhidi ya aliyekuwa anapewa nafasi kubwa ya kushinda, Martin Fayulu.

Lakini katika hali ambayo haikutarajiwa, Tshisekedi akatangazwa kuwa mshindi wa urais, hali iliyozua malalamiko ya kuhujumiwa kwa matokeo hayo na kufanikisha azma ya kumuingiza madarakani Rais huyo akitokea upinzani.

**KWA NINI ISINGEKUWA SHADARY**

Swali lililogusa hisia za walio wengi ni kwa sababu gani Kabila, kama alikusudia kuhujumu matokeo ya uchaguzi huo, hakuwezesha aliyekuwa mgombea kupitia chama chake, Ramazani Shadary kushinda?

Lakini wachambuzi kadhaa wa masuala ya siasa wanaeleza kwamba kama ushindi ungeelekezwa kwa Shadary, ingeweza kusababisha upinzani mkubwa na kuibuka maandamano ya kupinga matokeo hayo.

Sasa ni takribani miezi mitano tangu Rais Tshisekedi aingie madarakani akiwa bado hajaunda serikali, lakini Kabila anaendelea 'kuzitikisa' siasa za nchi hiyo.

Miongoni mwa nguvu za Kabila kudaiwa kujikita katika mihimili mikuu ya utawala nchini humo, zinatajwa katika uamuzi wa mahakama kutengua ubunge wa wabunge 33 ambapo 23 kati yao ni kutoka upinzani.

Kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi nchini humo, matokeo yanapotenguliwa na mahakama, nafasi ya ubunge inachukuliwa na mshindi anayefuata, na kwa mujibu wa matokeo ya awali, nafasi hizo zilikuwa za wagombea kutoka upande wa Kabila.

Wabunge wengine nane walitenguliwa wadhifa huo walikuwa kutoka kilichokuwa chama tawala.



Rais Felix Tshisekedi wa DRC (kulia) akiwa na mtangulizi wake Joseph Kabila. **PICHA: MTANDAO**

Mwandishi wa habari, aliyepo Mashariki mwa DRC, John Kanyonyi anasema baada ya uamuzi wa mahakama, watu waliingia mitaani wakichoma matairi barabarani kuonyesha kutoridhishwa kwao na uamuzi huo.

Anasema maeneo yaliyoathiriwa zaidi na vitendo hivyo ni Goma na eneo la Maseke katika Wilaya ya Sake.

Rais wa Chama cha UPDS, Valentine Mubake, anasema mambo yanayotokea hivi sasa nchini humo yanaonyesha namna Kabila alivyojipanga 'kutundika koti lake Ikulu' kabla ya kuondoka madarakani.

Anasema hata majaji sita kati ya nane wa Mahakama ya Katiba iliyobatilisha ushindi wa wabunge hao, waliteuliwa na Kabila alipokuwa madarakani.

"Kwa hiyo mambo hayashangazi kwa maana alijipanga tangu awali...ana vikwazo ambavyo alitaka avishinde, kwa hiyo amejikinga ipasavyo," anasema Mubake katika mahojiano ya mwishoni mwa wiki kupitia DW ya Ujerumani.

Kwa upande wake, Ruben Mikinda anasema tuhuma dhidi ya Kabila hazina mashiko, kwa vile wahusika wengi wanaotoa madai hayo walikuwa kwenye utawala kabla ya kuwa wapinzani.

Mwandishi wa Habari, Saleh Mwanamilongo, anasema mifumo ya kisiasa nchini DRC hivi sasa haitoi taswira ya namna ya uendeshaji wa serikali ya Rais Tshisekedi.

Anasema hata baadhi ya wapinzani wa sasa bado wanatiliwa shaka kwa vile awali walikuwa katika utawala wa Kabila, hivyo wanahisiwa kuwa ni 'mapandikizi' yenye kuiendesha nchi hiyo kwa 'mlango wa nyuma'.

Kwa mujibu wa Mwanamilongo, malalamiko yanayohusiana na kukosa mwelekeo bora wa kuiongoza DRC yanatolewa pia hata ndani ya chama cha Kabila.

Mwandishi wa habari mwingine anayeishi Mashariki mwa DRC, John Kanyonyi anasema 'ndoa' ya kisiasa kati ya Kabila na Rais Tshisekedi inaweza kuliathiri taifa hilo kama jitihada za kuiweka wazi kwa umma hazitafanyika.

Kanyonyi anasema taarifa zilizopo ni kwamba upande wa Rais Tshisekedi na ule wa Kabila, zinavutana kuhusu kuundwa kwa serikali.

Anaeleza kuwa chama cha Kabila kinataka kupata idadi kubwa ya mawaziri zikiwamo 'wizara nyeti' zinazotakiwa pia na upande wa Rais Tshisekedi.

Suala jingine linalotajwa ni mtu wa kuchukua nafasi ya Waziri Mkuu ambapo Kinyonyi anasema "huenda kukatokea mpasuko kama pande zote hazitawaweka pamoja watu wao."

> "Kwa hiyo mambo hayashangazi kwa maana alijipanga tangu awali... ana vikwazo ambavyo alitaka avishinde, kwa hiyo amejikinga ipasavyo," anasema Mubake katika mahojiano ya mwishoni mwa wiki kupitia DW ya Ujerumani.

Anasema dalili hizo zinadhihirika wazi katika ukanda wa Mashariki mwa DRC, anapokuita kuwa ni kitivo kwa masuala kama siasa, uchaguzi na usalama.

Valentine anasema matokeo hayo yanapowianishwa na mambo yanayotokea DRC kwa sasa, yanatoa tafsiri kwamba uchaguzi mkuu uliopita ulikuwa mfano wa kiini macho, na kwamba mambo yote yalipangwa ili kufanikisha hujuma dhidi ya uamuzi wa walio wengi nchini humo.

Valentine anazitaja taasisi za nchi hiyo zenye ushawishi kutoka kwa Kabila kuwa ni Bunge dogo na Bunge la Taifa, serikali, Jeshi na Polisi.

Hata hivyo, Mikindu anapinga hoja hizo na kusema Valentine alikuwa mshauri wa Tshisekedi, hivyo kama kuna kasoro anazoziona anapaswa kutambua kwamba nyingine zinatokana na ushauri wake.

Kuhusu chama cha Tshisekedi kupata idadi ndogo ya wabunge ikilinganishwa na wale wa upande wa Kabila, Mikindu anasema suala la msingi ni kufanya kazi kwa bidii katika kuwatumikia wananchi.

Anatoa mfano kuwa kuna wakati chama hicho kilikuwa na wabunge 12 kati ya 212 wa Bunge la Taifa, lakini walifanikiwa kuibua mageuzi yaliyobadilisha mifumo kandamizi nchini humo.

"Hata sasa tunapokuwa wachache ndani ya Bunge haina shida, kama tukiwa na nia moja tutafaulu tu," anasema.

Mikindu anasema ukosoaji unaofanywa dhidi ya Seni una mashiko kama ilivyo kwa serikali na kwamba yatafanyiwa kazi, ili kuleta mageuzi yenye tija kwa nchi na watu wake.

Kwa upande wake, Mwanamilongo anasema kinachopaswa kufanyika sasa kwa raia wa DRC ni kumpa nafasi Rais Tshisekedi ambaye hadi sasa bado hajaunda serikali yake.

"Hata hivyo bado ana kibarua kikubwa katika kuleta mageuzi nchini DRC," anasema Mwanamilongo.

**NAFASI YA KATUMBI**

Moses Katumbi ni mmoja wa wanasiasa wa upinzani waliokuwa wanamuunga mkono Fayulu, akitokea nje ya nchi alipokuwa anaishi baada ya kuikimbia DRC wakati wa utawala wa Kabila.

Lakini Mubake anasema ni vigumu kuamini kwamba Katumbi na Kabila wanaweza kukosana kwa vile wana maslahi kwenye kampuni za madini nchini humo.

*Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia simu namba 0754691540 ama barua pepe: HYPERLINK "mailto:mgeta2000@yahoo.com" mgeta2000@yahoo.com*

UCHAMBUZI

# Ethiopia; Watemi Amhara wamchoka Abiy, wataka kurudi madarakani

**Na Ani Jozeni**

JESHI nchini Ethiopia na serikali ya Waziri Mkuu Abiy Ahmed wamekuwa katika wakati mgumu mwishoni mwa wiki kukabiliana na jaribio la kuiangusha serikali, ambalo hata hivyo inaelekea lilielekezwa kwa utawala wa Jimbo la Kaskazini la Amhara.

Taarifa zilisema watu wanne waliuawa akiwamo mkuu wa majeshi ya Ethiopia na mkuu wa (rais) wa Jimbo la Amhara, katika jaribio la uasi lililoanza jioni ya Jumamosi.

Jenerali mmoja wa jeshi alifanya jaribio la kuteka makao makuu ya jimbo la Kaskazini, na inaelekea angetumia ngome hiyo kuondoa utawala wa Abiy Ahmed ili kurudisha udikteta.

Mkuu wa majeshi, Jenerali Seare Mekonnen aliuawa kwa kupigwa risasi nyumbani kwake jijini Addis Ababa na mlinzi wake, ishara kuwa mlinzi huyo alikuwa sehemu ya mtandao wa uasi Kaskazini ili kurudisha serikali inayodhibitiwa na maofisa wa kijeshi kutoka Kaskazini.

Ni jimbo la utawala nchini humo kwa karne zote, kiasi kwamba utawala wa Abiy Ahmed kutoka Jimbo la Oromo unaonekana haukubaliki kwa watemi hao wa Kaskazini, wakitaka kurudisha utawala ambao jeshi linajisikia vyema, na nguvu ya maofisa kutoka Kaskazini haina mashaka. Waziri Mkuu Abiy amewaudhi kwa vita kali dhidi ya rushwa.

Tangu aingie madarakani baada ya machafuko ya miezi kadhaa yaliyofikia chama tawala chenye msingi wake jeshini kumwondoa aliyekuwa Waziri Mkuu, Hailemariam Desalegn (2012-2018) na kabla ya hapo, Meles Zenawi (1995-2012).

Ethiopia ni nchi ambayo imekuwa na machafuko ya mara kwa mara na kupindua serikali kuanzia miaka ya 1960, ambako majaribio kadhaa yameshindwa na mengine kufaulu, kwa mfano mwaka 1960 jaribio la kumpindua Mfalme Haile Selassie lilishindwa.

Lakini mwaka 1974 wakati wa janga la njaa, jeshi lilimwondoa mfalme na kuitumbukiza Ethiopia katika vita ya kimapinduzi.

Katika shambulio dhidi ya Jenerali Seare, jenerali mmoja mstaafu aliyekuwa anamtembelea nyumbani kwake naye aliuawa, lakini vikosi vya usalama vilifaulu kumkamata mlinzi wa jenerali huyo.

Kiongozi wa jimbo la Amhara, Ambachew Mekonnen anasemekana kuwa alikuwa mtu wa karibu na Abiy, naye aliuawa pamoja na mshauri wake, Gize Abera.

Abiy alisema katika hotuba aliyoitoa kwa taifa Jumapili kuwa kiongozi wa Jimbo la Amhara alipigwa risasi na watu walio karibu naye, na kuwa matukio hayo mawili ya ushambuliaji, dhidi ya mkuu wa majeshi na dhidi ya mkuu wa jimbo, yalikuwa na lengo moja.

Taarifa zilisema kuwa jaribio hilo la kuteka serikali ya jimbo na kupunguza uzuiaji wa harakati hiyo katika utawala wa jeshi la Ethiopia liliandaliwa na mkuu wa usalama wa jimbo la Amhara, Jenerali Asamnew Tsige.

Aliachiwa kutoka jela mwaka jana ambako alipata msamaha baada ya kushiriki jaribio lingine la kupindua serikali, halafu akarudishwa katika nafasi yake jeshini.

Viongozi wa jimbo la Amhara walikuwa katika mkutano wakijadili hatua za kuchukuliwa kufuatia wimbi la kuandikisha askari wa kujitolea alilokuwa akiendesha Jenerali Tsige wakati jaribio la kupindua serikali hiyo lilipoanza.

Vyombo vya habari vilisema kuwa wiki moja kabla, Jenerali Tsige alitoa ushauri wa wazi kwa watu wa Amhara, moja ya majimbo yenye watu wengi zaidi nchini humo, kutwaa silaha, kwa kutumbukiza video katika 'facebook' yenye ushauri huo.

Milio ya risasi ilisikika karibu na uwanja wa ndege wa kimataifa wa Bole saa tano na nusu usiku Jumamosi na baadhi ya barabara zilikuwa zimefungwa.

Ubalozi wa Marekani ulitoa tahadhari kwa wafanyakazi wake wasitoke katika maskani yao ubalozini, tahadhari iliyokuwa na mashiko zaidi ukilinganisha na ile iliyotolewa kuwa magaidi walikuwa na nia ya kushambulia eneo la Masaki jijini Dar es Salaam.

Ni taarifa iliyoleta kiwewe na kuwakasirisha wakuu wa vyombo vya usalama nchini, lakini nchini Ethiopia ubalozi huo haukugundua mpango kama huo licha ya dhamira ya kuinua uasi kuonekana katika 'facebook,' na risasi zilipoanza ndipo ukawashtua raia wake.

Kitaaluma, ni rahisi zaidi kutumia utaalamu kwa suala la kutafuta, na si kugundua mpango halisi wa siri.

Baadaye Jumamosi, mkuu wa vikosi maalum vya jeshi jimboni Amhara, Jenerali Tefera Mamo aliiambia televisheni ya taifa kuwa waliojaribu kufanya mapinduzi ya kijeshi wamekamatwa, ingawa wapo wachache walioponyoka.

Waziri Mkuu Abiy akasema Jumapili kuwa Jimbo la Amhara limedhibitiwa kikamilifu na Serikali ya Shirikisho ilishirikiana na Serikali ya Jimbo, ingawa taarifa zilizoingia katika vyombo vya habari vya kimataifa, na matamshi ya Abiy Ahmed, hayakufafanua misukumo jimboni Amhara iliyoielekeza katika jaribio la kupindua serikali ya jimbo, kuandikisha askari kwa uasi, n.k.

Ila tu inaelekea ni kutokufurahishwa na mabadiliko ambayo Abiy ameyasimamia tangu aingie madarakani mwezi Februari mwaka jana, ambako ni mara ya kwanza asiye wa jinbo la Amhara kuongoza Ethiopia.

Ethiopia ni nchi ya pili kwa wingi wa watu barani Afrika ikiwa na watu zaidi ya milioni 100, ambako jimbo la Amhara kwa miongo kadhaa limekuwa likitoa wakuu wa nchi na hata sasa maofisa wengi wa ngazi za juu wanatokea jimboni humo, kwa mfano mkuu wa majeshi aliyeuawa.

Waliojaribu kupindua serikali wanaonekana kutaka utawala uliotangulia kurudi, licha ya kuwa haukuwa unaungwa mkono na watu hivyo kukawa na maandamano makubwa hadi waziri mkuu Desalegn akaachia ngazi.

Inaelekea ni kutokutaka mageuzi, kuunda serikali ya jimbo kuitumia kutaka mabadiliko serikali kuu, kwani kujitenga na Ethiopia isingewezekana.

Wako wanaodhania kuwa kinachoendelea nchini Sudan kimewapa nguvu wapinga maendeleo nchini Ethiopia, ambako vikosi maalum nchini Sudan vikijulikana kwa jina la Janjaweed ndivyo viko madarakani hivi sasa.

Vikosi hivyo ni ngome ya aliyekuwa rais wa muda mrefu wa Sudan, Jenerali Omar el Bashir, aliyeondolewa madarakani na waandamanaji wanaotaka demokrasia lakini sasa wanapata tabu kuiondoa Janjaweed madarakani.

Waziri Mkuu Abiy amekuwa akitafuta suluhu kati ya waandamanaji na utawala wa kijeshi ukisimamiwa na Jenerali Mohamed 'Hemeti' Dagalo, Naibu Mwenyekiti wa Baraza la Kijeshi na Mkuu wa Vikosi Maalum.

Bado hakuna ushahidi kuwa utawala wa Sudan ungeweza kutafuta washirika Ethiopia kupunguza msukumo na ushawishi wa Abiy Ahmed asiendelee kuingilia siasa za Sudan, kulisumbua jeshi.

Nchi za Sudan na Ethiopia zina historia ndefu ya hujuma ambako Sudan iliunga mkono jimbo la Eritrea kujitenga nchini Ethiopia katika vita ya wenyewe kwa wenyewe iliyodumu miaka mingi, hadi 1991.

Ethiopia nayo ikaunga mkono Sudan Kusini kujitenga katika vita ndefu iliyoishia uhuru wa nchi hiyo 2011 na imekuwa ikisimamia mwendelezo wa mapambano ya wenyewe kwa wenyewe baada ya uhuru, hasa ikisaidia upande dhaifu zaidi wa kiongozi wa uasi Dk. Riek Machar dhidi ya Rais Salva Kiir.

Hakuna nchi nyingine katika Afrika au kwingineko duniani iliyojaribu kuingilia suala la Sudan isipokuwa Ethiopia, hivyo ni kuichokoza Janjaweed, ishtuke.

Kwa upande mwingine, kukwama kwa mabadiliko ya kisiasa kuelekea utawala wa kidemokrasia nchini Sudan, kumetoa ishara kwa wahafidhina nchini Ethiopia kuwa mageuzi yanaweza kubatilishwa, endapo kutakuwa na uwepo wa vikosi maalum au jeshi la kujitolea angalau kujitwalia madaraka katika Jimbo la Kaskazini.

Ni kama Janjaweed nchini Sudan ilivyopata umaarufu kwa kudhibiti hali ya sasa jimboni Darfur kwa kuwezesha makundi ya watemi wa Kaskazini ya Sudan kujipanua huko, kuchoma moto vijiji na kukamata ng'ombe na ardhi, aina ya vita iliyoenea ukanda wote wa Sahel barani Afrika, ikiwemo Sudan Kusini, Nigeria na kwingine kuliko na machafuko ukanda wa Afrika Magharibi.

Inaelekea kuwa wahafidhina nchini Ethiopia wameridhishwa na jinsi jeshi Sudan lilivyokataa ukamilishaji wa mageuzi.

Matabaka tawala ya Sudan yakiongozwa na chama cha kizalendo cha siasa kali kilichomtumia Omar el Bashir madarakani na kupindua makundi ya wasaidizi wake, kikagawanyika likaundwa kundi la u-Mahdi likiongozwa na hayati Sadiq el Mahdi yanaangalia kwa makini kama demokrasia itafaulu.

Kuutingisha utawala wa Abiy Ahmed katika wakati huu, hata kama hakutokani na Janjaweed, ni kama baraka kwao.



Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed. **PICHA: MTANDAO**

UCHAMBUZI

**Inatoka Uk. 13**

dika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa.

Wiki iliyopita tulianza na utangulizi wa kitabu hicho na tukaishia mwisho wa Sura ya Kwanza. Sasa fuatilia kuanzia Sura ya Pili ya kitabu hicho inayoanza na sababu za kuanzishwa kwa Muungano...

SABABU ZILIZOCHOCHEA KUANZISHWA KWA MUUNGANO

Kulikuwa na sababu kubwa tatu, ambazo zilichochea upatikanaji wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika kipindi hicho husika, na katika mazingira husika ya wakati huo. Sababu hizi zinatajwa na kufafanuliwa vizuri zaidi hapo chini:

2.1. Shauku kubwa ya kupatikana kwa Umoja wa Afrika

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, pamoja na Rais Abeid Aman Karume wa Zanzibar, wote wawili walikuwa ni waumini wakubwa wa upatikanaji wa Umoja wa Bara la Afrika.


Kwa upande wa Mwalimu Nyerere, ushahidi wa imani yake hiyo umo katika baadhi ya hotuba zake alizokuwa akizitoa katika vipindi husika, na vilevile, katika baadhi ya maandiko yake. Lakini, pia, aliamini kwamba, Umoja huo haungeweza kupatikana kwa kuunganisha nchi zote za Bara hili kwa wakati mmoja. Kwahiyo, aliunga mkono juhudi za kuanza kwa kuunganisha baadhi ya nchi zilizokuwa katika kanda moja, kama njia ya mpito kuelekea kwenye Muungano wa Bara zima la Afrika. Ndiyo sababu alichangamkia na kushabikia sana suala la kuundwa kwa Shirikisho la nchi tatu za Afrika Mashariki za Kenya, Tanganyika na Uganda.

Hapana shaka kwamba, shauku hiyo ya kutaka kuona nchi za Afrika zikiungana, ilikuwa ni sababu mojawapo kubwa iliyochochea kupatikana kwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar 26 Aprili, 1964. Hii inadhihirishwa na hotuba ya Rais Nyerere ya kuliomba Bunge la Tanganyika likubali kuridhia Mkataba wa Muungano baina ya Tanganyika na Zanzibar aliyoitoa katika Bunge hilo tarehe 25 Aprili, 1964, Rais Nyerere alisema hivi:

"Leo kuna tamaa kubwa sana ya umoja katika Afrika. Mioyo ya Waafrika ina shauku kubwa ajabu ya kuungana tuwe kitu kimoja... Lakini, pamoja na kujivunia shauku hii, yafaa tukumbuke kuwa, umoja hautakuja kwa sababu ya shauku tu na maneno matupu. Hatua lazima zichukuliwe za kuonesha kwamba, shauku hii na matumaini haya si ndoto isiyowezekana, bali ni jambo linaloweza kutimia... Hivyo basi, ikiwa nchi ambazo ni marafiki na ni jirani zikiweza kuungana, Muungano huo waweza kuwa ni thibitisho la vitendo kwamba, matumaini ya Bara letu si ya bure. Kwamba, nchi mbili zikiweza kuungana na kuwa nchi moja, basi, tatu zinaweza, na ikiwa tatu zinaweza , basi thelathini zinaweza."

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano - 2



Waasisi wa Muungano, Mwalimu Julius Nyerere (kushoto), akiwa na Mzee Abeid Amani Karume. **PICHA: MTANDAO**

"Tanganyika na Zanzibar ni nchi ndugu. Tunashirikiana kwa historia, lugha, mila, tabia na siasa. Udugu wa Afro – Shirazi Party na TANU wote mnaufahamu. Udugu wa viongozi wa vyama hivi viwili haukuanza jana. Basi...

Aidha, Rais Mwalimu Nyerere aliendelea kama ifuatavyo:

"Tanganyika na Zanzibar ni nchi ndugu. Tunashirikiana kwa historia, lugha, mila, tabia na siasa. Udugu wa Afro – Shirazi Party na TANU wote mnaufahamu. Udugu wa viongozi wa vyama hivi viwili haukuanza jana. Basi, tunazo sababu zote hizo za kutufanya tuungane na kuwa kitu kimoja. Juu ya yote hayo, kuna shauku ya Umoja wa Bara la Afrika. Basi, kwa kuzingatia yote hayo, mimi, kwa niaba yenu, na Rais Karume kwa niaba ya ndugu zetu wa Unguja na Pemba siku ya tarehe 22 mwezi huu, tukatia saini mkataba wa umoja baina ya nchi zetu mbili.

Mnao mkataba huu na mtaujadili. Endapo Bunge hili, pamoja na Baraza la Mapinduzi la Zanzibar, yataukubali mkataba huu, nchi zetu zitakuwa nchi moja. Siyo nia yangu kueleza mkataba wenyewe. Mtaelezwa wakati wa majadiliano. Kazi yangu ni kuwaombeni muukubali mkataba huu".

Kwa upande wake, Sheikh Abeid Amani Karume vilevile alikuwa ni muumini mkubwa wa Umoja wa Afrika tangu alipokuwa anapigania Uhuru wa Zanzibar. Kwa hiyo, mafanikio ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964, ambayo yalimuweka Sheikh Karume katika madaraka ya kuwa Rais wa Zanzibar, yalitoa nafasi na fursa nzuri sana kwa Viongozi hawa wawili, Mwalimu Nyerere akiwa Rais wa Tanganyika, na Sheikh Karume akiwa Rais wa Zanzibar, ya kuweza kuzungumza na kuafikiana juu ya suala la kuunganisha nchi zetu mbili, ikiwa ni hatua ya mpito kuelekea kwenye Umoja wa Afrika.

**2.1.1** Matumaini ya Umoja wa Afrika

Kwa hakika, katika kipindi hicho, matumaini ya kupatikana kwa umoja wa Afrika hayakuwa ni ndoto tu, kwa sababu kulikuwa na hatua mahsusi zilizokuwa zikichukuliwa za kuunganisha baadhi ya nchi za Afrika kwa kuanzia na baadhi ya kanda za Bara hili.

Kwa mfano, katika Kanda ya Afrika Mashariki, kulikuwa na juhudi zinaendelea za kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki. Hali kadhalika, katika Kanda ya Afika Magharibi, kulikuwa na mafanikio yaliyopatikana ya kuunganisha nchi za Ghana, Guinea, na Mali. Aidha, kulikuwa na Muungano mwingine ulioundwa na nchi za Senegali na Gambia, ambao ulizaa nchi iliyoitwa Senegambia.

Ni bahati mbaya kwamba, Muungano wa nchi zote hizo baadaye ulisambaratika. Na ni bahati mbaya vilevile, kwamba juhudi za kuundwa Shirikisho la Afrika Mashariki nazo hazikufanikiwa.

Lakini, ni kweli kabisa kwamba juhudi hizo za kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki, zilichangia kwa kiwango kikubwa katika kuziwezesha nchi za Tanganyika na Zanzibar kuungana katika wakati huo zilipoungana.

**2.1.2** Juhudi za Kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki

Katika kipindi hicho, kulikuwa vilevile na mazingira yenye matumaini makubwa ya kuanzishwa kwa Shirikisho la nchi za Tanganyika, Kenya na Uganda, ambalo lingejulikana kama Shirikisho la Afrika Mashariki. Ushahidi wake ni kwamba mnamo mwezi Juni mwaka 1963, lilitolewa Tamko moja zito, ambalo lilitolewa kwa pamoja na marais wa nchi hizi tatu. Tamko hilo liliutangazia ulimwengu nia waliyokuwa nayo wakuu hao, ya kuunda Shirikisho la Afrika Mashariki kabla ya mwisho wa mwaka huo wa 1963. Kwa kuwa wakati huo Zanzibar ilikuwa bado haijapata uhuru wake, haikuweza kushirikishwa katika tamko hilo.

Bahati mbaya tamko hilo, pamoja na uzito wake mkubwa, halikufuatiwa na hatua zozote za utekelezaji, na mwaka huo ukapita bila Shirikisho hilo kuwa limeundwa.

Lakini, bado matumaini yaliendelea kuwapo, kwani mwezi Machi 1964, wabunge wa Kenya waliitisha kikao cha pamoja na wabunge wenzao wa Uganda na Tanganyika, kwa madhumuni ya kushinikiza utekelezaji wa tamko hilo. Wabunge wa Uganda hawakujibu mwaliko waliopelekewa. Lakini, wabunge wa Tanganyika na wenzao wa Kenya walikutana; na baada ya majadiliano, walipitisha Azimio la kutaka lile tamko la wakuu wa nchi hizi litekelezwe mara moja. Na kwa madhumuni ya ufuatiliaji, waliteua ujumbe mdogo kutoka miongoni mwao wa kwenda kwa Wakuu wote wa nchi hizi tatu, kujaribu kushinikiza utekelezaji wa Tamko lao hilo.

**2.1.3** Wazo la kuunganisha Tanganyika na Zanzibar lilipoibuka

Wakati hayo yakiendelea, mazungumzo tayari yalikwisha kuanza baina ya marais Nyerere na Karume juu ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Juhudi hizi za wabunge ziliwapa marais Nyerere na Karume matumaini ya kupatikana kwa shirikisho hilo ndani ya muda mfupi, hata wakafikiria uwezekano wa kusubiri kidogo hadi wenzao wa Kenya na Uganda watakapokuwa tayari, ili nchi zote nne ziweze kuingia kwa pamoja katika Shirikisho la Afrika Mashariki. Lakini, kuna mambo mawili yaliyotokea, ambayo waliyafanya waachane na wazo hilo la kusubiri. Moja, ni kile kitendo cha wabunge wa Uganda cha kutokushirikina na wenzao katika juhudi hizo, ambacho kiliwatia mashaka makubwa kama kweli shirikisho hilo litapatikana katika muda mfupi waliokuwa wakiutegemea. La pili, lilikuwa ni haja ya kuimarisha ulinzi wa nchi hizi. Katika mazingira yaliyokuwapo wakati huo, husasan, uhasama mkubwa uliokuwapo duniani kote baina ya nchi za kikomunisti za Mashariki; na zile za kibepari za Magharibi; suala la kuimarisha ulinzi na usalama wa Tanganyika na Zanzibar lisingeweza kusubiri, kama yalivyofafanuliwa katika kipengere cha 2.2 sura hii. Kwahiyo, Wakuu wetu wakaamua kuendelea tu na mpango wao wa kufanikisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar bila kuchelewa zaidi.

**2.2** Haja ya kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi hizi mbili

Itakumbukwa kwamba Mapinduzi ya Zanzibar yaliyomweka Rais Karume madarakani yalitokea mwezi Januari, 1964. Kwa hiyo katika kipindi kifupi kilichofuatia mara baada ya Mapinduzi hayo, kulikuwa na hofu kwamba huenda wale watawala waliopinduliwa wangeweza kurudi na kufanya mapinduzi mengine ya kuwarejesha wao madarakani. Katika muda mfupi huo, Zanzibar ilikuwa bado haijawa na jeshi lake la kujihami dhidi ya uvamizi kama huo. Lakini, hofu haikuwa kwa Zanzibar tu, kwani kama uvamizi huo ungetokea, basi, athari zake zingesambaa na kuvuka hadi Tanganyika; kwa kuwa, kama alivyosema Mwalimu Nyerere katika hotuba yake niliyoinukuu hapo juu,

"Tanganyika na Zanzibar ni nchi ndugu. Tunashirikiana kwa historia, lugha, mila, tabia na siasa."

Hofu ya uvamizi kama huo bila shaka nayo ilichangia katika kufikia uamuzi wa kuunganisha nchi hizi katika muda na wakati zilipoungana.

Lakini, hata bila kuwapo kwa hofu hiyo maalum, bado kuna haja kwa nchi yoyote kuweka ulinzi wa mipaka yake, na usalama wa raia wake. Ndiyo maana kila nchi huwa inaunda majeshi husika ya kufanya kazi hiyo, pamoja na kuweka mafungu maalum ya fedha katika bajeti yake ya kila mwaka kwa ajili ya kulipia gharama za majeshi hayo. Kutokana kuwepo kwa Muungano huu, Serikali ya Zanzibar haikuwa na haja tena ya kuweka mafungu ya fedha za ulinzi wa Jamhuri ya Muungano, pamoja na usalama wa raia wake, zinalipwa na Serikali ya Muungano.

**ITAENDELLEA WIKI IJAYO**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (aliyesimama) aki hutubia moja ya mikutano Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

## Mawaziri wadaiwa kula njama ya kumuua Naibu Rais Ruto

MAWAZIRI watatu wa Kenya, Peter Munya wa Viwanda, Cecilly Kariuki wa Afya na Joe Mucheru wa Teknolojia na Mawasiliano, wamehojiwa kwenye Ofisi ya Makao Makuu ya Upelelezi jijini Nairobi, kuhusiana na madai ya kupanga njama ya kumuua Naibu wa Rais William Ruto.



Naibu Rais wa Kenya, William Ruto. **PICHA: MTANDAO**

Hata hivyo, mawaziri hao wamekanusha madai hayo ya kupanga njama ya kumuua kiongozi huyo ili kuzuia azma yake ya kuwania kiti cha urais katika uchaguzi mkuu ujao.

Aidha, wamekataa kuandikisha taarifa wakisema kuwa naibu huyo wa rais hajawasilisha malalamiko rasmi kituo cha polisi.

Ruto ndiye mwanasiasa mkuu ambaye anatazamiwa kumrithi Rais Uhuru Kenyatta, pindi atakapokamilisha utawala wake.

Akizungumza na wanahabari kwa niaba ya wenzake, Munya anasema kuwa madai hayo hayana msingi wowote.

Hata hivyo, anakiri kuwepo kwa mikutano ambayo imekuwa ikifanyika kuhusu maendeleo ya eneo la Mlima Kenya, anakotokea Rais Kenyatta.

"Kwanza hakuna malalamiko yoyote ambayo yameandikishwa kwenye kitabu cha matukio, ambayo tunaweza kuyajibu hata kama tungetaka, hakuna malalamiko," anasema.

Munya anabainisha kuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai aliwataka wafike makao makuu ya upelelezi, baada ya Ruto kulalamika kupitia mawasiliano kwa njia ya simu.

Watu hao wanasema kuwa wana uhuru wa mahusiano na kwamba mkutano wao umetokana na ukweli kwamba eneo hilo limetengwa kwenye masuala ya maendeleo.

Gavana huyo wa zamani wa Jimbo la Meru pia anasema kuwa Rais Kenyatta alimpa jukumu la kuandaa mikutano kati ya viongozi na maofisa wa serikali kutafuta suluhisho la matatizo ya wakazi wa Mlima Kenya.

"Bila shaka haya ni madai mazito, hasa yanapotoka kwa mtu wa hadhi na ofisi ya naibu rais...nilitarajia mtu wa hadhi hiyo, kufanya uchunguzi wa kina, kabla ya kukurupuka na madai hayo...nadhani ni ukosefu wa uwajibikaji," Munya anasema.

Kwa mujibu wa mawaziri hao wanaotokea Mlima Kenya, Ruto anadai kuwa baadhi ya maofisa serikalini kutoka eneo hilo walikuwa wanafanya mikutano ya siri ya jinsi ya kumuua.

Njama hizo kwa mujibu wa Ruto ni za kumzuia kutowania kiti cha urais baada ya Kenyatta kumaliza mihula yake.

Kwenye Baraza la Mawaziri ambalo hufanyika kila juma, Ruto hajawahi kuibua madai hayo.

"Watu wengi wanasumbuka eti mimi natembea Kenya hii... wanataka niende wapi na siku ya kwenda mbinguni haijafika...hata kwenda mbinguni nimejipanga pia. Kwa sababu Yesu hajarudi, mimi nitatembea Kenya hii," anasema Ruto.

Matukio haya ni ishara kuwa chombo cha Jubilee kinazidi kuzama kwenye bahari, kama kitaibuka baada ya misukosuko hii, ni suala jingine.

**DW**

# Senate yakataa mauzo ya silaha kwa Saudia Arabia

## • UN yamtaja mwanamfalme kumuua Khashoggi



Mwanamfalme wa Saudia, Mohamed bin Salman. **PICHA: MTANDAO**



Marehemu Jamal Khashoggi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Nimi Mweta**

WIMBI la kutokukubalika kimataifa linamnyemelea mwanamfalme Mohamed bin Salman licha ya kuwa si rahisi kwa wapinzani wake duniani kote kuchukua hatua yoyote ya kulenga kupatikana kwa uwajibikaji.

Hiyo ni kuhusiana na kuuawa kwa mwandishi mkongwe Jamal Khashoggi ubalozini Uturuki mwaka jana.

Baraza la Senate la Marekani lilipiga kura iliyoafikiwa na wajumbe 53 dhidi ya 45 kwa azimio la kuzuia mauzo ya silaha zenye thamani ya mabilioni ya dola za Marekani kwa Saudi Arabia na Falme za Kiarabu (Emirates).

Ni azimio ambalo linalenga kukosoa na kusahihisha sera za Rais Donald Trump anayepuuzia mauaji hayo au umwagaji damu Yemen, ili tu kuuza silaha.

Nchini Uingereza uamuzi wa Mahakama kuwa mwanamfalme huyo anahusika na mauaji ya Khashoggi ulifikia kufutwa kwa leseni mpya za kuuza silaha kwa Saudia, wakati mratibu maalum wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu anayechunguza mauaji nje ya mifumo ya kisheria (yaani bila kufikishwa mahakamani) ilitoa taarifa baada ya uchunguzi mrefu.

Ilieleza kwa kina jinsi ambavyo yaliyotokea katika ubalozi wa Saudia jijini Istanbul yasingeweza kufanyika nje ya amri ya mwanamfalme MBS, Shirika hilo pia lilitoa tamko la kutaka kesi inayoendelea Saudia kuhusu mauaji ya Khashoggi iondolewe; xxx hailengi wahusika halisi, katu.

Taarifa nchini Marekani zinasema kuwa Rais Trump ameahidi kwamba kama azimio la Senate litafika mezani kwake, na hakuna shaka kuwa litafika, atatumia haki yake ya 'veto' kulikataa, hivyo ina maana anaweza bado kuuza silaha lakini atapata tabu sana kujieleza kote nchini.

Kwa sababu tayari ameshazindua kampeni ya kuchaguliwa tena mwakani, Rais Trump atajiongezea washindani hata kwenye chama cha Republican ambao wana wasiwasi mkubwa na kufungamana na watawala wa kiimla kama Rais Vladimir Putin wa Russia na Mohamed bin Salman, Saudia.

Licha ya kutaka faida kuuza silaha, wanataka iwe kwa nchi isiyo na dosari za wazi kama Saudia.

Agnes Callamard, mratibu wa kupeleleza mauaji nje ya mifumo ya sheria, alieleza kwa kina jinsi utawala wa Saudia ulivyopanga na kutekeleza mauaji ya mwandishi huyo nguli, ambaye taarifa za kiintelijensia nchini Marekani zilisema alikuwa anafuatilia ushahidi kuwa Saudia ilitumia silaha za kemikali katika vita yake nchini Yemen.

Watu wa karibu na Khashoggi waliojua anafuatia taarifa hizo wanasema punde walipoisikia kuwa suala hilo limempa wasiwasi na alikuwa anatafuta ushahidi wa kimaandishi wa tukio hilo, ndipo akapotea.

Saudia mwanzoni ilianza kwa kukataa kuwa mwandishi huyo hata alifika ubalozini, wakaumbuliwa na video.

Taarifa ya 'Human Rights Watch' ililenga pia kutoa vithibitisho vya vitendo vingi vya kukiuka haki za binadamu nchini Saudia kwenyewe na katika vita ya mbaya inayoiendesha nchini Yemen dhidi ya wapinzani wa dhehebu la Shia wanaotaka kuondoa madarakani serikali inayoutii ufalme wa Saudia.

Marekani imeweka vikwazo kwa maofisa 17 wa Saudia ambavyo havimgusi bosi wa kila kitu nchini humo, mwanamfalme bin Salman, na utawala wa Trump umeendelea kuuza silaha za mabilioni ya dola kwa Saudia.

Ndiyo sasa wajumbe wengi wa mabaraza yote mawili ya Congress, lile la Wawakilishi halafu la Senate, wameonyesha kuchoshwa kabisa na hali hiyo.

Ukiongezea Trump kuikingia kifua Russia kuingilia uchaguzi 2016, tatizo linaweza kumwathiri.

Upande mwingine wa msukumo dhidi ya MbS nchini Marekani ni kusekwa kizuizini kwa wanaharakati wanawake nchini Saudia, wanaotaka haki za wanawake zipanuliwe na siyo tu kuruhusiwa kuendesha magari bila kufuatana na waume zao au wana wa kiume wenye umri unaoridhisha.

Taarifa zilizoanza kusikika baada ya mauaji ya Khashoggi zilisema kuwa mauaji hayo siyo ya mwandishi tu nguli aliyekuwa akifuatilia habari nyeti, ila ni mkanganyiko wa kiintelijensia ambako mhanga huyo alikuwa mhusika wa karibu na utawala wa kifalme.

Alikuwa rafiki wa karibu wa mkuu wa ujasusi nchini humo (inaelekea aliondolewa na MbS katika kampeni iliyosemekana ni dhidi ya rushwa baada ya kuingia madarakani chini ya baba yake, Mfalme Salman ibn Abdulaziz.

Anasemekana ni mkereketwa wa itikadi kali, mwanachama wa 'Muslim Brotherhood' kama ile ya kina hayati Mohamed Morsi nchini Misri inayopigwa vita mbaya na jeshi la nchi hiyo; alikuwa rafiki wa Osama bin Laden na kushiriki au kuunga mkono mapambano yake (kupitia Al Qaeda) nchini Afghanistan.

Baada ya MbS kuchukua madaraka na kuanza kuwasakama watawala waliotangulia katika ukoo wa kifalme, alihamia Marekani na kuanza kuandika safu katika gazeti mashuhuri la Washington Post, la mwelekeo wa kiliberali.

Kukamilika kwa uchunguzi kuhusu kuuawa Khashoggi kumeonyesha jinsi mashirika ya UN yasivyoweza kufanya lolote pale nchi wanachama wakiwa na maslahi tofauti kwa suala fulani ukilinganisha na taarifa husika ya chombo kimojawapo cha UN.

> Kukamilika kwa uchunguzi kuhusu kuuawa Khashoggi kumeonyesha jinsi mashirika ya UN yasivyoweza kufanya lolote pale nchi wanachama wakiwa na maslahi tofauti kwa suala fulani ukilinganisha na taarifa husika ya chombo kimojawapo cha UN.

Nguvu ya Saudia kama soko la uhakika la silaha za Marekani imehakikisha kuwa inazuia vilivyo kuingizwa katika mkondo wa uwajibikaji, huku utawala wa Trump ukifumba macho usione kabisa ushahidi kuhusu amri ya kuuawa kwa mwandishi Khashoggi.

Ili iendelee kuuza silaha kubwa na nzito kwa Saudia, inabidi utawala wa Trump ukwepe taarifa za kina za haki za binadamu, utake tu kuendeleza uchunguzi.

Jambo ambalo bado haliko bayana ni kama kuna uwezekano wowote katika siku za usoni, au tuseme miaka ya karibuni, kwa harakati nchini Saudia zivuke mipaka ya kudai tu haki za wanawake na kuwa sehemu ya hitaji la demokrasia na haki za binadamu kama katika nchi nyingine za Kiarabu.

Kichocheo cha hali hiyo kinaweza kuwa ni vita ya Yemen, kwani siku zinavyokwenda inaonekana kuwa kutumia silaha za nguvu na kuteketeza sehemu kubwa ya Yemen kwa mabomu ili kuvunja ngome za waasi wa mweleko wa ki-Houthi kumeshindwa kumaliza hali hiyo.

Hivi karibuni vikundi vya waasi hao vimekuwa vikiingia Saudia na hata kuharibu miundombinu, hali inayodhoofisha utii wa wananchi wa Saudia kwa serikali hiyo.

Kilichowashangaza wachunguzi wa habari hivi karibuni ni kuwa licha ya Marekani kuwa dola ya kidemokrasia na Saudia kuwa utawala wa kifalme wenye kutumia adhabu ya kifo mara kwa mara au operesheni za kuuawa watu nje ya sheria wanaotoa taarifa nyeti za utawala wa kifalme, kuna ukaribu wa kushangaza na Rais Trump.

Hivi karibuni gazeti maarufu la New York Times liliandika taarifa ya kina iliyothibitishwa na baadhi ya maofisa wa mashirika ya ujasusi ya Marekani ikiwamo CIA kuwa nchi hiyo imekuwa ikifanya mashambulizi ya kuweka virusi vya mawasiliano kimtandao dhidi ya shirika la ugavi wa umeme nchini Russia.

Walieleza kuwa sababu ni kuwa Russia imekuwa ikitumia silaha za virusi vya kimtandao (cyber warfare) dhidi ya mifumo ya ugavi wa umeme nchini Marekani na maeneo mengine.

Rais Trump ambaye taarifa zinaonyesha kuwa hakupewa taarifa juu ya operesheni hiyo ya kuingiza virusi vya kimtandao alisema taarifa ya gazeti hilo 'haitofautiani na uhaini,' msimamo ambao hautofautiani na ule wa MbS kuhusu Khashoggi kufuatilia kwa karibu Saudia kutumia silaha za kemikali vitani Yemen.

Ina maana kusingekuwa na vielelezo maridhawa vya kidemokrasia, 'uhaini' huo ungelipiwa.

UCHAMBUZI

# Kakunda: Serikali iigawe Sikonge kusogeza huduma kwa wananchi

Na Sabato Kasika

JOSEPH Kakunda ni Mbunge wa Jimbo la Sikonge mkoani Tabora kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), ambaye aliibuka mshindi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, anasema kwamba aliahidi wakati wa kampeni za uchaguzi kuzingatia vipaumbele vya Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015-2020, katika kuwatumikia wananchi wa jimbo hilo.

Ahadi hizo ni pamoja na kuondoa umaskini, kupunguza tatizo la ajira, kuendeleza vita dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya umma, kudumisha amani, ulinzi na usalama wa maisha ya wananchi na mali zao.

"Utekelezaji pia umezingatia mwelekeo alioutoa Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; alipolihutubia Bunge Novemba 20 mwaka 2015 jijini Dodoma na kuzitaja kero mbalimbali ambazo pia zipo Sikonge," anasema.

Anabainisha kero hizo kuwa ni pamoja na mazingira duni ya kujifunzia na kufundishia katika shule nyingi za serikali ikiwamo madarasa, ofisi za walimu, nyumba za walimu, madawati, mabweni, mabwalo, maabara, maktaba na vifaa vya kufundishia.

"Kuna malalamiko ya walimu, hali isiyoridhisha ya barabara, madaraja, huduma za umeme vijijini na huduma za maji mijini na vijijini, mawasiliano duni ya simu hasa vijijini, huduma duni katika vituo vya afya pamoja na kuwa mbali na makazi ya wengi," anasema.



Mbunge wa Jimbo la Sikonge, Joseph Kakunda (kushoto), akitambulishwa na Mwenyekiti wa CCM, Rais John Magufuli. **PICHA: MTANDAO**

### MFUKO WA MAENDELEO JIMBONI

Kakunda anasema katika kipindi cha 2015/2016 hadi 2018/2019, jumla ya Sh. 291,884,000 zilipokelewa kwenye Mfuko wa Jimbo, ambapo kamati ya mfuko huo ilizipangia matumizi fedha hizo kwenye miradi 78 ya wananchi.

Anasema katika sekta ya elimu fedha hizo zilitekeleza jumla ya miradi 61 iliyotumia Sh. 211,455,280.

Miradi hiyo inajumlisha kutengeneza madawati 113; ujenzi wa madarasa mapya 22, ukarabati wa madarasa chakavu 47, ukamilishaji wa matundu ya vyoo 104; ukarabati na ujenzi wa ofisi 19 za walimu na ukamilishaji wa nyumba 13 za walimu.

"Sh. 22,850,000 zilitumika kutekeleza miradi minne kwenye sekta ya afya ikiwamo ukamilishaji wa choo katika zahanati ya Kikungu, kuchangia ujenzi wa zahanati za Kidete, Mwamayunga na Ibaya; na ununuzi wa vyandarua 134 katika Hospitali teule ya Wilaya ya Sikonge," anasema.

### KILIMO

Kwa upande wa uzalishaji wa chakula; mahindi, mpunga, maharage na mazao mengine, ambayo hutegemewa kwa chakula, anasema kuna mafanikio makubwa anayojivunia, hasa kuongezeka kwa uzalishaji kutoka tani 164,658 mwaka 2015 hadi 166,543 mwaka jana.

Mbunge anasema, kwa sasa Sikonge imeanza taratibu za kuanzisha mazao mapya kama korosho, alizeti na muhogo ili kuboresha maisha ya wakulima.

### KUPAMBANA NA UMASKINI

Anasema tumbaku ni zao kuu la biashara linalotegemewa kwa kipato.

Anabainisha kwamba kutokana na changamoto za pembejeo na mikataba ya mikopo, ambayo wakulima kupitia vyama vyao vya ushirika vya msingi hukubaliana na benki; bado yapo malalamiko mengi ya wakulima wa tumbaku dhidi ya makisio na hata bei ya tumbaku; ambayo huamuliwa kabla ya mkulima hajalima.

"Serikali inaandaa utaratibu wa kushughulikia changamoto hizo ikiwamo kupata wanunuzi wapya na mbegu mpya...mpango mwingine ni kupata masoko mapya ya tumbaku katika nchi za China na Misri ili kuongeza ushindani," anasema.

Anasema kwa upande wa uzalishaji wa chakula; mahindi, mpunga, maharage na mazao mengine, ambayo hutegemewa kwa chakula, kuna mafanikio makubwa anayojivunia kwa vile uzalishaji umeongezeka kutoka tani 164,658 mwaka 2015 hadi tani 166,543 mwaka 2018.

### MIUNDOMBINU

Kakunda anasema ujenzi wa barabara ya Tabora- Ipole- Mpanda yenye urefu wa kilometa 359 inayogharimu zaidi ya Sh. bilioni 700 ulianza 2015/2016, na kwamba hadi sasa kipande cha kilometa 30 kutoka Tabora- Pangale kimekamilika.

"Ujenzi wa kuanzia Pangale hadi Mpanda ulioanza Mei, 2018 unaendelea, ambapo uwekaji wa tabaka la lami umeanza katika baadhi ya maeneo... matarajio ni kukamilika ifikapo mwaka 2021," anasema.

> "Serikali inaandaa utaratibu wa kushughulikia changamoto hizo ikiwamo kupata wanunuzi wapya na mbegu mpya... mpango mwingine ni kupata masoko mapya ya tumbaku katika nchi za China na Misri ili kuongeza ushindani," anasema.

### MAWASILIANO

Kwa upande wa mawasiliano, anasema mwaka 2015 hakukuwa na mawasiliano ya simu kwenye Tarafa ya Kitunda; lakini sasa minara imesimikwa ya Vodacom (Kipili na Kitunda) TTCL, (Kipili), na Halotel (Kitunda na Kilumbi).

Anasema minara hiyo imewezesha kuwapo mawasiliano ya simu kwenye tarafa hiyo na kwamba ofisi ya mbunge inaendelea kufuatilia ili mamlaka zinazosimamia sekta ya mawasiliano ziongeze nguvu ya minara ihudumie eneo kubwa zaidi.

Kakunda anasema hatua hiyo itahusisha kuifungua baadhi ya minara, ambayo haijafunguliwa ikiwamo ya Airtel (Kipili) na Halotel (Kilumbi) na kufuatilia ujenzi wa minara mipya Nyahua, Igigwa, Kiloli, Ngonywa na Ipole, ambayo wizara imeahidi kutekeleza.

### UMEME NA VIWANDA

Mbunge huyu anabainisha kwamba hadi sasa vijiji 35 vimeunganishiwa umeme wa REA (awamu ya I, II na III); mpango unaoendelea kupitia REA III ambapo utaunganisha umeme vijiji na vitongoji vyote ifikapo Juni 2021.

Aidha, anataja orodha ya viwanda vidogo vilivyoko katika Jimbo la Sikonge kuwa ni pamoja na mashine za kukoboa na kusaga nafaka hadi viwanda vya kukamua mazao ya kula na kwamba vimeongezeka kutoka 267 mwaka 2015 hadi 291 mwaka 2018.

### ELIMU NA AFYA

Anasema pamoja na kuwa kuna idadi ya shule za msingi 95 zilizosajiliwa, idadi ya madarasa imeongezeka kutoka 478 mwaka 2015 hadi kufikia 559 kwa mwaka 2018.

"Nyumba za walimu zimeongezeka kutoka 192 mwaka 2015 hadi kufikia 214 mwaka 2018, na shule za sekondari za serikali zimebaki 17 zilizosajiliwa, lakini ujenzi wa sekondari mpya Kilumbi na Mpombwe uko katika hatua za mwisho na ujenzi wa Sekondari Nyahua pia umeanza," anasema.

Kuhusu afya, anasema ofisi yake iliwezesha kupatikana kwa jumla ya Sh. 2,300,000,000 ambazo zimegawanywa katika maeneo mbalimbali ili kuboresha huduma za afya jimboni ikiwamo Kituo cha Afya cha Kitunda kilichopatiwa Sh. milioni 300.

Kituo hicho kilipatiwa fedha hizo kukiwezesha kutoa huduma za rufani kwa wagonjwa wa eneo lote la tarafa ya Kitunda na mikoa ya jirani na pia Sh. milioni 500 zilipelekwa Kipili kujenga kituo kipya cha afya.

### OMBI KWA SERIKALI

Kakunda anaiomba serikali kuigawa Sikonge ili iwe wilaya mbili, kwa madai kwamba ni kubwa kuliko wilaya nyingi za hapa nchini.

Anabainisha kuwa hilo likifanyika litasogeza maendeleo karibu zaidi na wananchi.

# Trump afuta mashambulizi dhidi ya Iran dakika 10 kabla hayajaanza

**Na Anil Kija**

ALHAMISI ya wiki iliyopita, Marekani iliafiki halafu ikafuta kufanyika mashambulizi dhidi ya maeneo kadhaa muhimu kijeshi nchini Iran, ambako taarifa zilizotolewa na maofisa wa jeshi kwa gazeti mashuhuri la New York Times zilisema yangelenga vinu vya kurushia makombora na mifumo ya radar.

Hatua hii ilikuwa ichukuliwe baada ya vikosi vya kimapinduzi vya Iran kuangusha kwa kombora ndege ya upelelezi ya Marekani isiyo na rubani (droni) baharini.

Marekani na Iran ziliendelea kuvutana kama ndege hiyo ilikuwa juu ya bahari ya kimataifa au ilikwaruza eneo la bahari la Iran kama jeshi la Iran lilivyodai, na Wizara ya Nje ikasema itafikisha suala hilo Umoja wa Mataifa (UN).

Ndege hiyo iliyopewa jina la kimedani la RQ-4 Global Hawk (tai wa kimataifa) ilikuwa inafanya upelelezi au doria, na Iran ikapata nafasi ya kuonyesha msimamo mkali kuhusu uwepo wa meli za kivita za Marekani karibu na mpaka wake baharini, ndani ya mfumo mzima wa vikwazo vinavyoiumiza nchi hiyo.

Kuangushwa kwa ndege hiyo zaidi kidogo ya wiki moja baada ya kulipuliwa meli kubwa ya mafuta kulionekana kuifikisha Marekani ukingo wa uvumilivu, hasa miongoni mwa wasaidizi wa Rais Donald Trump na maseneta wa chama cha Republican.

Spika wa Baraza la Wawakilishi, m-Democrat, Nancy Pelosi, alisisitiza hiyo Alhamisi kuwa wananchi wa Marekani hawana hamu ya vita kabisa na Iran, huku Seneta Lindsay Graham wa Republican akisema uchokozi, ubabe wa Iran umetosha, hivyo 'kama wana uchu wa kupigana, watapata vita'

Kabla ya kulielekeza Jeshi la Marekani kufanya mashambulizi hayo, Rais Trump aliandika katika ukurasa wake wa twitter kuwa hatua ya Iran ya kuiangusha ndege yake ya upelelezi baharini ilikuwa ni 'kosa kubwa,' kwa maana ya kutoelewa wanachokifanya.

Baada ya kutoa agizo la kufuta mashambulizi hayo, Trump alitoa maelezo kuwa mashambulizi yasingelingana na tukio husika, akisema kuwa jenerali mmoja alimweleza kuwa watu wanaofikia 150 wangeweza kufa katika mashambulizi yaliyopangwa au kuelekezwa kufanyika kupiga mifumo ya radar, n.k.

Baadhi ya wachunguzi wa habari walijiuliza kwanini suala la idadi ya watu wanaoweza kufa katika shambulio la kijeshi ipatikane dakika za mwisho baada ya mashambulizi kuruhusiwa kufanyika, wakati vielelezo kama hivyo ni sehemu mahsusi ya kubuni mashambulio, n.k.

Hata hivyo, Rais Trump alionekana kujali sana kuwa Iran ni taifa lililo taabani, limedhoofika sana baada ya Marekani kujitoa katika mkataba unaodhibiti mipango ya Iran katika urutubishaji madini ya urani kwa ajili ya nishati na



Kiongozi wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei. **PICHA: MTANDAO**

> Wakati Iran inatoa angalizo la kuanza kuongeza kiwango cha urutubishaji ndani ya wiki mbili, Rais Trump anaapa katika ukurasa wa twitter kuwa Iran haitakaa iwe na silaha za nyuklia. Ina maana kuwa ikianza tu, wanajiandaa kupiga vinu.

hata silaha, uliotiwa saini kati ya Iran na mataifa kadhaa makubwa wakati wa Rais Barack Obama, 2015.

Kujiondoa kwa Marekani na kurudishia vikwazo kumeudhoofisha uchumi wa Iran na Trump alisema Alhamisi kuwa kuna vikwazo vingine vipya.

Akiandika kama kawaida yake kwa herufi zilizojaa alama za mshangao, Rais Trump alichekelea: "Vikwazo vinauma na vingine vimeongezwa jana usiku.

Iran kamwe haitakuwa na silaha za nyuklia, siyo dhidi ya Amerika, na siyo dhidi ya dunia!'

Baadhi ya wachunguzi wa habari walisema Rais Trump aliona aendelee kutumainia kuwa vikwazo vya kuzuia Iran kupata fedha katika mitandao ya fedha duniani vitaifikisha ukingoni.

Baadhi ya watu nchini Marekani wanaamini kuwa uchumi wa Iran ukiendelea kuporomoka kutokana na vikwazo, utawala uliopo utaanguka.

Hara hivyo, yako maeneo mengine ya matukio kutokana na mpangilio wa sera nchini Iran hivi sasa unaoweza kufikisha Ikulu ya Marekani kupuuzia hata kama kutakuwa na vifo vya watu zaidi ya 150.

Ni tangazo la Iran kabla ya ndege hiyo ya upelelezi kuangushwa, kuwa inatoa siku 10 kwa wawakilishi wa nchi kadhaa za Umoja wa Ulaya (EU) kuja na mapendekezo ya kurudisha hali ya mkataba wa kudhibiti uendelezaji miradi ya nyuklia ilivyokuwa.

Dhana ni Ulaya kutumia ushawishi ilio nao kwa Marekani kuondoa vikwazo ili Iran iendelee kufuata mahitaji ya mkataba huo, vinginevyo Iran itapunguza uwajibikaji wake, ianze kuongeza wigo la urutubishaji urani.

Nchi za Ulaya zimekataa angalizo hilo la Iran kuzihitaji kutatua suala gumu la kidiplomasia kwa muda wa siku 10, kwani nchi za Ulaya zinataka Iran ibaki katika mkataba huo hata kama Marekani imejitoa na hata kama kuna vikwazo.

Ni kama vile ni mkataba kati ya Ulaya na Iran pamoja na washirika wengine, hasa wajumbe wengine wa kudumu wa Baraza la Usalama UN, yaani Russia na China, jambo ambalo halileti maana kwa Iran, kudumisha mkataba na Ulaya wakati Marekani imejitoa na kuweka vikwazo.

Wakati Iran inatoa angalizo la kuanza kuongeza kiwango cha urutubishaji ndani ya wiki mbili, Rais Trump anaapa katika ukurasa wa twitter kuwa Iran haitakaa iwe na silaha za nyuklia. Ina maana kuwa ikianza tu, wanajiandaa kupiga vinu.

Isitoshe, Iran bado ina shauku ya kudhibiti na kuzuia kwa kiasi inachoweza nchi nyingine za Ghuba, ambazo kwa sehemu kubwa ni wakinzani wake zikiwamo Saudia na Falme za Kiarabu (Emirates) wanaouza mafuta nje kupitia ukanda bahari inaodai kudhibiti, na huku Iran haiwezi kupeleka mafuta nje kuuza.

Inafanya hivyo kwa tabu kwa nchi ambazo zina uwezo wa kukataa kutii vikwazo vya Marekani, kwani ikiweka vikwazo mahali, kila kampuni inayotaka kufanya biashara na kampuni zilizosajiliwa Marekani lazima itekeleze vikwazo hivyo, vinginevyo itaondolewa ruhusa ya kisheria ya kufanya biashara nchini Marekani, ihamie Iran au kwingine.

Kulikuwa na taarifa za kilichojiri katika uwasilishaji wa hali ilivyo katika chumba kikubwa cha mikakati ya operesheni za vita Ikulu kiitwacho 'Situation Room' wakati wa kufanya maamuzi ya kuipiga Iran kwa shambulio dhidi ya droni.

Katika maandalizi hayo, Waziri wa Mambo ya Nje, Mike Pompeo, anasemekana alitoa maelezo kuwa vikwazo vimeathiri sana uchumi wa Iran kwa kufyeka mapato yake kwa mauzo ya mafuta, kwa mujibu wa ofisa mwandamizi aliyekuwapo karibu na mandhari hiyo.

Pompeo alikuwa akipendekeza kupigwa kwa vielelezo vichache vya mifumo ya kijeshi ya Iran kuhusiana na kuangusha ndege, ila alisisitiza vikwazo vimeleta tija.

Wachunguzi wa habari walisema baadaye kuwa alichoeleza Pompeo katika majadiliano hayo hatimaye kuliwezesha Trump kubadili uamuzi wake wa kufanya mashambulizi, kuwa licha ya kuwa vifo vya watu 150 kulipia ndege isiyokuwa na rubani ni gharama kubwa mno, pia haikuwa na sababu.

Ni kama Trump alivyopuuza majaribio ya hivi karibuni ya Korea Kaskazini kurusha makombora ya masafa mafupi, kama ni mateke ya mfamaji kwani makombora hayo si tishio kwa Marekani, na kwa hali yoyote ile nchi hiyo haiwezi kushambulia jirani zake.

Trump alisema katika yale aliyoandika kwenye ukurasa wa twitter baada ya kufuta amri ya kufanya mashambulizi kuwa 'hana haraka' ya kujibu mashambulizi ya Iran (meli ya mafuta, droni).

Ni kama anangoja Iran walete mezani sababu inayotosha kwa shambulio la kina, tena kubwa, kwa mfano kuongeza kiasi cha kusumbua dunia kwa urutubishaji urani, kushambulia tena meli kubwa za mafuta, au kutungua tena droni (labda moja au mbili zaidi katika anga ya kimataifa baharini).

Ni presha kwa utawala wa Iran; ujipalie vita au utulizane na vikwazo.





# Wakulima tumbaku wakumbwa na taharuki

**Na Nebart Msokwa, CHUNYA**

ZAIDI ya wakulima 5,800 wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wako hatarini kukosa soko la zao hilo katika msimu wa kilimo wa 2019/20 baada ya moja ya kampuni zinazonunua kutangaza kujitoa.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Ramadhani Shumbi, alisema hayo juzi wakati wa Kikao cha Baraza la Madiwani huku akiitaja kampuni iliyotangaza kujitoa kuwa ni Tanzania Leaf Tobacco Company (TLTC) Alisema kampuni hiyo ni miongoni mwa kampuni kubwa zinazonunua zao hilo na kwamba kitendo cha kujitoa kinawakatisha tamaa wakulima na kuna hatari kubwa ya zao hilo kukosa soko na kusababisha hasara kubwa.

Kutokana na hali hiyo, aliiomba serikali kuwatafuta wanunuzi wengine watakaoziba pengo la TLTC kabla msimu wa mpya wa kilimo haujafika ili kuwaepusha wakulima kupata hasara.

"Hapa kwetu tuna kampuni mbili pekee zinazonunua zao hili na sasa hivi tumeambiwa TLTC wanajitoa. Tunaomba serikali iwahakikishie wakulima wetu soko kabla msimu haujafika ili wasije wakazalisha na wakakosa soko," alisema Shumbi.

Ofisa Ushirika wa Wilaya ya Chunya, Mwaji Magomba, alikiri kuwapo kwa taarifa za kampuni hiyo kutaka kujitoa na kwamba serikali imeshaanza kuchukua hatua za kushughulikia tatizo hilo.

Alisema kwa sasa hata yeye hajui sababu ya kampuni hiyo kutaka kujitoa lakini akawahakikishia wananchi wa wilaya hiyo kuwa zao hilo bado litakuwa na soko la uhakika mwakani hata kama TLTC itajitoa. "Baraza Kuu la Tumbaku nchini lilikuwa na kikao Morogoro hivi karibuni na liliuagiza uongozi wa TLTC kuandika barua rasmi ya kujitoa ili hatua za kutafuta wanunuzi wengine kuziba pengo na hatua zingine na mpaka sasa bado barua hiyo haijawasilishwa," alisema Magomba.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Bosco Mwanginde, aliwataka madiwani na watendaji wa halmashauri kuanza kuwahimiza wananchi kulima mazao mbadala ya tumbaku ili kuepuka kuingia hasara.

Alisema wakulima kwa sasa wanatakiwa wazalishe zaidi alizeti na ufuta, mazao ambayo alisema yana soko la uhakika na kwamba hata yakikosa soko yanaweza yakatumika kama viungo kwenye mboga na yakaliwa tofauti na tumbaku.

Alisema tumbaku kwa sasa soko lake si la uhakika, hivyo lazima wakulima waanze kubadili fikira zao na kuanza kuzalisha mazao yenye uhakika wa soko ndani ya nchi na nje.

"Tumbaku ikikosa soko tafsiri yake ni kwamba mkulima anakuwa ameingia hasara na haiwezi kuliwa, hivyo lazima wakulima wabadilike na waanze kuzalisha mazao mbadala na ni muhimu pia wakulima wakahimizwa kulima korosho ambayo imethibitika kuwa inastawi vizuri," alisema Mwanginde.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Meneja wa Kanda ya Mashariki, Aikansia Muro, pamoja na meneja wengine baada ya kuhudhuria vikao vya Bunge. Benki ya NMB iliwapeleka mameneja wa kanda zote nchini kuhudhuria vikao ya Bunge jijini dodoma hivi karibuni. **PICHA; MPIGAPICHA WETU**

# Mamilioni waugua kwa kula vyakula vichafu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAKRIBANI watu milioni 600 duniani wanaugua maradhi yatokanayo na kula vyakula visivyokuwa salama kila mwaka vikiwamo vyenye sumu, imeelezwa.

Hayo yalisemwa jijini hapa na Meneja wa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Rodney Alananga, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu shughuli zinazofanywa na mamlaka hiyo. Alisema kati ya idadi hiyo, watu 420,000 wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na kula vyakula visivyokuwa salama barani Afrika ambako ndiko kwenye tatizo zaidi.

Alananga alisema asilimia 70 ya Watanzania wanaokula chakula kwa mama lishe na baba lishe, ambako vyakula vingi haviandaliwi kwa usalama na ubora unaotakiwa kwa ajili ya afya za watumiaji.

Meneja huyo aliwatahadharisha wananchi kuwa makini sehemu wanazokula chakula ikiwa ni pamoja na kuangalia mazingira ya uandaaji, usafi na kuzingatia kunawa mikono kabla ya kula.

Aidha, aliwataka wananchi kutoa ripoti TFDA au kwa maofisa afya wa kata na halmashauri, ikiwa watapata madhara ya tumbo kutokana na kula chakula ambacho wanahisi si salama.

"Kwa Afrika tu watoto 120,000 wanafariki dunia kila mwaka kutokana na kula chakula ambacho si salama, hivyo wafanyabiashara wa vyakula watangulize mbele utu badala ya pesa kwa kuhakikisha wanaandaa vyakula vyao kwa usafi na kuangalia vyakula hivyo vinatoka wapi," alisema. Naye mmoja wa wadau wa afya, Samwel Ndoni, mbali na kuishukuru TFDA kutoa elimu, alisema vyombo vya habari ni wadau muhimu katika kufikisha ujumbe na kutoa elimu kwa umma kuhusiana na udhibiti wa bidhaa zilizopigwa marufuku.

Alisema kupitia elimu waliyoipata watakuwa mstari wa mbele kuhamasisha wananchi kuzingatia usalama wa chakula na kuandaa maudhui yatakayosaidia kupiga vita kuingiza na kutumia bidhaa zilizozuiliwa na mamlaka hiyo.

"Tunaweza kufanikisha hayo ikiwa vyombo vya habari havitaachwa nyuma kwenye mikakati yenu dhidi ya mapambano ya kudhibiti vipodozi, vifaa tiba, chakula, vitendanishi na dawa. Tunawaomba mtoe kipaumbele kwa vyombo vya habari vinaaminika na jamii," alisema Ndoni.

## Wahamasishwa kusajili simu zao

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wametakiwa kujitokeza kusajili kadi za simu kwa kutumia alama za vidole kupitia kampuni ya simu na mawakala ili wakamilishe kazi hiyo kwa muda uliopangwa na serikali.

Wito huo ulitolewa jijini Mbeya na Mhandisi Mwandamizi wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Charles Thomas, wakati akizungumza na gazeti hili kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma.

TCRA iliadhimisha Wiki ya Utumishi wa Umma kwa kufanya usajili wa kadi za simu kwa kutumia alama za vidole katika eneo la Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia (Must) na stendi ya Kabwe.


Mhandisi Thomas alisema TCRA imetumia maeneo hayo kama sehemu ya kutoa hamasa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kusajili simu kazi inayoendelea nchi nzima.

Alisema kazi hiyo imewahusisha watoa huduma kutoka kampuni zote ya simu za mkononi, Jeshi la Polisi, Uhamiaji, Mamlaka ya Vitambulisho (Nida), ofisa mtendaji wa kata, na kwamba kwa kutumia mfumo wananchi wanapata huduma zote za usajili sehemu moja.

"Tusiposajili laini zetu kwa muda ulipangwa tunaweza kujikuta hata salamu za mwaka mpya tutakazotumiwa na ndugu zetu tusizipate kwa sababu tutafungiwa laini Desemba 31 kama tutakuwa hatujazisajili kwa kutumia alama za vidole," alisema Thomas.

Mhandisi Thomas alisema TCRA, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa kutumia vyombo vya habari, mikutano na mikusanyiko ya watu kuhusu umuhimu wa kusajili kadi za simu kwa njia ya alama za vidole.

Baadhi ya wananchi waliozungumza na gazeti hili walisema kazi hiyo imewasaidia kutumia muda mfupi kwa kuwa wahusika wote wa mchakato wa usajili walikuwa wanapatikana sehemu moja.





# Waanzisha klabu ya wanafunzi kurejesha uzalendo

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

JUKWAA la Walimu Wazalendo nchini limeanzisha klabu za wanafunzi shuleni kwa ajili ya kurejesha uzalendo kwa Taifa ambao ulikuwa umeanza kuporomoka.

Akizungumza jana wakati wa jukwaa hilo likifanya usafi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Mlezi wa Jukwaa hilo, Wilaya ya Kinondoni, Mkomanile Mahundi, alisema miongoni mwa madhumuni ya kuanzishwa kwa jukwaa hilo ni kuisemea na kuisaidia serikali.

"Pia ilikuwa ni kuanzisha klabu za kizalendo shuleni kwa sababu tuliona kuwa maadili yanateketea watoto hawaishi kama vile walivyoishi wazazi wetu, tukaona tuwaeleze watoto wapi wanatoka na wapi wanastahili kwenda," alisema.

Alisema pia kuwawezesha watoto kujua mambo muhimu ambayo serikali ya awamu ya tano inaendelea kuyafanya nchini ikiwamo utaratibu wa elimu bila malipo.

Akizungumzia mjadala unaoendelea nchini baada ya mapendekezo ya serikali kurejesha kodi kwenye taulo za kike, Katibu wa jukwaa hilo, Misago Athumani, alisema uamuzi wa serikali kurejesha kodi katika taulo za kike ni uamuzi sahihi.

Alisema baada ya serikali kuondoa kodi kwa taulo hizo bei ilibakia kuwa ileile hivyo kutowanufaisha wanafunzi wa kike kama ilivyokuwa imelengwa na serikali.

"Bora iendelee kutozwa kodi kwa sababu hata wale wanaouza hawaoni huruma ama umuhimu wa kuwasaidia hawa watoto wa kike ingawa lengo la serikali lilikuwa ni hilo," alisema Athumani.

Kwa muda sasa mjadala wa kurejeshwa kwa kodi umekuwa ukiendelea katika mitandao ya jamii na bungeni mara baada ya kusomwa kwa bajeti ya serikali iliyopendekeza kurejeshwa kwa kodi hiyo.

# Osha yawajengea uwezo wanafunzi Udom

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Usalama Mahala Pa kazi nchini (Osha), umetoa mafunzo kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom), wanaosoma shahada ya mazingira na udhibiti wa mjanga, ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na majanga kwa vitendo pindi watakapoingia katika soko la ajira.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika chuo hicho, Mkaguzi wa Mazingira na Ekonomi kutoka Osha, Venance Buliga, alisema mafunzo hayo yatasaidia kuwajenga wanafunzi hao.

Alisema mafunzo hayo yanahusu masuala ya usalama na afya mahala pa kazi. "Hawa ni wanafunzi ambao wanasoma shahada za masuala ya maafa katika kazi zao mambo wanayokutana nayo ni usalama mahala pa kazi wakimaliza hapa watakwenda mtaani hivyo ni vyema sasa wakapata mafunzo haya kivitendo ili wakienda huko waweze kukabiliana na changamoto zilizopo," alisema.

Alisema kutokana na sera ya uchumi wa viwanda lazima kuwaanda vijana wengi wenye utaalamu wa masuala ya majanga na maafa ili kuwa na mazingira salama kwa wananchi.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwapatia maarifa wanafunzi hao ili waondoke chuoni hapo wakiwa wameiva badala ya kuondoka na cheti pekee bila kuwa na ujuzi. Mmoja wa wanafunzi hao, Pascal Cheka, alisema mafunzo hayo yamekuja wakati mwafaka kwa kuwa yatawasaidia kuongeza ujuzi kutokana na wakati mwingi kujifunza kwa njia ya nadharia badala ya vitendo.

Cheka alisema mara nyingi wamekuwa wakisoma darasani bila kufanya mafunzo kwa vitendo hali ambayo inaweza kuchangia kuondoka na vyeti lakini wakawa hawana ujuzi wa kutosha.

Cheka alisema wanaiomba serikali kuwekeza jitihada za kutosha katika kuboresha vitendea kazi kwa ajili ya kusaidia wakati yanapotolea majanga.

"Serikali iwekeze kwa kuwaandaa wataalamu wa majanga pamoja na vifaa vya uokoaji katika maeneo mbalimbali ili kuondokana na matukio ya vifo vya watu katika majanga mbalimbali nchini," alisema.

Mhadhiri wa chuo hicho, Idara ya Jiografia na Mafunzo ya Mazingira, Japheth Rongo, alisema pamoja na chuo hicho kutayarisha wataalamu katika masuala ya maafa na majanga bado serikali haijawapa kipaumbele.

"Wataalamu wengi tunawatengeneza hapa toka mwaka 2011 tumekuwa tukitoa wataalamu wa majanga, lakini bado serikali haijawaweka katika mfumo wa ajira rasmi serikalini zaidi wamekuwa wakiajiriwa na kampuni kama uchimbaji wa madini," alisema Ringo. Alisema ni wakati sasa Ofisi ya Waziri Mkuu inayohusika na maafa kuwatumia vijana hao na kuwawekea mfumo rasmi kwa ajili ya kuwawezesha kutoa msaada katika maeneo mbalimbali ambayo yamekuwa yakikumbwa na maafa ya mafuriko na tetemeko.




Katibu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, akimsikiliza Meneja wa Tawi la Dodoma, Dickson Raymond, toka Kampuni ya Poly Machinery Co.Ltd akiwa anakagua moja kati ya vifaa vinavyouzwa na kampuni hiyo. **PICHA: PAUL MABEJ**

# Serikali kupunguza ukatili kwa 50% 2022

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau mbalimbali nchini, imejipanga kutekeleza mpango wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ambao unalenga kupunguza ukatili huo kwa asilimia 50 ifikapo 2022.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee, Wanawake na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, wakati akizungumza katika siku ya wajane duniani iliofanyika kitaifa jijini Dodoma.

Dk. Ndugulile alisema katika kuhakikisha mpango huo unatekelezwa kamati za ulinzi za wanawake na watoto zimeanzishwa katika mikoa na halmashauri zote hapa nchini.

"Kamati hizo zimeanzishwa kwa asilimia 50 ya kata zote, hivyo serikali inaamini mpango wa kutokomeza ukatili utafanikiwa," alisema Dk. Ndugulile.

Alifafanua kuwa serikali imeanzisha dawati la jinsia na watoto kwenye vituo vya polisi 417, katika maeneo mbalimbali na kuitaka jamii kuyatumia madawati yao pale wanapokumbana na matatizo ya ukatili wa kijinsia.

Alisema serikali inawahamasisha wajane na Watanzania wajenge utamaduni wa kutoa taarifa kwa kamati na madawati hayo pale wanapofanyiwa ukatili wa kijinsia, ili kuhakikisha wanaohusika wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za nchi.

Dk. Ndugulile alisema serikali imewezesha kutungwa kwa sheria ya msaada wa kisheria namba 1, ya mwaka 2017 na kutungwa kwa sheria hiyo kunatoa fursa kwa wajane kudai haki zao za msingi katika vyombo vya sheria ikiwamo mahakama kupitia huduma za msaada wa kisheria.

Alisema pamoja na jitihada zote serikali haitaweza kutatua changamoto zote za wajane na makundi mengine endapo hawatambui fursa zinazotolewa ili kujikwamua na kujiendeleza.

Alitoa fursa ya kukutana na mashirika yasiyo ya kiserikali kwa ajili ya kujadili suala zima na kubadilishwa kwa sheria kandamizi kwa wajane ili kuona wanafanyaje kutatua suala hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WILDAF), Neema Makando, alisema wanatamani kuona sheria zinafanyiwa marekebisho ili kuondoa unyanyasaji unaowakabili wanawake wanaofiwa na waume zao.

Naye Mkurugenzi wa Chama cha Wajane Tanzania (TAWIA), Rose Sarwat, alisema serikali inatakiwa kuangalia sheria ya mirathi ya kimila ili wajane wapate haki zao stahiki.





Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, akipokea kadi 32 za pikipiki za tarafa 32 za Mkoa wa Manyara kutoka kwa Mkurugenzi wa nchi wa PharmAccess International, Dk. Heri Marwa, zitakazotumika vijijini kutoa elimu ya mfuko wa bima ya afya ulioboreshwa CHF juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Bil. 10/- zanunua boti za uokozi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imetumia Sh. bilioni 10 kwa ajili ya kununua boti mbili za kisasa za uokozi ambazo zimekabidhiwa kwa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM).

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Shamata Khamis Shaame, alisema hayo jana kwenye Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Konde, Omar Seif Abeid.

Katika swali lake hilo, Abeid alitaka kujua mikakati iliyochukuliwa na serikali katika kukabiliana na matukio ya ajali na uokozi.

Alisema boti mbili hizo ambazo ni za kisasa, zina uwezo mkubwa wa kukabiliana na majanga ikiwamo kuokoa wananchi wakati wanapokumbwa na maafa.

Alisema boti moja ina uwezo wa kuokoa ya watu 600 katika matukio ya ajali, huku nyingine ikiwa na uwezo wa kuokoa watu 400. Alizitaja baadhi ya sifa za boti hizo kuwa haziwezi kuzama katika matukio ya ajali, huku zikiwa na uwezo wa kwenda kasi katika maeneo ya matukio. “Mheshimiwa Naibu Spika, tayari serikali imenunuwa boti mbili kwa ajili ya uokozi wa matukio mbalimbali ya ajali ambazo zimekabidhiwa KMKM,” alisema.

Alisema boti hizo zimenunuliwa baada ya kujitokeza kwa matukio mbalimbali ya ajali na kusababisha vifo vya wananchi.

Naibu Waziri alisema baada ya kununuliwa boti hizo, kazi inayofanywa kwa sasa ni pamoja na kujenga vituo Unguja na Pemba ili kurahisisha huduma za uokozi.

Alisema vituo sita vinatarajiwa kujengwa na hadi sasa vitatu vimejengwa Mkoani, Kibweni na Nungwi.

# Tasaf yaahidi kuendelea kupunguza umaskini kaya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Uongozi ya Taifa ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (Tasaf), Dk. Moses Kusiluka, amesema serikali itaendelea kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia mfuko huo, ili kuwawezesha kujikwamua na umaskini na kuondokana na dhana ya kupokea pesa hizo bila kujiendeleza.

Aliyasema hayo jana katika ukumbi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar katika kikao cha maandalizi ya kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa na Tasaf visiwani Zanzibar.

Kikao hicho kilikuwa cha kwanza tangu kuteuliwa kwa kamati hiyo mpya na kuangalia changamoto zilizopo katika utekelezaji wa miradi hiyo. Katika mkutano huo ambao uliwakutanisha viongozi wa ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na wajumbe wa kamati hiyo mpya, Dk. Kusilika alisema lengo la Tasaf ni kuwasaidia wananchi kujishughulisha na ujasiriamali ambazo zitawaendeleza kuwakomboa kiuchumi na kuondokana na umaskini.

“Tasaf itaendelea kuzisaidia kaya maskini hususan katika kijikita zaidi na ujasiriamali na kujindeleza, kwani wakifanya hivyo itawasadia kujikimu kimaisha ikiwamo hata kusomesha watoto wao vizuri,” alisema.

Dk. Kusiluka na wajumbe walipotembelea mradi wa Kituo cha Afya cha Kianga ambacho kimejengwa kupitia miradi ya Tasaf na kuahidi kuwa serikali itendelea na mpango wa pili wa Tasaf ambao utakuwa endelevu utakaotekelezwa kwa miaka minne. Alisema mpango huo wa pili umeboreshwa kwa kuwataka wananchi wafanye kazi katika uzalishaji mali ambao utawaingizia kipato ambacho kitawapunguzia au kuwaondolea umaskini wanaokabiliana nao.

Dk. Kusiluka aliipongeza Zanzibar kwa kutekeleza vizuri miradi ya Tasaf licha ya changamoto ndogo zilizojitokeza ambazo anaamini miradi inayofuata zitafanyiwa kazi na kufanya vizuri zaidi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mihayo Nhunga, alisema miradi ya Tasaf imewasaidia kwa kiasi kikubwa wananchi walioko katika kaya maskini kutokana na kujikita katika shughuli za uzalishaji.

Alisema kupitia elimu waliyopewa, wananchi wengi walijikita katika shughuli za kilimo cha mboga, ufugaji wa kuku na utengenezaji wa bidhaa za mikono kama vile vikapu na sabuni.

# Mwongozo uchunguzi wa malaria watolewa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya kupitia Kitengo cha Kutokomeza Malaria Zanzibar, imezindua rasmi kitabu cha mwongozo wa uchunguzi na matibabu ya ugonjwa huo utakaotumiwa katika hospitali na vituo vyote afya vya umma na binafsi Unguja na Pemba.

Lengo kuu la mwongozo huo ni kuwa na tiba ya aina moja ya kutibu malaria ikiwa ni juhudi zinazochukuliwa na serikali katika kumaliza kabisa maradhi hayo nchini.

Akizindua mwongozo huo katika ofisi za kitengo hicho jana, Meneja wa Kitengo hicho, Abdalla Suleiman Ali, aliwataka madaktari na watoa huduma za afya wote kufuata mwongozo kwenda sambamba na matakwa ya Shirika la Afya Duniani (WHO).

Meneja huyo alisema hali ya malaria Zanzibar iko chini ya asilimia moja lakini baadhi ya sehemu hasa kisiwa cha Unguja wagonjwa wa maradhi hayo wanaendelea kuripotiwa.

Alizitaja baadhi ya sehemu ambazo kesi za malaria zinaendelea kutokea kwa sasa kuwa ni Shehia za Wilaya Kaskazini Unguja, Micheweni na Wilaya za Magharibi.

Kwa mujibu wa meneja huyo, kazi watakayoifanya katika kukabiliana na vimelea vya malaria ni kumwaga dawa sehemu zinazotuama maji katika maeneo ambayo wagonjwa wa maradhi hayo wanatoka.

Aliwashauri wananchi wanaogundulika na vimelea vya malaria kutoa taarifa sahihi wanapofika hospitali na vituo vya afya ili kufuatilia sehemu wanazotoka na kuondosha kabisa maradhi hayo.

Mkuu wa Sehemu ya Tiba Kitengo cha Kutokomeza Malaria Zanzibar, Shija Joseph Shija, alisema mwongozo huo mpya wa mwaka 2018 unatokana na marekebisho yaliyofanywa kutoka mwongozo wa mwaka 2014 kwa ushirikiano na WHO.

## DataVision yashinda tuzo ya Tehama

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya DataVision International yenye makazi yake jijini Dar es Salaam, imeshinda tuzo ya 'East Africa Brand Leadership 2019' kama Kampuni Bora Zaidi katika utoaji wa huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), utafiti pamoja na utengenezaji wa mifumo ya malipo ya kielektroniki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tuzo hizo zilitolewa Juni 19, 2019 jijini Dar es Salaam na Taasisi ya 'World Marketing Progress'. Washindi walichaguliwa kati ya kampuni 100 zilizokuwa zimependekezwa na watumiaji wa huduma husika kwenye vipengele mbalimbali kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

DataVision International ilitajwa kuwa mshindi katika kipengele cha huduma za ushauri wa kitaalamu. Kwa mujibu wa taasisi hiyo, utoaji wa tuzo hizo ulilenga katika kutambua kampuni, bidhaa, huduma au wafanyabiashara waliofanikiwa zaidi kwa uvumbuzi, ubunifu na ufanisi katika kulihudumia soko husika. Washindi walipatikana kupitia utafiti wa siri uliofanywa na taasisi hiyo uliowahusisha watu waliotumia bidhaa na huduma za kampuni husika katika nchi za Afrika Mashariki.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DataVision International, Geofrey Mwaijonga, alisema kuwa wameipokea tuzo hiyo kama heshima kwao na Taifa kwa ujumla, na kwamba tuzo hiyo ni kielelezo cha jinsi ambavyo kampuni hiyo imefanikiwa kutoa huduma bora zaidi kwa kila mdau wa huduma zake ndani na nje ya nchi.

"Tuzo hii ni kwa ajili ya wateja wetu ambao tunawathamini sana kwani wamekuwa wakituamini na kufanya nasi kazi tangu mwaka 1998, mwaka ambao DataVision International iliasisiwa. Pia, kwa upekee ulio sawa na huo, tunawashukuru wateja na washirika wetu duniani kote na tunapenda kuweleza kuwa tuzo hii ni kwa ajili yao pia," alisema Mwaijonga. "Pia, tunapenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Datavision International, waliopo na wale ambao waliwahi kufanya kazi nasi, tunawashukuru wote kwakuwa tuzo hii ni kielelezo halisi cha kazi yao nzuri waliyoifanya na wanayoendelea kuifanya, kujituma, uadilifu na dhamira yao ya dhati katika kupata mafanikio," aliongeza.

Hivi karibuni, DataVision International ilishiriki katika utoaji wa tuzo za kimataifa za 'Global Learning X-Prize' jijini Los Angeles nchini Marekani.

# Waomba kusaidia taulo za kike wenye ulemavu

**Na Christina Haule,** MOROGORO

SERIKALI na wadau mbalimbali wa masuala ya kijamii wameombwa kutoa msaada wa taulo za kike kwa mabinti walioko kwenye vituo vya kulelea watoto yatima na wenye ulemavu.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mwanzilishi wa Kituo cha Vijana wenye Ulemavu wa Akili (Mehayo), Linda Ngido, wakati akipokea msaada wa vyakula kwa ajili ya watoto wa kituo hicho zikiwamo taulo za watoto wa kike. Vitu hivyo vilitolewa na mjasiriamali Saida Msuya, maarufu kama Mama Halima Fashion, wa mjini Morogoro.

Alisema wamekuwa wakipata taulo za kike kwa ajili ya wenye ulemavu hao kutoka kwa watu mbalimbali na kwamba hawana uhakika wa kupata taulo hizo, jambo ambalo limekuwa changamoto kwao katika kuwahudumia na kulazimika kuwavalisha sketi nyeusi.

"Tuna utaratibu wa kuwakusanya watoto wa kike na kuwafundisha wanapoonekana kufikia umri mkubwa licha ya kuwa kuelewa kwao kunakuwa kuzito. Hata hivyo wako wanaoelewa na inapofikia kutumia taulo za kike hutumia na kama hatuna tunatumia vitambaa vya kawaida huku tukiwavalisha sketi nyeusi," alisema Ngido.

Alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 1995 ili kusaidia watoto wenye ulemavu wa akili wakiwa na umri mkubwa kujifunza shughuli za uzalishaji mali na kwamba walianza na vijana 10.

Katika stadi zao walijifunza kuandaa mambo mbalimbali ikiwamo kuandaa bustani, kufuga na kuchora lengo likiwa watajiajiri. Kwa sasa kituo kina watoto 68, wanawake wakiwa 34 na wanaume 34 wengi wao wakitokea vituo vya kulelea watoto yatima na nyumbani kwao.

Ngido alisema, lengo la kujiajiri watoto hao limeonekana kuwa haliwezekani kutokana na akili zao na kwamba wakaomba eneo lingine kubwa katika Mkundi na kuandaa kwa ajili yao ili kujimudu na maisha yao hata baadaye ikiwamo shughuli hizo walizojifunza kuzifanya wakiwa hapo kama nyumbani kwao.

Pamoja na hayo, aliwaasa wazazi wanapopata watoto wenye ulemavu wa akili kujenga tabia ya kuwasaidia wakiwa na umri mdogo badala ya kuwafungia ndani na wakiwaona hawawezi kufanya chochote hadi wanapofikia wakubwa na kuwapeleka Mehayo, jambo ambalo linamrudisha nyuma maendeleo ya mtoto.

"Wapo watoto wenye ulemavu wa viungo na akili ambao hufika hapa wakiwa hawajui lolote huku wakizidiwa na ulemavu. Kama wazazi wao wangewapeleka kwenye vitengo vya mazoezi mapema wangeweza kupata nafuu japo kidogo," alisema.

Naye Msuya alisema alipata wazo la kutoa msaada kwa wahitaji baada ya kupata tuzo ya mjasiriamali bora mdogo kutoka benki ya Citi na kupata dola 6,000 ambazo ni sawa na Sh. milioni 14 baada ya kushinda tuzo ya ujasiriamali bora na kununua vifaa kwa ajili ya watoto hao.




Mshauri elekezi wa huduma za malipo kwa njia ya kielektroniki wa DataVision International, Maclean Mwaijonga (wa pili kushoto), akipokea tuzo ya 'East Africa Brand Leadership 2019', akiambatana na Meneja Maendeleo ya Biashara wa DataVision International, Bwigane Mulinda (wa pili kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# Mawakala mabasi watakiwa kufichua uhalifu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAWAKALA wa mabasi katika kituo kikuu cha mabasi wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kuwa mstari wa mbele katika kufichua vitendo vya uhalifu na wizi vinavyofanywa na baadhi yao ambao sio waaminifu kwa kuwabia abiria mizigo yao.

Pia wametakiwa kuwafichua watu ambao wamekuwa wakisafirisha dawa za kulevya kwa kushirikiana na mawakala ambao sio waaminifu ili kuudhibiti mtandao huo wakiwamo madereva walevi ambao wanatumia dawa hizo.

Wito huo ulitolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Usalama Barabarani mkoani Shinyanga, Antony Ngwandu, kwenye uchaguzi wa umoja wa mawakala wa mabasi wilayani hapa, na kusema kuwa, baadhi ya mawakala wamekuwa na tabia ya kuibia abiria.

Alisema endapo matukio hayo yataripotiwa kwa wakati katika Jeshi la Polisi malalamiko yanayotolewa na abiria yatapungua hususan kuibiwa mizigo na kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ambayo vinaendelea kuripotiwa.

"Kuweni wazalendo kwa kufichua vitendo vya usafirishaji wa dawa za kulevya, na wale wanaotumia ili tuweza kudhibiti mtandao huo kwani asilimia kubwa dawa zinasafirishwa kwa kutumia vituo vyetu vya mabasi, nanyi mnatambua, lakini mmekaa kimya," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa makala katika kituo kikuu cha mabasi wilayani hapa, Salumu Said, aliyechaguliwa katika uchaguzi huo aliwataka mawakala hao kuwa waaminifu katika kazi zao na kuwakamata watu ambao wanachafua kazi yao kwa kujitambulisha kuwa ni mawakala, huku ni matapeli.

Said alisema atasimamia nidhamu ya mawakala hao ili kudhibiti wimbi la matapeli wanaotumia kivuli cha uwakala kuwaibia abiria.

# Idadi waliofariki kwa ebola DRC yafikia 1,500

**KINSHASA, Congo**

WIZARA ya Afya nchini Congo imesema kuwa zaidi ya watu 1,500 wameripotiwa kufa katika kipindi cha miezi 10 tangu kuripotiwa kwa mlipuko wa ugonjwa wa ebola Mashariki mwa nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC).

Kadhalika imesema vijana waliokuwa na hasira wameripotiwa kuchoma moto vituo vitatu vilivyokuwa vinatoa matibabu ya ugonjwa huo, pamoja na kuharibu magari ya wagonjwa jijini Beni.

Mlipuko wa ebola DRC Mashariki ni wa pili kwa ukubwa katika historia.

Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya watoto duniani (UNICEF), limesema mlipuko huo ni wa 10 kutokea nchini DRC, ni mbaya zaidi kuwahi kushuhudiwa nchini humo.

Imesema mlipuko huo ni wa pili kwa ukubwa kuwahi kushuhudiwa kwenye historia wa kwanza ukiwa ni mlipuko wa ebola huko Afrika Magharibi kati ya mwaka 2014 hadi 2016.

Kumekuwa na ongezeko la matukio ya ebola katika Jimbo la Kivu Kaskazini nchini DRC, hususani kwenye eneo la Katwa ambapo timu za kukabiliana na mlipuko zimekumbwa na ukosefu wa imani kutoka kwa wanajamii.

Msemaji wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Stephane Dujarric alisema mlipuko wa ebola umesamba hadi maeneo ya Kayina ambako hali ya usalama ni hatarishi.

Chini ya kampeni iliyozinduliwa Agosti 8, 2018 watu 96,136 wamepatiwa chanjo nchini DRC. Ebola, kwa mara ya kwanza ililipuka mwaka 1976.

Virusi vya ebola vilianza kuenea katika Afrika Magharibi Desemba 2013. Mwaka 2014 hadi 2017 nchini Guinea, Liberia na Sierra Leone, watu elfu 30 waliambukizwa na zaidi ya watu 11,000 wameshafariki.

Wataalamu wa afya wanasema kuna haja ya mataifa yaliyo kwenye hatari ya kukumbwa na ugonjwa wa ebola kuwekeza zaidi kwenye mikakati ya dharura ya kupambana na ugonjwa huo.

Shirika la Afya Duniani (WHO) hata hivyo limesikitishwa kuwa hadi leo fedha zinazotengwa kupambana na ugonjwa huo ni kidogo mno.

*RFI*

# Pompeo, Mfalme wa Saudia wateta

**RIYADH, Saudi Arabia**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo na Mfalme wa Saudi Arabia, Salman, wamekutana mjini Jeddah na kufanya mazungumzo kuhusu mvutano wa kikanda.

Mazungumzo hayo ni sehemu ya shinikizo la kidiplomasia la kuunda muungano wa kidunia dhidi ya Iran.

Mfalme Salman na Pompeo walitathmini uhusiano wa kimkakati na maendeleo ya hivi karibuni ya eneo hilo na yale ya kimataifa.

Kwenye mazungumzo hayo, Pompeo alisema Marekani inatafuta muungano wa kidunia dhidi ya Iran aliyoiita dola kubwa linalofadhili ugaidi.

Mazungumzo yao yalikuwa kuhusu mashambulizi dhidi ya meli za mafuta katika Guba ya Kiarabu.

"Tulikuwa na mkutano wa kufana na Mfalme Salman bin Abdulaziz Al Saud leo kujadili wasiwasi wa kikanda uliopo na umuhimu wa kukuza usalama wa baharini katika eneo la Hormuz," aliandika Pompeo katika mtandao wake wa kijamii wa twitter muda mfupi baada ya mkutano wake na Mfalme Salman.

Pompeo pia alikutana na mwanamfalme aliye na ushawishi Mohammed bin Salman katika bandari ya Magharibi mjini Jeddah kabla ya kuondoka kuelekea Umoja wa Falme za Kiarabu.

Wizara ya Habari ya Saudia ilisema kukutana kwa viongozi hao wawili ni ishara kuwa mataifa hayo mawili yamesimama pamoja kusitisha shughuli za uchokozi za Iran na kudhibiti ugaidi.

Hata hivyo, Iran ilisema vikosi vyake havitajizuia kutungua ndege zaidi za Marekani kutoka katika anga yake. Ziara ya Pompeo imekuja saa chache baada ya waasi wa Houthi kutoka Iran kushambulia Uwanja wa Ndege wa Abha Kusini Magharibi mwa Saudi Arabia kwa kutumia ndege isiokuwa na rubani na kusababisha kifo cha mtu mmoja huku wengine 21 wakijeruhiwa.

**DW**



Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo (kushoto), akiwa katika mazungumzo na Mfalme wa Saudi Arabia, Salman bin Abdulaziz Al Saud. **PICHA: REUTERS**

# Joto kali kuikumba Ujerumani

**BERLIN, Ujerumani**

IDARA ya hali ya hewa nchini Ujerumani imesema hali ya joto kali inayofikia nyuzi joto 38 inatarajia kuikumba nchi hiyo. Imesema hali hiyo inafahamika kama Ulla.

Mtaalamu wa idara hiyo, Sabine Krueger alisema kuwa eneo pekee ambalo halitaathirika na hali hiyo ya joto kali ni la Bahari ya Kaskazini, ambako hali ya hewa itabakia katika nyuzi joto 29.

Alisema hali ya hewa inatarajiwa kuwa katika viwango vya juu kabisa hadi kufikia nyuzi joto 39 katika maeneo kuzunguka mji wa Frankfurt na kwamba inaweza kufikia nyuzi joto 40 katika maeneo mengine.

Hali ya hewa ya joto kali nchini Ujerumani ilikwa kufikia nyuzi joto 40.3 Agosti 7, 2015, katika mji wa Jimbo la Bavaria la Kitzingen. *DW*

# Museveni: Mahakama EAC haina mamlaka kufuta kipengele cha umri wa rais

**KAMPALA, Uganda**

SERIKALI ya Uganda imesema kuwa Mahakama ya Afrika Mashariki iliyoko mjini Arusha nchini Tanzania, haina mamlaka ya kusikiliza kesi kuhusu kipengele cha umri wa rais.

Kesi hiyo ilipelekwa kwenye mahakama hiyo na wanaharakati wakitaka ibatilishe uamuzi wa mahakama ya katiba iliyokubaliana na bunge kuondolewa kwa ukomo wa umri wa mtu kuwania urais mwezi Aprili mwaka huu.

Serikali ya Uganda ilikuwa ikijibu kesi iliyowasilishwa mbele ya majaji wa mahakama hiyo ambao watatoa uamuzi ikiwa wanaweza kusikiliza kesi hiyo au la.

Pendekezo la kuondoa ukomo kwa mgombea urais Uganda lilowasilishwa bungeni limesababisha mvutano mkubwa uliosababisha uvunjifu wa amani ndani ya Bunge.

Hatua ya kuondoa kiwango cha umri wa kuwania urais ilionekana kama juhudi za Rais Museveni kuongeza utawala wake.

Wakosoaji wake wanasema Rais Museveni anataka aongoze taifa hilo hadi kifo kitakapomkuta.

Uchaguzi ujao nchini Uganda utafanyika mwaka 2021 kwa mujibu wa katiba ya nchi hiyo, na umri wa mwisho wa kugombea urais kabla ya Katiba kufanyiwa marekebisho ulikuwa miaka 75.

Rais Museveni atakuwa na umri wa miaka 76 wakati wa uchaguzi huo.

Rais Museveni ambaye kwa sasa ana miaka 75, ametawala Uganda tangu alipochukua madaraka kwa nguvu mwaka 1986.

*RFI*

HABARI KITAIFA

# Wanunuzi wachakachuaji tumbaku, pamba kukiona

Na Mwandishi Wetu, KATAVI

WAKALA wa Vipimo nchini (WMA) umewakumbusha wanunuzi wa tumbaku, ufuta na pamba kutumia vipimo sahihi, vinginevyo watakabiliwa na kifungo cha miaka mitano jela na faini ya Sh. milioni 100.

Hayo yalisemwa jana na Meneja wa WMA Mkoa wa Katavi, Phanueli Matiko, wakati wa kukagua mizani itakayotumika katika msimu wa mazao hayo, ambapo alisema wakala huyo yuko macho kuhakikisha wakulima wa mazao hayo wanapata kipato kulingana na kile walichokizalisha.

Alisema Sheria ya Vipimo Sura Na. 340 na mapitio yake ya mwaka 2002 imeboreshwa na imekuwa kali na endapo mnunuzi atajihusisha na uchezeshaji wa vipimo. Aidha, alisisitiza kuwa endapo mtuhumiwa atakamatwa na kosa kwa mara ya pili na kuendelea na akikutwa na hatia mahakamani, adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. 500,000 na isiyozidi milioni 100 au kifungo kisichozidi miaka mitano (5) au vyote kwa pamoja.

Kadhalika, mtuhumiwa akikamatwa na kukiri kosa lake, papo hapo atatozwa faini kati ya Sh. 100,000 hadi milioni 20 kulingana na makosa aliyotenda.

Matiko alisema sheria hiyo inakwenda mbali zaidi kwani endapo mtuhumiwa atakataa na kufikishwa mahakamani kwa kosa la kwanza atatozwa faini isiyopungua Sh. 300,000 na isiyozidi milioni 50 au kifungo cha miaka miwili au vyote kwa pamoja.

Alisema hadi jana, WMA wamekwishafanya ukaguzi wa vipimo mbalimbali vitakazotumika kununulia mazao, ambapo kwa ufuta pekee jumla ya mizani 31 imehakikiwa katika wilaya za Mlele (11), Tanganyika (12) na Mpanda mizani (8). Katika ununuzi wa tumbaku jumla ya mizani 35 imehakikiwa na kati ya hiyo, 18 imehakikiwa katika Wilaya ya Mlele, 17 Wilaya ya Tanganyika.

"Uhakiki wa mizani ya vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) zitakazotumika kununulia pamba umekwisha kukamilika ambapo jumla ya mizani 91 imehakikiwa na 71 ilikidhi vigezo na ikawekewa stika maalumu ya WMA na kuifungia lakiri (seal).

"Mizani 21 kati ya 91 iliyohakikiwa ilikataliwa na maofisa wetu kutokana na kuwa na hitilafu mbalimbali, hivyo imepelekwa kwa mafundi mizani kufanyiwa marekebisho na kuhakikiwa upya hivyo mizani zitakazokuwa sahihi zitaruhusiwa kuendelea na ununuzi wa pamba katika vituo vya mauzo," alisema Matiko.

Alisema jumla ya AMCOS 12 zimepatiwa mafunzo ya matumizi sahihi ya mizani katika ununuzi wa pamba, huku akiwaasa wakulima kuwa makini wanapokwenda kuuza mazao yao kwa kuhakikisha mizani inasoma sufuri (0) kabla ya kuanza upimaji kwa mizani ya digitali."

Matiko aliwaasa wananchi kutoa taarifa katika ofisi za WMA wanapokutana na changamoto za upimaji kwa kutumia namba ya bure ambayo ni 0800 11 00 97.

## 'Namthamini' ya EATV yazaa matunda

Na Elizabeth Zaya

KAMPENI ya 'Namthamini' inayoendeshwa na kampuni ya EATV kupitia vyombo vyake vya habari vya televisheni na radio, imeanza kuzaa matunda baada ya kuzalisha kampeni nyingine inayofanana na hiyo inayoendeshwa na Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Godwin Gondwe.

Akizungumza kwa njia ya simu katika kipindi cha Dada's kinachorushwa kila siku na EATV, Gondwe alisema na wao kama wilaya wamejifunza na kuamua kuanzisha kampeni yao inayojulikana kama 'kiki shujaa' ambayo inalenga kumsaidia mtoto wa kike.

"Nachukua nafasi hii kuwapongeza EATV kwa jitihada zao wanazozifanya za kugusa shida za wananchi na pia mtoto wa kike ambaye ndiye mwenye nguvu katika jamii zetu, namkubali sana Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, maana mtu yeyote aliyekaa na mtoto wa kike ambaye ndiye mama huwa ana chagizo kubwa katika maendeleo," alisema Gondwe na kuongeza:

"Sisi Handeni tumeguswa sana na kazi kubwa mnayofanya, mimi huku niko kijijini najua umuhimu wa taulo kwa watoto wa kike. EATV mmetu-inspire (hamasisha) sana sisi tumeamua kuanzisha kampeni inayofanana na hiyo na hii imetokea baada ya kuona kwenu, mmekuwa waanzilishi na magwiji, nawapongeza sana kwa kuendelea na kampeni hiyo kila mwaka, napongeza pia kipindi cha Dada`s mnafanya kazi nzuri."

Kampeni hiyo inalenga kuwasaidia watoto wa kike 5,000 walio pembezoni mwa nchi katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Pwani, Mara, Kigoma, Manyara, Tabora, Morogoro na Njombe.

Kampeni hiyo inayoendeshwa na EATV inatarajiwa kuhitimishwa Juni 30 mwaka huu.



Meneja Mikopo Midogo wa Benki ya NBC, Mtenya Cheya, akizungumza na baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Biashara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDBS), wakati wa semina kuhusu ujuzi katika sekta ya benki pamoja na masoko ya fedha na mitaji hapa nchini. Semina hiyo ilifanyika chuoni hapo jijini Dar es Salaam juzi.

# JPM azindua Taifa Gas

INATOKA UK. 4

wenye moyo wa namna hii."

Rais Magufuli alimpongeza Rostam ambaye ndiye Mwenyekiti wa Bodi ya Taifa Gas kuwa uwekezaji alioufanya umezalisha ajira za moja kwa moja 260 na zisizo za moja kwa moja 3,500 na kwamba pamoja na kuuza Tanzania kampuni hiyo inasambaza gesi katika nchini za Uganda, Rwanda, Burundi, DRC na Sudani Kusini.

Uwekezaji huu umekwenda sambamba na ujenzi wa maghala na mitambo ya gesi katika mikoa 20 nchini kwa gharama ya Sh. bilioni 150 na hivyo kuifanya Taifa Gas kuwa kampuni kubwa zaidi ya uwekezaji kwa idadi ya mitambo na kwa ukubwa wa ghala lenye mitambo ya kisasa kuliko yote Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Rais Magufuli aliwahimiza Watanzania na wageni waendelee kuwekeza Tanzania kwa sababu zipo fursa nyingi kwenye sekta ya nishati. "Mbali ya gesi ipo fursa ya kuzalisha umeme wa joto la ardhi, jua, upepo maji na makaa ya mawe zipo sheria na sera zinazoruhusu sekta binafsi kufanya hivyo," alisema.Alisema uwekezaji wa Taifa Gas ni uthibitisho kuwa serikali inaipenda sekta binafsi na ipo tayari kushirikiana nao na kuwahimiza wajiamini waje kuwekeza kwa sababu wanawahitaji.

**PANUENI USAMBAZAJI**

Alitoa wito kwa wasambazaji wa gesi ya mitungi kuendelea kupanua huduma kwa sababu kwa sasa inapatikana mikoa 23 kati ya 31 iliyopo.

"Taifa Gas mmejipanga miaka mitano ijayo kuongeza mitambo kwenye miji na wilaya nawapongeza, mfikishe huduma hadi vijijini hii itasaidia kutunza mazingira kwa sababu Watanzania zaidi ya asilimia 60 wanaishi vijijini na wanatumia kuni na mkaa," alisema.

Pia aliihimiza wizara kupitia shirika lake kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi asilia maeneo mbalimbali nchini.

Kuhusu uagizaji wa pamoja wa gesi, Rais Magufuli aliitaka Wizara ya Nishati na wawekezaji wakae meza moja wakubaliane kwa lengo la pande zote mbili kunufaika.

"Mmetoa pendekezo kuitaka serikali kuanzisha utaratibu wa ununuzi wa pamoja ya gesi kama ilivyo kwa petroli, sina la kuzungumza kwa sababu nimelisikia leo natumaini wizara na wawekezaji mtakaa mkubaliane ili pande zote zinufaike," alisema. "Ninasema hivi kwa sababu sisi tunakimbilia kukusanya na tunajifanya tunaweza kudhibiti, lakini tunaharibu, inawekezeka na mwekezaji anakimbia hii njia kukwepa, kwa sababu serikali hawawezi kwenda kuangalia flow mita kwamba imeingia kiasi gani." Alizitaka pande zote mbili zizungumze ili serikali ipate haki na kwamba haitaki kujiingiza kwenye uwekezaji.

"Serikali isijiingize kwenye uwekezaji wa sekta binafsi kwa sababu ilishindwa kuleta hii gesi, leo wanakimbia haraka haraka kufanya nini badala ya kukusanya mapato, kikubwa lazima tuangalie kazi nzuri inayofanywa kwa kuingizwa gesi katika nchi yetu.

"Ninafahamu siku za nyuma waliwahi kuchukua uamuzi fulani, huku kukiwa na kampuni ya Tipper, sipendi kuona yakiendelea yale yaliyoifanya Tipper ikawa haipo, ambalo lilikuwa ni shirika letu yasije yakatokea kwenu," alisema.

Alisema ndiyo sababu serikali iliamua kuchukua uamuzi wa kufuta kodi na tozo mbalimbali kwenye sekta hiyo.

Naye, Rostam alisema msimamo thabiti wa Rais Magufuli dhidi ya matendo ya ujanja ujanja katika biashara, uwekezaji na ukwepa kodi, ndivyo vimewafanya leo hii baadhi yao ambao kwa miaka mingi waliamua kuwekeza mitaji yao nje ya Tanzania, kupata moyo na kuanza kuirejesha nchini. Rostam alisema Taifa Gas ni moja ya mfano ya uwekezaji na kwamba wameamua kuongeza uwekezaji wa miradi mingine yenye thamani ya Sh. bilioni 500, katika miaka mitatu ijayo.

Alitoa wito kwa wafanyabiashara wa ndani na nje watambue kwamba milango ya uwekezaji ipo wazi, waje kuwekeza kwa kufuata sheria, taratibu na kanuni za nchi. Mkurugenzi Mtendaji wa Taifa Gas, Hamisi Ramadhani, alisema uwekezaji huo wa Kigamboni umefanyika kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2018 na umeongeza uwezo wake kutoka tani 1,650 hadi kufikia 7,650.

Naye, Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alisema juhudi mbalimbali zilizofanywa na sekta ya nishati kuanzia mwaka 2015 hadi sasa sekta ya nishati imeongeza idadi ya Watanzania wanaotumia gesi ya kupikia kutoka milioni moja.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### MCHANGANYIKO


**MASHINE INAUZWA,** Profesional Floor Machine cleaning inauzwa. Model namba: A005, Speed 154/min. Rated Power 1100W mpya kabisa. Ukihitaji Mawasiliano: 0715 942255


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**


### KUPOTEA KWA CHETI



**Erick Benjamen** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0308-0139** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1994 katika shule ya Sekondari Enaboishu. Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **DAR/KIJ/RB/83834/2019**

115293802


### KUPOTEA KWA CHETI



**Hawa Issa** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0496-070** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1990 katika shule ya Sekondari Jitegemee. Yeyote atakaekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: **MS/RB/6012/2019**

115293502

### GARI INAUZWA



Gari inauzwa aina ya
**TOYOTA HILUX 2.4, engine 2L.**
Ukitaka kuiona inapatikana Upanga Mtaa wa Undali nyumba namba 185, iko kwenye hali nzuri, full AC haina shida yoyote.

**Mawasiliano piga simu namba: 0711506758/0652316880 0686 316880**

115292402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA TARAKA NAMBA: 50..2019.**
**Mdai: LISSU SELEMANI SWALEHE**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: SHARIFA ISMAIL**

**Kwa:**
**SHARIFA ISMAIL**
**WA MUSOMA**

**Ombi la mdai; LISSU SELEMANI SWALEHE**
**Madai ya: TARAKA**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 22 mwezi 07 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii **leo tarehe 25 mwezi 06 mwaka 2019**

115294602

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**

**SHAURI LA RUFAA NA 55 OF 2018**

**LAKAIRO INVESTIMENT LIMITED...MWOMBA MAREJEO**

**DHIDI YA**

1. **KIBANZI PAULO**
2. **AUGUSTINE LUPEMBE**
3. **RICHARD DANDU......WAJIBU MAREJEO**

**KWA: KIBANZI PAULO NA WENZAKE WAWILI (2)**
**POPOTE MLIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Mnaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 27/06/2019 saa 3.00 asubuhi kuja kusikiliza marejeo yaliyofunguliwa na mwomba marejeo dhidi yenu. Mnataadharishwa kuwa endapo hamtafika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi. Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 31/05/2019

115294802

## alkhalij enterprises Limited

### JOB OPENING

## SALES EXECUTIVE

**Roles and Responsibilities:**

- Present and sell the Company's products and solutions to new and existing accounts
- Accountable for ensuring timely communication and customer satisfaction at assigned accounts
- Understand each customer's business and technical applications, anticipating their needs for products and solutions
- Establish and strengthen individual relationships within purchase, maintenance, and operations departments at assigned accounts
- Identify and analyze key opportunities and threats as it relates to products, markets, and competitors
- Prepare weekly and monthly reports on customer visits, significant quotations, and overall sales activity
- Achieve the allocated sales target for assigned accounts and new business

**Requirements:**

- A degree from a reputable academic institution
- Minimum 2-3 years' sales experience related to products
- Effective communication skills and an ability to build and sustain strong customer relationships
- English proficiency is a must
- Willing to work in Dar es Salaam, Tanzania and travel to other cities

**To apply, please send your CV to careers@alkhalij.com**

115289902


*KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO*
*Tupigie 0767 223311*


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CYPRIAN LUBUVA MAURUS** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOYA MARKX** yenye namba za usajili T 335 DCM. Chassis namba **GRX1200025621.** Engine NO. **4GR0070135.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **RB/1234/DO/2019.**

115294302

### KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

**LIVETS RESA LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya FEKON yenye namba za usajili **MC 286 BBB.** Yenye Engine Namba 157FMI215F15052 na Chassis Namba **LDAPAJOB1FGB15052** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi Taarifa Polisi.**MUH/RB/2032/2019.**

215294002

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PNR SERVICES LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **ASHOK LEYLAND/DRILLING RIG** yenye namba za usajili **T 430 DQT.** Chassis namba **MB1DTCHDXJRXZ7400.** Engine **NO.JXHZ446152.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **RB/1235/DO/2019.**

115294402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURIN MDAIWA**
**Mahakama ya mwanzo CHAMWINO MJINI**
**Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Madai Nambari. 127/2019**
**Mdai: LISIOUSLIGHT FINANCIAL SERVICE CO. LTD**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: DEOGRATIUS B. MBOGOYO**
**KWA: DEOGRATIUS B. MBOGOYO**
**K.K. AFISA UTUMISHI WIZARA YA MAMBO YA NDANI (UTAWALA)**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**Madai ya FEDHA TSH. 3,437,500/=**

Kwahiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Alhamisi tarehe 04/07/2019 saa 08:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashaidi wako na hati zote zilizohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikidhibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshidwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 25/06/2019

115294702


*Kwa Habari Motomoto*

*usikose Gazeti lako la*

*Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuzi kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BUFFON KUMRITHI CASILAS PORTO

**LISBON, Ureno**

GOLIKIPA wa zamani wa Juventus na timu ya Taifa ya Italia, Gianluigi Buffon, aliyekuwa anaichezea Klabu ya Paris Saint German msimu uliopita, anakaribia kujiunga na FC Porto aliyokuwa anaidakia Iker Casilas.

Buffon anaenda kurithi mikoba ya Casilas ambaye ametangaza kustaafu baada ya kusumbuliwa na ugonjwa wa moyo ambao unadaiwa kushindwa kupokea damu ya kutosha kwa wakati.


Wakala wa Buffon, Silavano Martina alikiri kuwasiliana na watu wa klabu hiyo na mteja wake ameonyesha kuhitaji kucheza zaidi.

"Buffon anataka kucheza kwa mwaka mmoja zaidi na Porto ni miongoni mwa timu ambazo anazipenda, lakini ana watoto wanne hivyo wanahitaji kusafiri ni jambo analoliwazia," anasema.

Anasema mteja wake alicheza na Sergio Conceicao na ni vizuri akiwa kama kocha wake hivi sasa katika timu kubwa ambazo zina historia kubwa Ulaya.

Aliongeza ndani ya siku 10 mbeleni watatoa uamuzi wao juu ya hatima ya kipa huyo mkongwe.




# KOULIBALY

## AMRUDISHA GUARDIOLA KWA MAGUIRE

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imeripotiwa kuwa haipo tayari kulipa pauni milioni 107 kwa ajili ya kunasa huduma ya beki wa kati wa Napoli na Senegal, Kalidou Koulibaly.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England wanahitaji saini ya beki huyo wa kati, lakini shida ipo kwenye bei wanayotaka walipwe Napoli ili kumuachia beki wake Koulibaly, pauni milioni 107 ambayo Man City imesema haipo tayari kulipa.

Koulibaly, ambaye kwa sasa yupo huko kwenye michuano ya Afcon 2019, anasakwa pia na klabu nyingine za Man United na Juventus na umri wake ni miaka 27.

Napoli wala haina presha kwa sababu beki huyo bado ana mkataba wa miaka minne kwenye kikosi chake, hivyo kama kuna timu inataka kumsainisha mkataba itabidi ikubaliane na masharti yake, ikiwamo bei iliyopangwa.

Lakini, Kocha Pep Guardiola ambaye kwa sasa yupo sokoni kusaka beki wa kati wa kuziba pengo la Vincent Kompany hayupo tayari kumsainisha Koulibaly kutokana na bei yake anayouzwa hivyo amehamishia nguvu kwa Harry Maguire wa Leicester City, ambaye timu yake imedaiwa itahitaji kulipwa pauni milioni 65 tu.

# Liverpool kumvuta beki wa Uholanzi

**LIERPOOL, England**

LIVERPOOL ipo katika hatua za mwisho kuinasa saini ya beki anayecheza kwa mkopo katika Klabu ya PEC Zwolle, Sepp van den Berg, kwa mujibu wa ESPN FC.

Klabu yake ya PSV Eindhoven imetoa ruhusa ya kufanya makubaliano kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kusaini mkataba na Bayern Munich na Ajax, lakini beki huyo wa kati ameamua kuichagua klabu hiyo ya Anfield kwa ajili ya kucheza msimu ujao.

Ada yake imeripotiwa kuwa ni pauni milioni 2, wakati mchezaji huyo akiingia kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake.

Mchezaji huyo ameripotiwa kuwa leo Jumatano atafanyiwa vipimo vya afya na kutangazwa rasmi kuwa mchezaji wa Liverpool Kabla ya Ijumaa.



Van den Berg alianza kuicheza timu ya Zwolle kwa msimu wa 2017-18, akicheza mechi saba za Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, kabla ya msimu uliopita kucheza mechi 16.

Mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya Uholanzi chini ya umri wa miaka 19, ataanza kwanza kucheza katika akademi ya Liverpool kabla ya kupandishwa timu ya wakubwa.

# BENITEZ AAGWA NEWCASTLE

**NEWCASTLE, England**

KOCHA Rafa Benitez ataondoka Newcastle United wakati mkataba wake utakapomalizika Juni 30 mwaka huu, klabu hiyo ya Ligi Kuu England imesema.

Benitez mwenye umri wa miaka 59, alitarajiwa kuondoka baada ya kushindwa kukubaliana kusaini mkataba mpya na mmiliki wa Newcastle, Mike Ashley kwa kipindi cha miezi michache iliyopita.

Huku kukiwa na sitofahamu kama Ashley ataiuza klabu hiyo kuelekea msimu wa 2019-20.

“Kwa masikitiko tunatangaza kwamba kocha, Rafael Benitez ataondoka Newcastle United mara tu mkataba wake utakapomalizika Juni 30, 2019,” klabu hiyo ilisema katika taarifa yake.

“Tulifanya juhudi kuhakikisha Rafa anaongeza mkataba wake kwa muda mwafaka, hata hivyo imeshindikana, kwani tumeshindwa kufikia makubaliano na Rafa pamoja na wawakilishi wake.”

Kocha huyo wa zamani wa Liverpool na Real Madrid, Benitez alijiunga na Newcastle Machi mwaka 2016, lakini alishindwa kuwaokoa kutoshuka daraja.

Mhispania huyo alibakia na klabu hiyo kabla ya kupanda tena Ligi Kuu na aliiwezesha kumaliza ligi nafasi ya 10 ilipopanda na msimu uliopita imemaliza nafasi ya 13.

“Tunapenda kumshukuru Rafa na nafasi yake ya ukocha kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita na mchango mkubwa alioutoa kwa klabu,” taarifa ya klabu hiyo iliongeza.






# MAN UNITED

## YAKATAA POGBA KUBADILISHANA NA NEYMAR

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imesema kwamba imekataa ofa ya PSG ya kumbadilisha Paul Pogba kwa Neymar.

Wachezaji wote wawili wanataka kuondoka kwenye klabu zao, huku Barcelona ikitajwa kumwania Neymar na Real Madrid na Juventus zikipigana vikumbo kuwania saini ya Pogba.

Huku PSG ikiona kwamba haiwezi kumbakisha Neymar, Gazeti la The Independent limeripoti kwamba PSG imejaribu kuishawishi United kubadilishana Neymar na Pogba.

Pogba mwenyewe ameshaweka wazi kwamba, anataka kuondoka hapo United kwa ajili ya kutafuta changamoto mpya baada ya kutua hapo kwa ada iliyoweka rekodi akitokea Juventus.

Baada ya kuwa na msimu mbaya uliopita, Pogba anaona kwamba, ni wakati muafaka kwake kuondoka klabuni hapo.

Neymar ambaye ni mchezaji ghali zaidi duniani, alitua PSG mwaka 2017, lakini sasa amebainisha wazi kuwa anataka kurudi katika klabu yake ya zamani ya Barcelona.

PSG wenyewe wameshabainisha wazi kwamba, Neymar hataki kuendelea kuichezea klabu hiyo msimu ujao na kwamba watamruhusu kuondoka.

Neymar anatajwa kuwa na urafiki wa karibu na Lionel Messi na Luis Suarez na hivyo amekuwa akimshawishi kurudi tena klabuni hapo.

# Uwanja wa San Siro sasa kujengwa upya

**MILAN, Italia**

AC Milan na Inter Milan zinapanga kubomoa uwanja wao wa San Siro na kuujenga upya katika eneo hilo, kwa mujibu wa rais wa Rossoneri, Paolo Scaroni (pichani).

Klabu hizo mbili zimeungana kwenye mradi huo na kwa mujibu wa Scaroni, watajenga uwanja mpya wa kisasa zaidi.

Timu hizo mbili kwa muda mrefu zinautumia uwanja huo kwa pamoja.

“Kila kitu kinaendelea,” alisema Scaroni akiliambia Gazeti la La Gazzetta dello Sport kutoka Lausanne, ambako Kamati ya Olimpiki ilikuwa ikichagua mwenyeji wa michezo hiyo ya mwaka 2026, ambapo Jiji la Milan ni moja ya majiji yenye nafasi hiyo.

“Tutajenga uwanja mpya wa San Siro eneo lile lile.

“Uwanja huu wa sasa utabomolewa na pale pale tutajenga uwanja mwingine mpya.”



Muda wa kuanza na kukamilika kwa uwanja huo upya bado haujatajwa, lakini Scaroni anatumaini kwamba utakuwa tayari wakati wa sherehe za ufunguzi wa michezo ya Olimpiki mwaka 2026.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# 'MESSI, NEYMAR TATIZO MAKOMBE BARCA, PSG'

Ni makombe mangapi ya Ligi ya Mabingwa wameshinda na wanachosema ni mchezaji bora...

**Barcelona, Hispania**

Lionel Messi na Neymar wanapunguza mafanikio ya Barcelona na Paris Saint-Germain kwa sababu si "wachezaji wa kitimu", kwa mujibu wa kocha wa zamani wa 'Blaugrana' hao wa Camp Nou, Louis van Gaal.

Messi anachukuliwa kama mmoja wa wachezaji wa kiwango cha juu wa wakati wote, wakati Neymar ni mchezaji ghali zaidi katika historia ya soka, na bado Barca haikuweza kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu mwaka 2015. PSG, pia bado inasubiri kombe lake la kwanza katika michuano hiyo.

Na Van Gaal, ambaye aliifundisha miamba hiyo ya Camp Nou kuanzia mwaka 1997 hadi 2000 na 2002 hadi 2003, anasema wawili hao wanapaswa kubeba majukumu kwa kushindwa kwao.

"Itazame Barcelona. Ni makombe mangapi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wameshinda na wanachosema ni mchezaji bora duniani?" Aliliambia El Pais.

"Mtazame Neymar pale PSG. Ni makombe mangapi ya Ligi ya Mabingwa wameshinda? Ninampenda Neymar na Messi kama wachezaji binafsi lakini si kama wachezaji wa kitimu. Ninaamini hivyo katika mchezaji kitimu."

Kwa kupanua wazo lake, Van Gaal alimfananisha Messi na Neymar kiraka wa Liverpool asiyekubalika, James Milner.

"Miongoni mwa walio bora ni James Milner," alisema. "Katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, alicheza kama beki. Alikuwa mzuri kuliko ambavyo anaweza kukitoa katika umri wa miaka 33.

"Nadhani Messi anapaswa kujiuliza binafsi ni vipi inawezekana kutotwaa ubingwa wa Ulaya kwa kipindi kirefu namna hiyo.

"Sipo ama kwenye chumba cha kubadilishia au mazoezini Barcelona. Siwezi kuhukumu. Ninampenda Messi kama mchezaji binafsi. Yeye ndiye mchezaji binafsi bora zaidi duniani kwa sababu takwimu zake ni za kushangaza. Ninampenda.

"Lakini kwa nini hajatwaa Kombe la Mabingwa Ulaya tangu miaka mitano iliyopita? Kwa nini? Kama nahodha, lazima ujiulize binafsi kwa nini timu hajashinda michuano ya Ulaya.

"Barca ina kikosi cha kushangaza. Huwezi kusema kuwa [Ivan] Rakitic ni mbaya, ama kuwa [Philippe] Coutinho ni mbaya, au kuwa [Jordi] Alba ni mchezaji mbaya, au [Marc-Andre] Ter Stegen ni kipa mbaya, ama Arthur au [Arturo] Vidal.

"Nadhani Messi pia anahusika kwa kinachotokea Barcelona - na si kocha tu. Wachezaji wana sehemu kubwa ya wajibu wa kile kinachotokea katika timu."

Van Gaal hakuwa na wasiwasi mkubwa kwa taarifa ya Neymar kujiandaa kujiunga tena na Messi hapo Barca, lakini anahisi nahodha huyo wa 'Blaugrana' amepewa uhuru mkubwa sana na makocha wake.

"Ninakumbuka kuwa Neymar pale Barca alicheza kwa huduma ya Messi," kocha huyo wa zamani wa Manchester United pia, alisema. "Sipo dhidi ya Neymar. Ni wa kipekee. Lakini PSG, hachezi kwa ajili ya timu.

"Na ninaamini kila mchezaji lazima acheze kwa ajili ya timu - hata Messi. [Barcelona] ina wachezaji 30 na ninadhani Messi lazima azoee kwa timu na si vinginevyo vinavyomzunguka.

"[Pep] Guardiola alicheza kwa faida ya timu, lakini makocha wa hivi karibuni wamezoea sana kwa Messi badala ya kulinda roho ya timu. Hiyo ni muhimu zaidi. "

Akitathimini kipigo cha bao 4-0 Barca ilichokipata nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Liverpool, Van Gaal alisema: "Kama kuna moyo wa kweli wa kujitoa kwa timu, kwa kiwango cha juu matokeo haya hayawezekani."

Kwa PSG, aliongeza: "Hawana moyo sahihi wa kujitoa. Ni wazi. Nimewaona pale Parc des Princes siku wakiichapa Bayern 3-0 kwenye Ligi ya Mabingwa mwaka 2017.

"Niliwaona uwanjani: wachezaji wenzake hawakuwa ni wenye furaha na staili ya uchezaji ya Neymar. Na bado hawa furaha."

## KWA UFUPI

### TIERNEY KUKAMUA BAJETI ARSENAL
ARSENAL itapaswa kutumia nusu ya bajeti yao ya usajili majira haya ya joto ili kuipata saini ya beki wa Celtic, Mscotland Kieran Tierney, 22, wakati huu beki huyo wa kushoto akithaminishwa na pauni milioni 25 na mabingwa hao wa Scotland. ***(Telegraph)***

### UNITED KUMPANDIA DAU MAGUIRE
MANCHESTER United ipo tayari kulipa dau kubwa zaidi ya Manchester City katika harakati za kuipata saini ya beki wa kati wa Leicester City, Harry Maguire, 26, lakini nyota huyo wa kimataifa wa England anapendelea zaidi kutua kwa mabingwa City. ***(Sun)***

### KOVACIC HAKIJAELEWEKA CHELSEA
MUSTAKABALI wa baadaye wa kiungo Mcroatia Mateo Kovacic, 25, hapo Chelsea haueleweki, na mkataba wake wa mkopo akitokea Real Madrid ukimalizika Julai Mosi, mwaka huu. Wakali hao wa Stamford Bridge bado hawajampa ofa ya mkataba mpya. ***(Goal)***

### PSG YATAKA NEYMAR, POGBA KUPISHANA
PARIS St-Germain imeipa ofa Manchester United uwezekano wa kufanyika dili la kubadilishana wachezaji, mshambuliaji Mbrazil Neymar, 27, kwa kumpata kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26. ***(Independent)***

### CARRASCO AVUTIWA PUMZI ARSENAL
ARSENAL bado inavutiwa na saini ya winga wa Dalian Yifang, Yannick Carrasco, lakini bado haijatoa ofa kwa nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji. ***(Football.London)***

### MRITHI WA BENITEZ KUWAHISHWA
NEWCASTLE United inatumai kuwa na mrithi wa Rafael Benitez kwa wakati pindi itakaposafiri kwenda China katika michuano ya Premier League Asia Trophy kwa zaidi ya wiki mbili. ***(Telegraph)***

### MADRID YATAJA DAU LA CEBALLOS
REAL MADRID haitakuwa tayari kusikiliza ofa chini ya pauni milioni 47.7 kwa kiungo Mhispania Dani Ceballos, ambaye anawindwa na Tottenham. ***(AS- in Spanish)***

### MIGNOLET ASUBIRISHWA LIVERPOOL
LIVERPOOL inatarajia kipa Mbelgiji Simon Mignolet atabaki klabuni hapo vinginevyo labda ofa itue mezani kwao jambo ambalo ni jema kwa klabu na mchezaji husika. ***(Times)***

### ARSENAL YAIGOMEA TORREIRA MILAN
ARSENAl inakataa wazo la AC Milan la kumnunua kiungo wa kimataifa wa Uruguay, Lucas Torreira, 23. ***(Mirror)***

### SARRI KUANZA NA TRIPPIER JUVE
KOCHA mpya wa Juventus, Maurizio Sarri amemtaja beki wa kulia wa Tottenham, Kieran Trippier, 28, kama mchezaji wa kwanza anayetaka kumsainisha mkataba, lakini anakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka kwa Napoli ambayo tayari imeshatupa ndoana zake. ***(Mirror)***

### RODRIGUEZ HANA UHAKIKA MADRID
MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Mcolombia James Rodriguez, ambaye amecheza kwa misimu miwili kwa mkopo Bayern Munich, hana uhakika kama atakuwapo Bernabeu msimu ujao. ***(Marca)***

### LIVERPOOL KUANZA NA DEN BERG
USAJILI wa kwanza Liverpool majira haya ya joto utakuwa ni kwa beki wa kati wa FC Zwolle, Sepp van den Berg, 17, ambaye pia anazivutia Ajax, Bayern Munich na PSV Eindhoven. ***(Mail)***

### ZOLA ASIKILIZIA KOCHA MPYA CHELSEA
KOCHA ajaye wa Chelsea atakuwa na nafasi ya kumbakisha Gianfranco Zola, ambaye alikuwa kocha msaidizi wa Maurizio Sarri msimu uliopita, kama sehemu ya benchi la ufundi la timu hiyo. ***(Express)***

HABARI MICHEZO

# MWAKYEMBE AGEUZIA LAWAMA SIMBA, YANGA KIPIGO TAIFA STARS

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

HUKU akitupiwa lawama bungeni kwa wizara yake kushindwa kwenda Misri kuipa hamasa timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, amegeuzia lawama za kipigo cha Stars dhidi ya Senegal kwa Simba na Yanga.

Kufungwa kwa timu ya Taifa Stars katika mchezo wake wa kwanza Afcon dhidi ya Senegal, kumeibua mvutano bungeni jana baada ya wabunge kuonyesha hisia zao huku wakitaka serikali ihakikishe inatenga bajeti kwa timu hiyo.

Katika mechi iliyochezwa Jumapili nchini Misri, timu hiyo ilichezea kichapo cha mabao 2-0 kutoka Senegal jambo ambalo wabunge walihoji ni kwa nini Waziri na Naibu wake wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Sanaa na Michezo hawajaenda nchini Misri kushuhudia kinachoendelea kwa timu hiyo.

Mvutano huo uliibuka jana bungeni mara baada ya kumalizika kwa kipindi cha maswali na majibu, ambapo Mbunge wa Rombo (Chadema), Joseph Selasini aliomba mwongozo kwa spika akitaka apewe majibu ni kwanini waziri na naibu wake katika wizara hiyo wapo nchini.

Katika mwongozo wake, Selasini alisema timu ya taifa inaibeba nchi na kama alivyokuwa Misri, Spika Job Ndugai na viongozi mbalimbali, lakini waziri na naibu wake wapo nchini na kwamba kisaikolojia katika hali ya kawaida si sawa.

Kutokana na hoja hizo, Spika Ndugai alimwomba Waziri Mwakyembe kutoa maelezo, alisema kutokana na timu ya taifa kutokuwa na bajeti hivi karibuni aliandaa harambee ya kuichangia iliyoongozwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Kuhusu kocha wa timu hiyo, Emanuel Amunike, Mwakyembe alisema kunatakiwa kuwe na mjadala mpana baada ya kukamilika kwa michuano ili wasiwakatishe tamaa wachezaji.

Na kwa upande wa kipigo hicho, Mwakyembe alisema kinachoiumiza timu hiyo ni wachezaji wa kigeni kuwa wengi katika timu za Simba na Yanga.

"Timu zetu kubwa za Simba na Yanga ambazo ndizo zinazozalisha wachezaji zinategemea wachezaji wa nje kwa ajili ya 'midfield' (kiungo)," alisema.

Kutokana na majibu hayo, wabunge walianza kupaza sauti wakionyesha kupinga alichokisema Waziri Mwakyembe wakimtaka aeleze kwa nini hakwenda Misri.

Spika aliwataka wabunge watulie wamsikilize waziri ambapo Mwakyembe aliendelea kusema kuwa taifa liliwakilishwa na mmoja ya viongozi waandamizi ambaye ni Spika wa Bunge.

"Na mimi ndio maana nikaona niwakilishwe na ujumbe kutoka TFF na Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Michezo (BMT) mchango wake ulikuwa mkubwa kuliko hata mimi na wewe ulikuwapo uliona," alisema.

Baada ya Mwakyembe kutoa maelezo hayo, Mbunge wa Mlimba (Chadema), Susan Kiwang, aliomba kumpa taarifa Waziri Mwakyembe ambapo alisema hali ya kambi ya timu ya taifa haikuwa nzuri na bila ya juhudi za watu binafsi hali ingekuwa mbaya zaidi kwa kuwa hakukuwa hata na bendera za Taifa.

Spika Ndugai alihitimisha kwa kumuomba Waziri Mkuu asimamie ili Waziri Mwakyembe aende Misri kwa ajili ya kuangalia kambi ya Taifa Stars.




Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mnigeria Emmanuel Amunike, akizungumza na waandishi wa habari jijini Cairo, Misri jana. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Amunike: Ni ushindi tu kwa Harambee Stars

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

WAKATI Rais Magufuli akiwataka wachezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) kutokata tamaa, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Emmanuel Amunike, amesema anahitaji ushindi tu kuelekea mechi ya Kundi C ya fainali za Kombe la Mataifa Afrika (Afcon) 2019 dhidi ya Kenya (Harambee Stars), itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa June 30 jijini hapa.

Rais Magufuli alisema jana kuwa ushindi wa Taifa Stars ni ushindi wa Tanzania, na anawataka wachezaji kujituma zaidi ili kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo wa pili dhidi ya Harambee Stars.

"Kawaambie wasikate tamaa, wakajitume zaidi, ndani ya uwanja wa mpira kuna kushinda na kushindwa, kushinda kwao ni kwetu," alisema Rais Magufuli wakati anampa ruhusa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuifuata Stars Misri.

Akizungumza jana jijini hapa, Amunike, alisema kuwa timu yake imejiandaa kupata ushindi katika mchezo huo, na hii inatokana na changamoto zilizojitokeza wakati wanavaa Senegal kumalizika.

Amunike, mchezaji wa zamani wa Barcelona ya Hispania, alisema anafahamu pia, Harambee Stars nao wamejiandaa kupata ushindi katika mchezo huo, hivyo mechi hiyo haitakuwa rahisi kwa kila upande.

"Hii ni nafasi nzuri kwetu, kwa timu zote mbili, sisi ni majirani na tunajuana, kikubwa ni kujiweka sawa kuhakikisha tunashinda mechi hii ya pili, wametuangalia na sisi tumewaangalia pia, ni mechi itakayokuwa na changamoto za kiufundi zaidi," alisema Amunike.

Mnigeria huyo alisema kuwa kila timu inahitaji kuona inapata mafanikio katika mashindano haya ambayo mwaka huu nchi zote zimeonekana kuimarika kutokana na kujiandaa vema kabla ya kuanza kwa fainali hizi.

"Kila timu inahitaji kupata ushindi, tunataka kushinda, hakuna ambaye amekuja hapa kwa ajili ya kupoteza, kitu muhimu ni kuhakikisha tunakuwa watulivu, hizi ni fainali ngumu na si nyepesi kama baadhi wanavyoyatizama," alisema Amunike.

Aliongeza kuwa bado tunahitaji kupata muda wa kuendeleza timu yetu baada ya kufanikiwa kufuzu kushiriki fainali hizi.

"Jambo muhimu si kufuzu tena, sasa hivi tunatakiwa kuangalia hatima yetu, siku zinakwenda, tunatakiwa tuangalie ni namna gani tutawaandaa wachezaji chipukizi kwa ajili ya fainali zijazo, hapo timu tutakayoiandaa itakuwa imepata uzoefu," Amunike alisema.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Simon Msuva, anayecheza soka la kulipwa Klabu ya Difaa Hassani El-Jadidi ya Morocco, alisema mchezo dhidi ya Senegal ulikuwa ni "mkubwa" kwao, lakini anaamini hali itakuwa tofauti wakati wanaikabili Harambee Stars hapo kesho.

"Hii ndio nafasi ya kuonyesha uwezo wetu, itakuwa ni mechi ya kufa au kupona, tunaamini tutawapa furaha Watanzania," Msuva alisema.

## Misri yaihofia DR Congo leo

**Na Somoe Ng'itu, CAIRO**

BAADA ya kupata ushindi kiduchu katika mechi ya kwanza, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Misri, Javier Aguire, amesema kuwa kikosi chake kitaingia kwa tahadhari katika mchezo wao dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Cairo jijini hapa.

Misri ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Zimbabwe katika mechi ya ufunguzi wa fainali za Kombe la Mataifa Afrika zinazoendelea nchini hapa wakati DRC wao walichapwa mabao 2-0 dhidi ya Uganda (The Cranes).

Akizungumza jana jijini hapa, Aguire, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu wanakutana na timu iliyopoteza mechi yake ya kwanza na sasa wanataka kufufua matumaini ya kusonga mbele.

Aguire alisema amewaandaa wachezaji wake kucheza kwa tahadhari, kwa sababu wanahitaji kushinda na kujihakikishia tiketi ya kusonga mbele kwenye fainali hizi.

"Hakuna mechi rahisi, hasa unapocheza na timu iliyotoka kupoteza mchezo, tutakuwa makini kuhakikisha tunashinda, ninajua tukishinda mechi hii tutakuwa tumejihakikishia nafasi ya kutinga hatua inayofuata," alisema Mfaransa huyo.

Kocha wa DRC, Florente Ibenge, alisema kuwa wamejipanga upya kuhakikisha wanapata ushindi na wamewataka wachezaji wake wasahau matokeo ya mchezo uliopita.

## Usajili Mtibwa kuishia U-20

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI klabu mbalimbali zikizidi kujiimarisha wakati huu wa dirisha la usajili, uongozi wa Klabu ya Mtibwa Sugar yenye makao yake makuu Turian mkoani Morogoro, umesema hawatatoka nje na badala yake watapandisha yosso wao wa umri chini ya miaka 20 (U-20) kukisaidia kikosi hicho kwenye msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, msemaji wa timu hiyo, Thobias Kifaru, alisema kwa mujibu wa Kocha Mkuu, Zuberi Katwila, ameridhishwa na kiwango kilichoonyeshwa na timu ya vijana katika mashindano ya U-20 na kudai hana muda wa kutoka na kwenda kusajili wachezaji kwenye klabu nyingine wakati kuna vijana wenye uwezo mkubwa.

"Hivi karibuni uongozi wetu ulikuwa unawafanyia sherehe vijana wetu baada ya kuibuka tena mabingwa kwenye mashindano ya vijana na kocha alikiri kuongeza wachezaji kutoka kwenye timu yake ya vijana badala ya kwenda kuhangaika kusaka wachezaji kwenye timu nyingine," alisema Kifaru.

# Michezo

Jumatano Juni 26, 2019

Nipashe




‘Messi, Neymar tatizo makombe Barca, PSG’ HABARI UK 30

**MBRAZIL TENA...**




Mbrazil Gerson Fraga Vieira akitia saini mkataba huku Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Simba, Zacharia Hans Poppe (kushoto) akishuhudia. **PICHA: SIMBA**

# MBRAZIL VIEIRA NAYE AJIFUNGA RASMI SIMBA

## Ni beki kisiki aliyeichezea Brazil Kombe la Dunia U-17 pamoja na Neymar, Coutinho, huku pia akimudu...

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya wiki iliyopita kutangaza kuinasa saini ya mshambuliaji kutoka Brazil, Wilker Henrique da Silva, hatimaye mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Simba wamezidi kujiimarisha zaidi kuelekea msimu mpya kwa kufanikiwa kumsainisha Mbrazil mwingine, safari hii ikiwa ni beki wa kati, Gerson Fraga Vieira.

Vieira, 26, ambaye anamudu pia kucheza nafasi ya kiungo mkabaji anaungana na Da Silva wote kila mmoja akitia saini mkataba wa miaka miwili wa kuwatumikia mabingwa hao mara mbili mfululizo wa Ligi Kuu Bara.

Usajili wa Vieira ulitangazwa jana kupitia ukurasa wa Instagram wa Simba ambapo picha za Mbrazil huyo ziliwekwa akiwa anatia saini mkataba mbele ya Mwenyekiti wa Kamati ya Usajili ya Simba, Zacharia Hans Poppe.

Huo unakuwa usajili wa tatu mpya kwa wachezaji wa kigeni ikiwa ni baada ya wiki iliyopita pia kuinasa saini ya kiungo mkabaji, Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman kutoka Klabu ya Al Hilal ya Sudan.

“Mchezaji mwingine kutoka Brazil mwenye uwezo mkubwa wa kucheza nafasi ya beki wa kati na kiungo mkabaji, Gerson Fraga Vieira (26), ametia saini mkataba wa miaka miwili na mabingwa wa nchi.

“@g.fragav ambaye amewahi kuwa nahodha wa timu ya Taifa ya wachezaji wa chini ya miaka 17 ya Brazil iliyokuwa na wachezaji maarufu kama Neymar, Philippe Coutinho, Casemiro na golikipa Alisson, pia alicheza timu ya taifa ya wachezaji chini ya miaka 20 na alicheza klabu kadhaa za Brazil ikiwepo Gremio, amejiunga na klabu yetu akitokea ATK FC ya India,” ilisomeka taarifa ya Simba ambayo iliambata na mchezaji huyo akisaini mkataba.

Vieira aliyezaliwa Oktoba 4, 1992, wasifu wake wa juu kimataifa ni kuichezea timu ya Taifa ya Brazil U-17 kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2009 na aliendelea kwa kuitumikia jumla ya mechi 14.

Mbali na ATK ya India na Gremio ya Brazil aliyoichezea mwaka 2012-2016, pia ameichezea kwa mkopo Oeste (2012), Red Bull Brasil (mkopo- mwaka 2014) na kuifungia bao moja, Atenas (mkopo) 2014-2015 akaifungia bao moja pia.

Msimu wa 2015/16, akaichezea Red Bull Brasil kwa mkopo kisha mwaka 2016 akatua Mumbai City ya India na kufunga bao moja kabla ya mwaka 2017 kuichezea Atletico Tubarao akifunga bao moja pia katika mechi 14.

Msimu wa 2017/18, alirejea Mumbai City na kufunga bao moja katika mechi 17 na mwaka 2018 akatua Renofa Yamaguchi kabla ya mwaka huo kutua ATK na sasa Simba.

## JPM atoa neno kipigo cha Stars

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amekizungumzia kipigo cha mabao 2-0 ilichokipata Taifa Stars dhidi ya Senegal mjini Cairo Jumapili, huku akimtuma Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda kwenda Misri kwa kazi maalumu ya kuhamasisha ushindi katika mechi ijayo.

Taifa Stars inatarajia kucheza mechi yake ya pili ya Kundi C kesho dhidi ya Harambee Stars ya Kenya katika michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, inayoendelea nchini Misri.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Rais Magufuli aliwataka Watanzania wasimame kuisaidia na kuendelea kuiombea timu hiyo kwa sababu hata huo mwanzo walioanza nao siyo mbaya.

“Kufungwa tugoli tuwili tu (anatabasamu) kwa timu inayoongoza Afrika na ambayo wachezaji wote wanacheza nje, nawasihi tuendelee kuwapa moyo,” alisema.

Rais Magufuli alitoa kauli hiyo baada ya awali, Makonda kumuomba atoe neno moja kwa timu hiyo ili kuitia nguvu kwa sababu baada ya kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Senegal, wapo waliowabeza wachezaji usiku kucha kwenye mitandao ya kijamii.

Aidha, Makonda alimuomba Rais Magufuli kama itampendeza naye aende Misri kwa ajili ya kuhamasisha ushindi dhidi ya mechi ya kesho. Rais Magufuli akimjibu Makonda, alisema anajua amechomekea suala hilo, lakini lengo lake ni kutaka kwenda Misri.

“Najua Makonda amechomekea anataka kwenda Misri, nilijua anaomba kwenda huko, ninakuruhusu nenda, si umesema ukienda tutashinda, basi nenda sisi wote tunataka kushinda,” alisema.

Rais Magufuli alimtaka Makonda akapande ndege siku hiyo hiyo na atakapofika Misri awaeleze wachezaji kuwa wasikate tamaa kwa sababu kwenye uwanja wa mpira kuna kushinda na kushindwa.

“Wakakazane, wakajitume zaidi, sisi tuendelee kuwaombea kwa sababu kushindwa kwao ni kushindwa kwetu Watanzania na kushinda kwao ni ushindi wa Watanzania,” alisema.

Aidha, aliwataka Watanzania wasimame kuendelea kuwasaidia na kuwaombea kwa sababu ana uhakika hata huo mwanzo siyo mbaya.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >